Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 22 Julai, 2013

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 – Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea na ninayo idadi nzuri sana. Wajumbe ambao wanataka kuchangia, nafikiri hawa kufuatana na shughuli zetu zilivyo wanatosha. Kwa hivyo, tunakusudia kuendelea na majadiliano mpaka saa 5:00 Waziri yeye alikuwa yuko tayari kufanya majumuisho kuanzia siku ya Ijumaa saa 5:00, aliniandikia nikamwambia basi subiri kidogo tutafanya saa 5:00 ya siku ya Jumatatu yaani leo.

Kwa hiyo, wataopata nafasi ya kuchangia Mungu akipenda watakuwa ni pamoja na Mhe. Abdi Mossi Kombo, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Salma Mussa Bilali, Mhe. Salma Mohamed Ali, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi pamoja na Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Amina Iddi Mabrouk na mwisho itakuwa Mhe. Nassor Salim Ali. Basi tumkaribishe Mhe. Abdi Mossi Kombo, yuko wapi? Hayupo, ndio imekwenda hiyo.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia akatufikisha asubuhi hii tukiwa tumo ndani ya hali ya uzima na afya njema. Pia naomba nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ikiwa ni wa mwanzo katika kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa siku ya leo nakushukuru sana kwa hilo.

Mhe. Spika, kwanza sina budi pia nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake na jukumu hili walilonalo la kuwawezesha wananchi wetu wa Zanzibar kiuchumi, pia na ushirika ikiwa ni moja ya mashirikiano makubwa baina ya watu na serikali yao.

Mhe. Spika, nikianza katika mchango wangu nianze katika utekelezaji wa malengo ya Sera na Utafiti. Mhe. Waziri ameeleza hapa kuwa katika taasisi yoyote suala la ufuatiliaji na tathmini lina nafasi muhimu katika kuhakikisha mipango inayotekelezwa inaleta matokeo yanayotarajiwa. Mheshimiwa hili ni kweli na kwa kuliona hili wizara hii basi nichukue fursa hii kuwapongeza sana. Kwa sababu suala lolote ambalo litakuwa halina ufuatiliaji, halina mpango madhubuti wa tathmini yake basi huwa suala hilo halina umadhubuti wala halifikiwi lengo linalokusudiwa. Kwa hivyo, kwa hili naomba niwapongeze sana wizara hii kwa kuliona hili.

Lakini Mhe. Spika, Wizara hii ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hakuna tofauti baina ya wizara hii na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, wanawake na Watoto. Hizi ni wizara ambazo kazi zao zote wanakwenda sambamba, lakini cha muhimu ni kuweka mashirikiano makubwa ili hii azma na lengo wanalokusudia kuwawezesha hao wananchi kiuchumi liweze kufikiwa.

Mhe. Spika, ukiangalia kitabu cha Mhe. Waziri wa Kazi na Waziri wa Ustawi wa Jamii yaliyomo humu yote ndiyo anayoyazungumzia yeye. Sasa wizara hizi mbili zitakaposhirikiana kama wana nia madhubuti ya kuwawezesha wananchi kiuchumi basi itafikiwa lengo, kwa sababu Waswahili wanasema: **"***Mmoja hapotei njia, lakini wawili waganga njia***"**.

Kwa hivyo, ni mashirikiano makubwa baina ya Wizara hizi katika kufikia hili lengo. Kwa sababu ajira za watoto ukienda kwa Mhe. Zainab ziko na ukija kwa Mhe. Haroun Ali ziko, vikundi tele vipo. Sasa muhimu ni mashirikiano kati ya wizara hizi mbili kukutana wakapanga namna gani ya kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi na ushirika.

Mhe. Spika, nikienda katika ukurasa wa 28 kuna kupambana na ajira mbaya za watoto. Mheshimiwa katika kitabu chake hapa amesema kuwa, mradi huu

ambao utekelezaji wake umeanza mwaka 2012 unatekelezwa katika shehia 50 za Zanzibar, Unguja 25 na Pemba 25. Katika kipinchi cha mwaka 2012/2013 mradi huu umefanikiwa jumla ya shehia kazitaja Mhe. Spika, hapa shehia ambazo zimetekelezwa katika kupambana na ajira mbaya hizi za watoto.

Mhe. Spika, ajira mbaya za watoto ni ajira ambazo kitabu hiki au kabla ya wizara hii kuanzishwa hili suala lipo linazungumzwa kupitia ajira hizi mbaya. Nataka nichukue fursa hii kuwapongeza Shirika la Kazi Duniani tangu kuanzia mwaka 2000 nafikiri kazi hii wameshaianza. Na walionesha juhudi nzuri tu katika kulifanyia utafiti suala hili na kuziondoa hizi ajira mbaya za watoto. Lakini ndio pale tunaposema mwanzo kwamba suala la ufuatiliaji wa tathmini lilikuwa haliko, kwa sababu kama kulikuwa kuna ufuatiliaji na tathmini na udhibiti hasa wa suala hili la ajira za watoto, basi mpaka kufikia leo hii ingelikuwa ni asilimia kubwa ya watoto ambao wanaondokana na ajira hizi mbaya.

Lakini kutokana na hilo, Mheshimiwa mpaka hivi leo imeanzishwa tena wizara hii na inaendelea na shughuli hii. Lakini walipoifanya kipindi hicho walikuwa hawafuatilii kupitia wale wazazi wao, ilikuwa ni kuwachukua watoto kuwarudisha skuli, kuwapeleka skuli mbadala na kuwapa sare na mabuku kwenda skuli, lakini hili lilikuwa halitoshi, kwa sababu ilikuwa tutizame tatizo ni nini? Haiwezekani mtoto mdogo aende akatafute ajira ambazo hazimhusu isipokuwa kuna sababu au kuna chanzo nyuma yake kinachosababisha afikie pale.

Nashukuru mara hii kuwa wizara hii imeona kwamba kuna jumla ya familia 381 ambazo watoto wamerejeshwa skuli walio katika mazingira ya kujiingiza katika ajira hizo. Pia kuwa hawa wazee wao angalau kufanyiwa masuala ya kujiendeleza kwa namna ya kuwahifadhi wale watoto wao. Sasa hili ni jambo zuri na nadhani tukifanya hivi itatusaidia sana kuliko kuwachukua tu watoto tukawarudisha skuli lakini familia hatujui zina mazingira gani.

Sasa Mhe. Waziri mimi hapa nimuombe badala ya kufanya haya kama keshafanya pengine kitabu sijakisoma vizuri, lakini namuomba aanzishe kamati za kudhibiti hasa hawa watoto wanaojiingiza katika ajira hizi za watoto. Kamati zile utakapozielimisha wewe na wale watakapofanya tathmini ya mle kwenye shehia zao si lazima shehia zote za Unguja au za Zanzibar, waangalie katika zile shehia ambazo zimo ajira hizi za watoto ambazo zimekithiri kwa kiasi fulani ataanza kufanya majaribio.

Kamati zile atakapoziunda watamsaidia yeye kazi na kufuatilia utaratibu mzima na mwenendo ili kudhibiti kuwa badala ya kufanyiwa kazi hizi ajira zisirejee.

Mhe.Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kama hilo hajalifanya basi atafute shehia ambazo zina watoto wengi waliokuwa na ajira hizi mbaya kuanzisha kamati kama alivyofanya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii katika kuunda kamati zake za udhalilishaji wa kijinsia katika shehia. Kwa hivyo, na hili naye namuomba Mhe. Waziri alione ili kuondoa kero hii ya ajira za watoto ili kufikia lengo katika Kisiwa chetu cha Zanzibar.

Lakini watoto hao pia si hizi ajira mbaya ambazo wanazo, lakini pengine hata hicho kipato chao wanacholipwa ni watu ambao pengine wanawatumikisha ajira hizi basi hazikidhi haja. Mheshimiwa hili ni suala la kulifuatilia sana kwa sababu wamo hao watoto wengine ambao pengine washakuwa hawarejesheki skuli hizo ajira zao wanazozifanya basi matajiri wale huwafanyisha kazi ngumu na hatimaye kipato chao huwa ni kidogo sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili suala atakapolifanikisha namuomba sana hizo kamati azifuatilie mwenendo wake ili tufanye udhibiti wa hizi ajira badala ya kuongezeka siku zote tunazungumza ajira za watoto lakini hatimaye tunafikia kuwa ajira zile zinaendelea.

Mhe. Spika, nikiendelea hapa ukurasa wa 52 nataka niulize swali kidogo katika malengo ya Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Katika malengo ambayo amekusudia moja ni kutanua soko la bidhaa za wajasiri amali wadogo wadogo. Sasa hili soko silijui liko wapi, nakumbuka kuwa kumeanzishwa haya masoko ya Jumapili moja iko pale Chake Chake *Barclays* na hapa Unguja sijui iko maeneo gani. Sasa hili soko analokusudia kwa wajasiri amali wadogo wadogo aje anipe ufafanuzi ili kujua na mimi soko liko pahala gani.

Jengine Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 60 kwenye Idara ya Ushirika. Mhe. Spika, hapa mimi nataka nipate ufafanuzi katika viambatanisho hivi katika masuala mazima ya mikopo. Katika kiambatanisho Nam. 4 kinaonesha utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Kujitegemea nafikiri ni ule wa AK na JK.

Mhe. Spika, marejesho ya fedha ya malipo ya Mfuko wa kujitegemea Julai, 2012 – Julai, 2013 hapa ukiangalia kwenye hiki kiambatanisho yalikwenda vizuri mikopo hii ilipotolewa na kwa kiasi fulani watu wamerejesha. Lakini ukiangalia kiambatanisho Nam, 7 chini hapa kuna urejeshaji wa mikopo naona kuna Wilaya ya Micheweni ambapo fedha zilizolipwa katika Juali, 2012 – Mei, 2013 kwa Wilaya ya Micheweni inaonekana kama hakuna fedha iliyorejeshwa.

Sasa Mhe. Waziri nataka aje anieleze kwa sababu huku anaonesha kuwa kiambatanisho hiki walikuwa wanarejesha vizuri, lakini kiambatanisho hiki hapa chini ina maana huu karibu mwaka mzima mikopo hii haijarejeshwa.

Kwa nini au ni sababu zipi pengine zinazowakwaza mwanzo wakaanza vizuri lakini hatimaye huku wakafika pahali wakakwama katika suala hili.

Pia Mhe. Waziri suala zima hili la mikopo linataka taaluma ya hali ya juu sana, kwa sababu *SACCOS* nyingi zishakwama kupitia suala la mikopo, badala ya watu kuchukua mikopo watu hawairejeshi. Na hii mikopo ya AK na JK ilifika pahali hata ukienda benki basi ukiwauliza wanasema kuwa kuna tatizo la urejeshaji wa mikopo. Lakini pia linaonekana kuwa hili suala linaendelea kutolewa hii mikopo. Sasa mimi kiambatanisho hicho Mhe. Waziri naomba aje anieleze ili nipate ufafanuzi zaidi.

Jengine Mhe. Spika, Kamisheni ya Kazi. Kamisheni ya Kazi nayo pia inataka jamii kupatiwa elimu. Mhe. Spika, kunajitokeza changamoto nyingi sana ambazo kuwa watu zinapokuja kampuni wanajipeleka kutafuta kazi lakini hatimaye hufikia pahali wakakwama kutokana na hali ya kuwa hawajui mambo ya mikataba wala chochote. Wao wanajiingiza wakati wanatafuta rizki, wanapokwenda popote pale wanajiingiza katika sehemu hizo hatimaye hutokea migogoro katika suala zima la mikataba. Mhe. Spika, hili hata serikali nao wanachangia.

Kwa sababu kuna mfano mmoja ulio hai, kulijengwa soko la samaki kule Tumbe hatimaye kampuni ile iliyoletwa pale inasumbua watu kupita kiasi, sasa wao jamii pale wakiona kuwa tayari ile ni *tender* imekuja watu wanatafuta kazi watakwenda hawajui mikataba yoyote iliopo pale, wanakwenda kutafuta kazi kutegemea kuwa madhali kampuni hii imeingiliana na serikali kwa hali yoyote hapawezi kutokea machafuko. Lakini la kusikitisha Mhe. Spika, kampuni ile imefanyisha watu kazi pale mpaka leo hii soko limemalizwa kujengwa japokuwa si soko si wazimu, ni bovu, lakini kuna watu ambao walishindwa kulipwa mpaka leo hii karibu mwaka sasa hii ni usumbufu.

Sasa ina maana serikali wao wanapoleta zile kampuni wanashindwa kuwapa elimu wananchi wake ili kujua namna gani ya kuweza kujiingiza katika ajira zile japo kuwa ni umasikini unaowaingiza lakini pia wakajua hapa panaendeka au hapaendeki. Mhe. Spika, hili linataka usimamizi wa hali ya juu ili wananchi wetu zinapokuja hata hizo kampuni basi serikali nayo iweze kutoa elimu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache mimi nasema naunga mkono hoja kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Micheweni kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwaombe radhi kuna baadhi ya wachangiaji waliomba mapema na wakasema kwamba wangechangia leo, sasa nilimsahau Mhe. Ashura Sharif Ali na Mhe. Fatma Mbarouk Said. Kwa hivyo nimkaribise sasa Mhe. Farida Amour Mohammed na baadae Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia machache katika Hotuba ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametulaza na kutuamsha tukiwa hai na afya njema mpaka kufikia kuja kusimama katika Baraza lako tukufu na kufanya wajibu wetu. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri katika wizara hii pamoja na watendaji wake jinsi wanavyofanya shughuli zao, pia nimpongeze kwa dhati kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii kwa muda mfupi na ikaeleweka.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwenye kiambatanisho Nam. 5 ukurasa wa 108 Utoaji wa Mikopo ya AK na JK. Katika maelezo yake hapa Mhe. Waziri aliingiza hii kwamba kuna Mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya ya Kaskazini Unguja imepata mikopo hii. Sasa hapa kidogo nataka kuuliza swali ili na mimi nipate kuelimika zaidi. Je, Mikoa ya Kusini Unguja, Kusini na Kaskazini Pemba itafaidika lini na mikopo hii, au walitumia vigezo gani hawa wenzetu wakapata mpaka ikawa mikoa hii ya Kusini Unguja, Kusini Pemba na Kaskazini Pemba ikawa haijapata.

Sasa naomba Mhe. Spika, niende katika Wizara ya Kazi. Wizara ya Kazi Mhe. Spika, nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa sababu inafanya kazi zake vizuri sana na inajishughulisha. Lakini kwenye suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi Mhe. Spika, kunahitaji elimu kubwa kama alivyotangulia mwenzangu hapa, kuzungumza kuwa elimu ni muhimu na baada ya kupata elimu wananchi wetu ndio watakapoelimika zaidi hasa wanawake, ili kufanikiwa na kupewa msukumo zaidi.

Mhe. Spika, katika hapa namuomba Mhe. Waziri atumie zaidi utaalamu, wataalamu kuwafunza hao watu wetu hasa wanawake, nikisema hasa wanawake Mhe Waziri asinielewe vibaya kwa sababu ukimsaidia mwanamke mmoja unaisaidia jamii. Sasa namuomba sana katika hili kwa kazi zake alizonazo na uhodari wake wote anaoufanya. Kwa hivyo, suala zima kwanza liwe la elimu kuwapa elimu watu wetu ili wapate msukumo zaidi na kuangaliwa.

Mhe. Spika, elimu ni muhimu ili watu wetu wafaidike kiuchumi. Kwa sababu kama huna elimu huwezi kufaidika kiuchumi. Kuna watu hawajui maana ya uchumi, hawajui maana ya chochote, hiyo kuwezeshwa hawajui nini maana yake, sasa lazima kwanza tupate elimu.

Mhe. Spika, suala jengine nije kwenye ujasiri amali. Mhe. Spika, ujasiri amali ni dhana mpya kwa jamii yetu, bado nalo linahitaji taaluma ili wananchi wetu wafikie yale malengo. Kwa sababu ujasiri amali huwezi kuupata, huwezi kujifunza vizuri, huwezi kupata zile bidhaa zako lazima upate elimu kwanza. Kwa hivyo, kila nitakapozungumza nitashadidia sana suala la elimu.

Mhe. Spika, ndani ya Wilaya yangu ya Wete kwa umuhimu wa elimu ulivyo kuna kikundi maana yake wananchi wa Wilaya ya Wete katika Jimbo la Gando wamepata elimu ndogo sana katika ujasiri amali, lakini elimu hii waliyoipata wanaitumia vizuri wajasiriamali hao wa Jimbo la Gando, wanazalisha bidhaa nzuri ni wa kupigiwa mfano Mhe. Spika.

Mhe. Spika, wajasiri amali hawa wana vikundi vyao na wanazalisha bidhaa mbali mbali tena nyingi. Sasa ninalomuomba Mhe. Waziri avitembelee vikundi vyangu hivi vilivyomo ndani ya Jimbo la Gando Wilaya ya Wete ili aone ile juhudi yao waliyoifanya na yeye ajue nini cha kuwasaidia.

Mhe. Spika, katika hilo pia naomba nimshauri Mhe. Waziri, katika wajasiri amali hawa baada ya juhudi kubwa wanazozifanya naomba awafanyie mpango mmoja mmoja Mhe. Waziri wa kuwatafutia vifunganishi. Kwa sababu vifunganishi ni muhimu kwa bidhaa hizi. Lakini cha kusikitisha wajasiri amali wa Zanzibar wanachukua vifunganishi hivyo Tanzania Bara au Kenya tena kwa bei kubwa mno. Sasa watakapofanyiwa mpango wakapata vifunganishi kwa bei nafuu na bidhaa zao zitapendeza na zitapata bei watauza na ule usumbufu utapungua.

Mhe. Spika, katika hili pia naomba Mhe. Waziri nimshauri ushauri mwengine, tuanzishe mitaala ya ujasiri amali ndani ya skuli zetu. Kwa sababu tukianzisha mitaala ya ujasiri amali ndani ya skuli zetu za Zanzibar kuanzia msingi hadi Chuo Kikuu basi nina imani wajasiri amali wetu watafanikiwa watajua jinsi ya kujifunza namna ya uzalishaji kuanzia mapema, watajua namna ya kufanya viwanda vidogo vidogo na mambo mengineyo. Kazi hii itakapofanikiwa Mhe. Spika, tutaipunguzia sana serikali mzigo mkubwa wa kuajiri watu watajiajiri wenyewe, lakini kama hakutakuwa na mpango maalum wa kuwafunza basi tutaipa mzigo serikali.

Kwa mfano, mimi nilipokuwa mwanafunzi nakumbuka tulipokuwa skuli kulikuwa na somo la ujasiri amali, ilikuwa kila siku kuna uzalishaji mali pale.

Tulikuwa tunapika uji tunauza, tunatayarisha vitu vingine, sasa ile ilikuwa inasaidia katika kipindi hiki. Sasa na hapa namshauri Mhe. Waziri alichukulie uzito hili aangalie na akiona linafaa na litatusaidia ndani ya nchi yetu basi alichukulie hatua.

Mhe. Spika, nataka nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri katika hili kwa kutuletea mtaalamu Dr. Rajjil, mtaalamu huyu kwa taarifa kafanya kazi nzuri sana katika nchi tafauti kwa kufundisha wajasiri amali. Kafanya kazi hizi Rwanda na wenzetu wa Rwanda sasa hivi wako mbele katika hali hii, katika kujitatulia maisha yao wajasiri amali, kafanya na shughuli nyengine.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri amtumie vizuri sana mtaalamu huyo ili awasaidie wajasiri amali wetu wa hapa Zanzibar na sisi tupate maendeleo watu wetu wasitegemee kila siku kuajiriwa ndani ya Serikali wakati ajira Serikalini ni kidogo.

Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri umtumie mtaalamu huyu na mimi binafsi pia natamani katika ratiba zako pia mtaalamu huyu uniletee katika Wilaya yangu ya Wete katika vituo ambavyo bado hawajapata elimu na wao uwasaidie. Na si hilo tu Mhe. Waziri kutokana na hekima zako ulizonazo nakuomba mtaalamu huyu umtumie pia kwa kuwatoa Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kwenda kusoma ndani ya nchi yake na sisi tutakaporudi kule tutaona jinsi wenzetu wanavyojifunza na sisi tuje kuwasaidia wananchi wetu ndani ya maeneo yetu.

Mhe. Spika, kwa kuendelea nataka nije kwenye kiambatanisho namba moja kwenye ukurasa wa 100 mapato yaliyokusanywa kuanzia Julai 2012 hadi Juni 2013. Hapa kuna kasma kuna na makadirio ya pesa zilizokusanywa na asilimia. Kamisheni ya kazi kutokana na makadirio na pesa zilizokusanywa asilimia 131 wamekwenda vizuri.

Lakini kwenye kasma 142213 Malipo ya ukaguzi sehemu ya kazi na mikataba, makadirio ni 3,000,000 lakini fedha zilizokusanywa ni 22,720000 sawa na asilimia 758. Hapa Mhe. Spika, naomba kidogo Mhe. Waziri anipe ufafanuzi. Kwa sababu katika uelewa wangu mdogo nahisi kwenye mikataba ndio pahali panapokuwa na mapato mengi. Lakini hasa walikadiria shilingi 3,000,000, baadae wakapata shilingi 22,720000.

Sasa naomba sana Mhe. Waziri anipe ufafanuzi je, hapa hii mikataba ilikuwa haipo au mikataba hii ilikuwa hailipiwi au vyengivyo naomba ufafanuzi kidogo.

Mhe. Spika, kwa kuendelea naomba kidogo nigusie kwenye ajira za watoto.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ananambia hamsikii vizuri Mhe. Farida Amour akichangia. Kwa hiyo tuzungumze kwa kunong'ona.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Nikienda kwenye ajira za watoto naomba niipongeze Wizara kwa juhudi kubwa iliyochukua katika kuunda vikundi mbali mbali na *NGO's* za kuzuia ajira mbaya za watoto.

Mhe. Spika, naomba niseme watoto wetu wengi wana ajira mbaya na wametoka katika maskuli na ajira hizi nyingi zinatoka katika maeneo ya baharini. Unapokwenda baharini unawakuta watoto wenye umri mdogo wa kwenda skuli wako kule wanaparishwa samaki, wanabanjishwa kokoto katika maeneo mengine na kupewa vibiashara vidogo vidogo kupita mitaani. Hili kiukweli linasikitisha kwani watoto hawa ndio taifa la kesho.

Sasa Mhe. Spika, mbali na jitihada alizonazo Mhe. Waziri pia naomba wapewe walimu, wazazi, kwa sababu wazazi saa nyengine wale watoto wanatoka kwa sababu ya maisha magumu kwa wazazi wao. Sasa Wizara inajitahidi kuwarudisha watoto wale skuli. Lakini ukitizama mtoto anakwenda skuli akirudi nyumbani kwenye jiko kalala paka hamna kula maneno ya watu wa kwetu huko.

Sasa kwa kweli hii watoto lazima watajiingiza kwenye ajira mbaya. Kwa hiyo, naomba sana mlione hili na wazazi wapewe elimu wafanyiwe utafiti wazazi wale wenye watoto wenye mazingira magumu ili wapewe msaada kwa njia moja au nyengine ili kuondosha tatizo hili.

Mhe. Spika, naomba niingie kwenye sehemu ya wakopaji jinsi ya watu wanavyokopa na ulipaji wao unakuwa unasua sua kiukweli. Katika maeneo mengine unakuta watu wanalipa vizuri lakini maeneo mengine unakuta watu ulipaji wao hauridhishi. Sasa hili linasababisha watu wengine kukosa ule mkopo, kwa sababu watu wanakopa ule mkopo warejeshe ili na wenzao wengine wapate kukopa na namna nyengine.

Lakini sasa watu wakichelewa kulipa au wakisahau kulipa kabisa kabisa inakuwa ni tatizo Mhe. Spika, na pengine wanakosa haki hii ya msingi. Jambo muhimu Mhe. Spika ni ufuatiliaji, na kabla ya kukopa yule anayetaka kukopa afanyiwe utafiti kwanza kwa sababu watu wengine wanakopa hawana kikundi hawana chochote wanakwenda kutumia tu pesa. Sasa inakuwa vigumu kurejesha kule kwa sababu tayari wameshatumia na hawana za kurejesha.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, naomba sana nimpongeze sana Mhe. Waziri lakini pia namuomba sana katika uzungukaji wake aje avitembelee vikundi

vyangu vilivyomo ndani ya Wete Wilaya ya Gando ili aone jinsi anatakavyotusaidia.

Baada ya hayo mimi na wananchi wangu wa Wilaya ya Wete naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi asubuhi hii kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza naomba kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Kwa kweli wizara hii ina majukumu mazito ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, baada ya hayo niende ukurasa namba 4 ambao Mhe. Waziri ameelezea muelekeo wa bajeti kwa mwaka 2013. Wizara yake kwa mwaka huu imeelekea kuchangia katika upitiaji wa malengo ya dira ya maendeleo 2020, mkakati wa kupunguza uchumi na kupunguza umasikini kwa mwaka 2010/2015 na malengo.

Kwa kweli mkatati wa wizara kwenye hili ni kutelekeza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa kweli Mhe. Spika, nimefarijika sana na kazi ambazo zinafanywa na Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Pia ikiwemo kuongeza upatikanaji wa ajira zenye heshima kwa wananchi. Kwani binaadamu bila ya kazi ya heshima basi hakuna maendeleo ya kijamii. Pia Mhe. Waziri nimpongeze kwa kuimarisha uwezo wa watendaji na mazingira ya kazi ili kuwezesha wizara kutekeleza majukumu kwa ufanisi. Nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hilo.

Mhe. Spika, vile vile nikienda kwenye muhtasari wa mapato na matumizi kwa mwaka 2012/2013. Mhe. Waziri ameelezea kwamba kulikuwa na ukusanyaji na makisio yalikuwa na 93,000,000. Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri hapa ni wafanyakazi wangapi wa kigeni ambao walipatiwa vibali hivyo.

Mhe. Spika, nikiendelea na ukurasa wa 68 kwenye Kamisheni ya Kazi. Kamisheni ya Kazi ina majukumu makubwa sana ya kutoa elimu ya sheria na utendaji wa kazi. Mhe. Spika, kwa kweli bila ya elimu na kazi inakuwa ngumu. Kwa hivyo, nimuulize Mhe. Waziri kwa nini elimu juu ya sheria ya kazi imetolewa maeneo ya mjini tu? Kwa mfano SHA Skuli ilioko kwa Mchina mwanzo, *Coconut Beach Hotel* ilioko Chukwani, Skuli ya Al-Hidaya ilioko Chukwani na kadhalika. Na wakati maeneo ya mashamba kuna maeneo

mengi yana migogoro mingi. Kwa hivyo, ni lazima katika suala hili Mhe. Waziri ajitahidi hii elimu kwa maeneo yote.

Vile vile nimwambie Mhe. Waziri kwamba kitengo hichi ni muhimu sana. Tunapozungumza utoaji wa elimu juu ya sheria za kazi kwa waajiri wa wafanyakazi kazi katika sehemu za kazi ni kwa kiasi gani nimuulize Mhe. Waziri kitengo hichi kimewezeshwa kuhakikisha wanafika katika maeneo yote ya kazi kutoa elimu hii na kuepusha Kanisheni ya kazi kupokea migogoro kwa wingi sana. Ili wananchi wafahamu sheria za kazi, ni vizuri kwa wizara ikaendesha vipindi hivi vya redio kwa redio tafauti. Kwa sababu humu inaonesha kwamba Bomba Fm ndio waliotoa elimu hii, lakini kuna redio nyingi mpaka redio binafsi. Kwa hivyo, ni lazima vitolewe kwenye redio tafauti kwa sababu unaweza ukakosa huku lakini ukapata huku. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri kwenye hili ajitahidi ili elimu hii ipatikane kila sehemu.

Pia Mhe. Waziri kwenye kitengo hiki walisema kwamba wamekwenda kwenye maeneo kumi kwenye Sekta binafsi. Kwa nini mwaka mzima elimu hii inatolewa kwenye maeneo kumi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba sana atakapokuja atuelezee ni kwa nini na ingawaje kuna maafisa ukaguzi mbali mbali lakini bado tuna jukumu la kutoa elimu kila maeneo.

Mimi nimshukuru kwenye Idara ya Mikopo ingawa wenzangu wameshazungumza Mhe. Spika, kwamba mikopo ni muhimu na ni lazima inapotolewa mikopo kuwe na ufuatiliaji ili mikopo irejee na wengine wapate kukopa. Vile vile niseme kwamba Idara ya Mikopo ina malengo mengi tu na hasa kwa mwaka 2013/2014 imelenga kutoa mikopo 1000 kwa vikundi vya watu binafsi na kiuchumi, na wajaasiri amali mmoja mmoja yenye thamani ya milioni 300. Lakini kama nilivyokwisha kusema kwamba ni lazima Mhe. Waziri jambo hili liweze kufuatiliwa ili mikopo hii irejeshwe na wengine wapate.

Vile vile niishukuru Idara ya Ushirika kwa kipndi cha mwaka 2012/2013 ilipanga kutekeleza mipango ifuatayo na yote ni mizuri kuanza maandalizi ya kuanzisha Benki ya Ushirika Zanzibar. Hili ni jambo la msingi kabisa ambalo ndio jukumu la Wizara hii, na nitoe pole kwa Idara hii ambayo imebeba Vyama Vya Ushirika kwa kifo cha ndugu yetu, mpenzi wetu ambaye amefariki ghafla tarehe 02/06 Mungu amrehemu ndugu yetu Saada Abdulrahman ambaye kwa upande wangu mimi nasema alitusaidia sana kwenye mfuko ule wa *ZAKKA*, na nimshukuru pia Mhe. Waziri vikundi vyangu viwili vilifanikiwa kupitia kwa msaada mkubwa ambao alitusaidia ndugu yetu Saada Abdulrahman Mungu amlaze pema peponi amin.

Baada ya hayo Mhe. Waziri kwa sababu mengi wameshachangia wenzangu, na kwa vile muda ni mchache naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Amani.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru *Subhana hu Wataalah*, kutujaalia siku ya leo kukutana hapa kujadili hotuba ya Mhe. Waziri Haroun Ali Suleiman.

Mhe. Spika, kwanza mchango wangu nichangie ukurasa wa 14 sehemu ya 18 Programu ya ajira kwa vijana. Mhe. Spika, sina budi kumpa hongera sana Mhe. Waziri kwa kuzihusisha baadhi ya wizara zinazohusiana na maslahi ya vijana kama vile Wizara ya Habari sehemu ya Utalii, Mifugo na Uvuvi pamoja na Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi.

Hili ni jambo jema sana kwani wizara hizi ni miongoni vijana wanamopatikana kwa wingi hata sehemu ya Tawala za Mikoa. Kwa hivyo, kuzihusisha wizara hizi ni jambo la maana sana. Lakini nataka nimuombe sana, wizara hii ya mama Zainab nayo ina umuhimu wake kwa sababu vikundi vingi vya kina mama, vijana, vinapatikana katika wizara ile. Kwa hivyo, ni vyema nayo wizara ikaihusisha ili wizara yake ije kufanya kazi vizuri ikaweza kuwa na eneo zaidi.

Mhe. Spika, kuna idadi Mhe. Waziri aliitaja hapa ya vijana waliopatiwa mafunzo, karibuni 150 wanaojishughulisha na masuala ya utembezaji wa watalii. Kwa kweli kutokana na hali ya Zanzibar tulivyo watu hawa 150 kwa kweli bado vijana kidogo sana, lakini naamini kwamba hii wizara bado ni mpya. Lakini nadhani kwa ninavyomfahamu Mhe. Haroun Ali Suleiman kwa ujasiri wake, hawa vijana atapambana nao kwa nguvu zaidi ili vijana wetu waweze kupata ajira hii na kuwatembeza watalii na kuijua hasa ile historia ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya hawa wanaotembeza hawa watalii historia ya Zanzibar wanaipotosha. Kwa hivyo, kama wizara imeamua kuwapa vijana historia Zanzibar na kuwaelimisha watalii basi Zanzibar itaweza kutambulikana zaidi duniani na kupata heshima na watalii wakaja Zanzibar kwa wingi ili kunyanyua uchumi wa Zanzibar.

Lakini naomba nimwambie Mhe. Waziri kwamba vijana tukiwapa historia ya Zanzibar basi njia moja ya kuinyanyua kiuchumi Zanzibar na kuwafanya wageni wengi wavutike ili waweze kuja Zanzibar na vijana wetu waweze kupa ajira mbali mbali.

Mhe. Spika, katika maelezo yake Mhe. Waziri alisema kwamba kuna gharama za ujenzi wa Masilabi na mwaka uliopita walijenga Masilabi mawili na lengo walikuwa wajenge Masilabi yasiyopungua kumi, ili kuweza kuwaajiri vijana kwa wingi. Lakini suala hilo halikuwezekana katika maeneo mbali mbali. Lakini maelezo yake kajifunga kwamba hakujieleza ni mangapi baada ya hayo kumi anayotarajia kuyajenga, hatukujua kwamba ni matatu au mawili, naomba hapa Mhe. Waziri atupatie jawabu sahihi ni mangapi baada ya kumi aliyoyapata kuyajenga.

Mhe. Spika, kuna mradi huu wa kupambana na ajira za Watoto ibara ya 25 ukurasa wa 28. Kwa kweli Mhe. Spika, tunayo kazi kubwa sana katika ajira hizi za watoto na mimi sisemi kwamba watoto au wazazi wa hawa watoto walikubali kuwatumikisha hawa watoto wadogo kuwafanyia kazi, lakini imani yangu inanipa kwamba ni kutokana na hali ngumu mno ya maisha ya watoto hao.

Kwa hivyo, baadhi ya maeneo yetu tuna hali ngumu ya maisha. Hebu Mhe. Waziri kupitia na kuwashajihisha na kupatiwa sare na mabuku bado havijaondosha tatizo. Kwa sababu Mhe. Spika, tatizo ni maisha, leo na kesho atachukua mabuku watakwenda skuli lakini akirudi tumboni mna njaa, kaenda akirudi tumboni mna njaa kesho atarudi katika diko atakwenda kutafuta maisha.

Kwa hivyo, ili kupunguza maisha haya magumu basi hawa wazee walio na hali hii ya maisha hawa na wengine ndio wanastahiki kupewa huu mfuko wa ZAKKA ili kuwanyanyua kimaisha, ili vijana wetu hawa waweze kupata taaluma, wanapopata taaluma hii baadae watakuwa na uwezo wa kuja kuziendesha familia zao.

Lakini Mhe. Spika, ikiwa mfuko huu wa ZAKKA hauwafikii hawa Waheshimiwa wenye vikundi vyao, lakini wenye hali ngumu ya maisha wanakuwa hawapati chochote itakuwa hapa tunajidanganya, na wala hakuna lolote litakalokuwa, na itakuwa bado tunabeba dhima tunawaacha watu wenye hali ngumu tunawanyanyua watu ambayo tayari wameshanyanyuka kimaisha. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri abadilike au awatafute hawa watu ili waweze kuyamudu maisha.

Mhe. Spika, watu tuliokuwa pembezoni mwa bahari kwenye Madiko hasa Jimbo langu la Tumbe mpango huu wa ajira za vijana kwa kweli umetuathiri sana. Nashukuru kwamba Kamati za Masheha wote wawili pale Mashariki na Magharibi suala hili kwa kushirikiana na viongozi tumelivalia njuga sana ili kupambana nalo. Kwa kweli hata kwenye vyombo vya Bahari suala hili limetoka kwenye Jimbo la Tumbe, lakini Mhe Spika, maisha magumu watu

hawamiliki hata mlo mmoja ni lazima vijana wale watakuja bandarini kwenye madiko wabadilishe biashara yao wapate mambo mengine.

Kwa hivyo, kama hatutawaandalia mazingira mazuri vijana hawa tutakuja hapa tukiimba tu Mhe. Spika, lakini tatizo bado litakuwepo pale pale. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ili tuweze kupambana na ajira hizo za watoto basi ni kuwafikia walengwa katika maeneo yao na kuwasaidia kimawazo, kifikra na kiuchumi, kinyume na hivyo basi tutakuwa hatujawa tayari kupambana na ajira hizi za watoto.

Mhe. Spika, kuna vikundi vya Ushirika ukurasa wa 60. Kwa kweli bado katika Wizara ya Mhe. Waziri kuna ajizi ya kuvipatia usajili vikundi hivi mbali mbali na nashukuru kwamba Serikali imechukua jitihada kubwa ya kuwaelimisha mwananchi wetu wakae pamoja na waunde vikundi vya ushirika wafanye miradi mbali mbali, na wananchi wito wameuitikia na kwa kweli wamefaidika vizuri. Lakini ili utambulike kama wewe ni kikundi cha ushirika uwe na hati sasa wananchi wameshachanga mapesa yao mengi tu wameshafikisha katika taasisi hizi lakini upatikanaji wa hati za usajili umekuwa ni tatizo haupatikani, na tuna kesi mbali mbali Mhe. Waziri tumeshampatia lakini bado hadi leo hazijatatuka.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri punguza msongamano wa vikindi hivi ili wananchi waweze kupata yale ambayo wanayahitaji. Kwa hivyo, kuna haki za wanyonge nyingi kabisa Mhe. Waziri umezizuia pengine vijana wako hujawapitia ukawapa majukumu vizuri.

Kwa hivyo, vijana wanasubiri ni hati zao za usajili. Kwa hivyo, Mhe. Waziri jitahidi na hilo mimi nafikiri kwamba hili kwako ni rahisi mno, siku moja tu ukilishughulikia tatizo hilo basi litatatuka. Mhe. Spika, kuna vijana wanaofanya kazi Ughaibuni nashukuru Mhe. Waziri ametueleza hapa *alhamdulillah* vijana wetu wengi wako nje na wengine wanatarajia kwenda ili kuweza kupata ajira na kuweza kumudu maisha yao, na kuweza kuipatia uchumi nchi yao ya Zanzibar.

Lakini Mhe. Spika, kwa kumalizia juzi nilipa khofu kubwa kwa vijana wetu hawa walioko nje hasa wenzetu hawa wa Kenya ilitangaza kwenye vyombo vya habari kuwataka vijana wao wote walioko nje hasa Qatar warudi nchini kwao kutokana na hali ya mateso, na kutojaliwa utu wao, kuchukuliwa vitambulisho vyao na mambo mengine mbali mbali, wakatangaza rasmi kwamba warudi nchini kwao.

Kwa kweli niliposikia tangazo hili lilinitisha sana nikasema kwamba Kenya ni hivyo, nikasema Zanzibar ni vipi wote wanafanya kazi katika mashirika haya

haya. Kwa hali yoyote itakuwa haki za kibinaadamu hapa inawezekana zinakosekana. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kumuomba Mhe. Waziri hili suala alifuatilie vya kutosha kabisa, itakuwaje Kenya wawaambie wananchi wao warudi Kenya kwa hali yoyote itakuwa na matatizo fulani.

Kwa hivyo, isijekuwa wenzetu wameshapeleka taaarifa kwa nchi yao lakini vijana wetu taarifa wameshaleta ima zimekaliwa au hazikufika ikaja kuwa kuna mateso fulani wanayoyapata vijana wetu. Kwa hivyo, kama kuna matatizo kama hayo basi na sisi si vibaya kuwaambia vijana wetu warudi hapa nyumbani.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Spika,nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na sote ambao tupo hapa katika Baraza lako hili tukufu na kuweza kusimama kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, nianze kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao wameshirikiana katika kuitayarisha hotuba yao hii, na leo hii tunaendelea kuichangia katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Spika, pongezi za pekee zimuendee Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa kitaalamu aliotuwasilishia juzi kwa umahiri kabisa na alichukua muda mfupi kabisa na tulimuelewa na kumfahamu.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi sana, kwa sababu wenzangu wengi mengi wameshachangia, lakini angalau na mimi nizungumze machache katika kuchangia hotuba hii. Mhe. Spika, nianze katika programu hii ya ajira za watoto.

Kwanza napenda kumpongeza sana Waziri kwa juhudi zake za kuanzisha hii programu ya ajira za watoto. Haidhuru ulishaanza mapema katika Wizara ya Wanawake na Watoto kabla haijaletwa huku, lakini nimshukuru.

Mhe. Spika, watoto au vijana ni taifa la kesho, watoto hawa tunatakiwa lazima tuwaendeleze, tuwasaidie, tuwashughulikie ili waweze kuwa watoto wazuri baadae. Watoto hawa ndio ambao tunawategemea wawe Wawakilishi wa baadae, wawe Mawaziri, Maspika na wawe Marais. Kwa hivyo,

nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuandaa hii programu ya kuwasaidia watoto hawa.

Lakini Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri kwamba wizara yake imejipanga vipi ili kuona kwamba hawa vijana ambao wanawatoa kwenye janga hili la ajira mbaya za watoto na kuwarejesha maskulini. Je, wamejipanga vipi ili kuona kwamba vijana hawa hawarejei tena katika janga hili la ajira za watoto. Kwa sababu Mhe. Spika, kama walivyosema wenzangu ni kwamba kuwatoa tu katika ajira za watoto na kuwapa sare na mabuku kurudi maskulini bado hatujawasaidia. Kuwasaidia watoto hawa ni lazima kuwe na mikakati madhubuti iliyopangwa na wizara, badala ya kuwarejesha maskulini na kuwapa *uniform* na mabuku, lakini kuwe na mpango mbadala wa kuwawezesha na kuwasaidia ili wasiweze tena kurudi katika ajira hizi za watoto.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwamba amejipanga vipi au ana mikakati gani ya kuwasaidia watoto hawa ili wasiweze kurejea tena katika ajira hizi za watoto na waendelee na masomo, ili waje kuwa watoto bora na watusaidie wazee wao baadae.

Mhe. Spika, nikitoka hapa nije kwenye Idara ya Ushirika. Hapa naomba nimpongeze sana Mkurugenzi wa Idara ya Vyama vya Ushirika, pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi zao kubwa ambazo wanazozifanya, kupita kushajihisha usajili na kuviwezesha vyama vya ushirika.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwamba Idara ya Ushirika ni idara mbayo tunaitegemea sana hasa sisi wanasiasa katika kusajili vikundi vyetu na umaarufu wetu wengi tunaoupata kutokana na idara hii. Lakini Mhe. Spika, idara hii imekuwa kama ni mtoto yatima ambaye amekosa msaada, kwa sababu kuna mayatima ambao wanapata, lakini mayatima wa bahati mbaya ambao hawana misaada. Idara ya Vyama vya Ushirika ilikuwa katika jengo la Wizara ya Kilimo kule, wakati nilipokuwa kwenye wizara ya kilimo. Idara kule ilihama baada ya jengo lile kudata likahamia viwanda vidogo vidogo na sasa hivi idara hii iko katika wizara yako Mhe. Spika. Lakini idara hii imetoka kwenye jengo bovu na imeingizwa kwenye jengo bovu vile vile, jengo ambalo ikinyesha mvua linavuja halina nafasi, hawana vitendea kazi vya kutosha.

Mhe. Spika, si hapo tu, hata wilayani katika Ofisi za Ushirika za Wilaya wanakaa katika majengo mabovu, majengo yasiyostahiki, hamna vitendea kazi, hawana kompyuta, hawana meza. Meza moja anakaa Afisa Ushirika, anawekwa na Afisa Ustawi na mwengine, hawana mpangilio mzuri katika ofisi zao.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tutakuwa kila siku tunawalaumu maafisa ushirika kwamba zile hati hazipatikani, tunawalaumu maafisa ushirika hawasajili vikundi. Lakini maafisa ushirika wana kazi ngumu na kubwa sana, lakini leo afisa ushirika katika wilaya yake ana vikundi zaidi ya 500, amepewa pikipiki, lakini pikipiki hiyo inatiwa mafuta kwa awamu, na afisa huyo anatakiwa afuatilie pengine labda vyama vya ushirika vya Ukongoroni, afuatilie vya Uzi, afuatilie vya Matemwe na afuatilie vya kila pahali. Lakini bila ya nyenzo hatoweza kufika kule.

Mhe. Spika, kila wilaya ina afisa mmoja tu wa ushirika, afisa ambaye anatakiwa kushughulikia vyama vinafika zaidi ya 500 tuseme, sasa tutakuwa tunawalaumu maafisa ushirika, lakini hawana makosa kwa sababu vitendea kazi vya kufikia kule kwenye vikundi hawana, mafuta ya kutosha hawana, hawana kompyuta. Kazi za Afisa Ushirika sio mezani, kazi ya ushirika ni *field*, lakini atakaporudi *field* anatakiwa akae mezani, awe na kompyuta yake na afanye kazi zake alizokwenda kuzipata huko *field*, lakini vitendea kazi hana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba lile jengo la ushirika angalau kwa hatua za mwanzo lifanyiwe ukarabati ili inaponyesha mvua wasivujiwe, kwa sababu Mhe. Spika, tunaambiwa kwamba *'mali bila daftari hupotea bila habari'*. Lakini watakuwa wanaweka kumbukumbu, kumbukumbu ikinyesha mvua zinavujiwa, zinaroa hazifai. Unakwenda kutafuta kumbukumbu zako pale idarani hazipatikani zimeharibika kwa mvua, basi angalau ifanywe juhudi ya makusudi ili kukarabatiwa tu lile jengo ili wawe katika hali nzuri.

Pia Mhe. Spika, kuwe na utaratibu maalum kwa maafisa wa ushirika wa wilaya kupatiwa mafuta kwa kila wiki ya kutosha ili kuweza kufuatilia vikundi mbali mbali ambavyo vinakuwa mbali na maeneo yao, Jiografia za wilaya zetu tunazijua, kuna sehemu huwezi kufika kirahisi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika tunaomba Mhe. Waziri uione sana hii idara, hii ni idara muhimu na ni nyeti sana. Idara hii ndio inayotupa sifa sisi huko majimboni kwetu, idara hii ndio inayotupa sifa sisi kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika naomba hii idara uione kwa jicho la huruma.

Mhe. Spika, hapo hapo kwanza Mhe. Waziri katika uwasilishaji wake alisema hapa kwamba makisio ya mapato ya idara ya ushirika ni milioni 6, lakini kwa juhudi zao pamoja na hali zao ngumu wamepindukia makisio, wamekusanya mapato ya asilimia 122. Sasa suala hili Mhe. Waziri idara hii aipe kipaumbele ili waweze kufanikisha zaidi.

Mhe. Spika, nije katika mfuko wa Zakka. Nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuzindua huu mfuko na kuwapatia misaada hawa wananchi katika shehia mbali mbali kutokana na huu mfuko wa Zakka. Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kutaka kuhakikisha kwamba anawawezesha wananchi kiuchumi na anataka hasa kuwaondolea umaskini.

Lakini Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwamba awe na mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba hizi fedha ambazo zinatolewa zinatumika vizuri, zifuatiliwe ili ziweze kutumika vile ambavyo inavyopaswa. Mimi sikatai kuwa wasipewe labda watu wenye mazingira magumu au wapewe vikundi vya ushirika na kadhalika. Kwa sababu najua kila jambo lina mpangilio wake. Mhe. Waziri yeye anajua pesa hizi kapewa vipi na katakiwa azifanyie nini, tunajua kwamba yeye hakukurupuka tu kuzitoa hizi pesa akazipeleka kwenye vikundi, najua lazima hizi pesa alipewa kwa masharti maalum na mpangiliao maalum. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninachomuomba Mhe. Waziri ni kwamba ahakikishe kuwa kwa kupitia watendaji wake kwamba hizi fedha zinatumika vile ambavyo inapaswa na ule urejeshaji wake ambao umepangwa zinarejeshwa kwa mpangilio ili waweze kupatiwa watu wengine fedha hizi. Mhe. Waziri nampongeza kwa hili.

Mhe. Spika, jengine niende katika hii programu ya uwezeshaji wananchi kiushirika. Mhe. Spika, tumekuwa tukiunda vikundi vya uzalishaji vingi, lakini vikundi hivyo vinakuwa haviko endelevu, kwa sababu vikundi vinapoundwa vinatakiwa vifuatiliwe au bidhaa zinatakiwa pia zifuatiliwe, lakini hatuwezi kuwa na vikundi bora kama hatukuwa na ufuatiliaji wa kutosha katika vikundi hivyo. Vikundi vyetu vimekuwa na changamoto kubwa ya ubora wa bidhaa zetu, bado katika vikundi vyetu ubora wa bidhaa hautoshi. Tunapokwenda kwenye maonesho ya wenzetu tunaona hasa kwamba bidhaa zetu hazina ubora, *finishing* zetu sio nzuri. Utawakuta wanaushirika wetu pengine wanasuka mikoba mizuri au vitu vingine vizuri, lakini *finishing* haitoshi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri achukue juhudi ya makusudi ili kutoa mafunzo na kusaidia vikundi hivi katika mafunzo ya uboreshaji wa bidhaa, ili na sisi tuweze kuingia katika masoko ya kimataifa. Mhe. Spika, tunapokwenda katika maonesho tunaona, tunaangalia bidhaa za wenzetu, bidhaa za vikundi vyetu zinakuwa hazina ubora kusema kweli. Kwa hivyo, Mhe. Spika, Mhe. Waziri afanye juhudi za makusudi ili kufanya mafunzo ya vikundi vyetu katika uboreshaji wa bidhaa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama kawaida yetu na leo tumetembelewa na wageni mbali mbali ambao wapo kuona tunavyoendelea na shughuli zetu za bajeti. Wageni wetu wa leo ni Mhe. Balozi Ronald Jueman, ambaye ni Balozi wa Seychelles nchini Marekani, lakini pia ni Balozi wa Kudumu wa Seychelles kwenye Umoja wa Mataifa.

Could Your excellency rise and salute the Members, yes! Thank you.

Shughuli zake ni kushughulika katika mambo ya nchi za visiwa vidogo vidogo duniani, katika maendeleo endelevu ya mabadiliko ya tabia nchi.

Mgeni mwengine ambaye amefuatana naye ni Bwana Wills Angricole ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mazingira na Nishati wa Seychelles. Pia ni Rais wa *Western Indian Ocean Coastal Challenge and Climate Change (WIOCC). Yes. You are most welcome*!

Ndugu zetu wageni hawa wamefuatana na wenyeji wao wa hapa Zanzibar kwa shughuli za utekelezaji wa miradi ya maendeleo endelevu ya mazingira wa nchi za visiwa vidogo vidogo vya Bahari ya Hindi, na waliofuatana nao ni Mkurugenzi wa Mazingira bwana Sheha Mjaja Juma pamoja na afisa kutoka Mazingira Dk. Aboud Suleiman Jumbe.

You are most welcome to see how we are doing our budget session this time, thank you!

Wageni wengine ni wanafunzi kutoka Chuo cha Ufundi wa Magari hapa Mbweni, jumla yao ni wanafunzi 40 wamefuatana na walimu wao wanne. Wote kwa pamoja nawaomba wasimame ili kuwatambua. Karibuni sana muone shughuli za bajeti zinaendelea kwa kiasi gani. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana.

Waheshimiwa Wajumbe muda wetu unakaribia saa 5:00 ambazo nimemuomba tayari Mhe. Waziri aje kufanya majumuisho ya hotuba yake hii ya makadirio ya bajeti. Tunao wachangiaji wengine wanne, kwa hivyo niwaombe wafupishe muda katika kuchangia ili wachangiaji hao wanne tupate tuwamalize. Basi baada ya hapo nimkaribishe Mhe. Ashura Sharif Ali na baadae Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu aliyetujaalia uhai na akatupa uzima, tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika wizara hii ambayo iko mezani kuchangiwa wakati huu. Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake, alikuwa makini sana katika kuwasilisha. Vile vile niwapongeze na watendaji wake.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 19 kwenye kifungu cha 20 cha kitabu hiki cha hotuba ya Waziri katika programu ya kazi nje nje. Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri nataka anifanyie ufafanuzi kidogo, hapa nampongeza kwanza kwa kuweza kutoa mafunzo kwa wajasiri amali 901 wanawake wakiwemo 549 na wanaume 352.

Mhe. Spika, baada ya mafunzo ningependa nimuombe Mhe. Waziri anipatie ufafanuzi, je mmefanya ufuatiliaji, mmeona wamenufaika na manufaa yao ni ya aina gani na biashara labda wanazozifanya ni zipi, ningependa kuzielewa, maana isiwe biashara ikawa ni ile ile tu ya chapati na maandazi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu huu sasa nakwenda katika ukurasa wa 20 kwenye kifungu cha 22 kuhusu programu ya UNDA. Hapa nampongeza Mhe. Waziri kwa utekelezaji wa programu hii vizuri kabisa. Amesema pia ametoa mafunzo kwa wajumbe 150, katika hao wajumbe 150 wanawake walikuwa ni 38 na wanaume ni 112. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho uniambie ulitumia vigezo gani mpaka wanawake wakawa ni 38 tu kati ya hawa 112, kwani naona idadi kubwa ni ya wanaume na wanawake wamekuwa ni wachache, wakati naona idadi yetu sisi wanawake ni wengi zaidi na wajasiri amali wanawake ndio wengi zaidi.

Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi chango wangu sio mkubwa sana nikiendelea katika ukurasa wa 28 kwenye kifungu nambari 25 kuhusu kupambana na ajira za watoto. Mhe. Spika, hii sio siri kwamba kiutamaduni wetu sio vizuri watoto wetu kuweza kuingia katika ajira kabla ya muda wao. Ajira za watoto sio kitu kizuri sote tunajua kwamba miili yao haihimili; kwani hutumwa kazi ambazo nyengine zinakuwa ni ngumu, wakati mwengine hata mtu mzima akipewa anakuwa hawezi, lakini maskini wao watoto wanatumiwa hivyo.

Nikupongeze Mhe. Waziri kwa kuona kuwa na wewe unamsaidia sasa Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kuona kwamba sasa tunataka tupunguze au tuondoe kabisa watoto wetu kuajiriwa wakiwa wadogo. Lakini hili la kupambana na hii ajira ya watoto, basi Mhe. Waziri utakapokuja hapa kufanya majumuisho, umesema humu katika kitabu chako kwamba mbali na kuwapa sare za skuli watoto na vitabu lakini umesema kwamba umeziwezesha familia zao yaani umewafanyisha waweze

kufanya shughuli za kupata uchumi. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa unieleweshe kidogo kuwa biashara hizo ni za kiasi gani, kama ni fedha ulizozipatia hizo familia. Lakini ikiwa kama ni shughuli za ufugaji, basi tueleweshwe kuwa labda walipatiwa ng'ombe au mbuzi na idadi yenyewe halisi.

Baada ya kusema hayo niendelee katika ukurasa wa 77 katika kifungu cha 56 Idara ya Ajira. Mhe. Spika, tatizo la ajira ni tatizo ambalo linaikwaza sana serikali yetu au nchi yetu kwa jumla, ni ukweli usiofichika kwamba vijana wetu wengi hawana ajira. Mhe. Rais amelipanga hili ili kuona sasa ameliwekea wizara maalum ili tuweze kukwamuka.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika kitabu chake humu ameeleza mambo mengi na utaratibu mbali mbali wa kuonesha kwamba vijana wetu waweze kupata ajira. Lakini mimi nikiangalia labda Mhe. Waziri ningependa kuelewa tu, labda umeshirikiana nayo vipi sekta ya uwekezaji, ili kuona kwamba vijana wetu ambao wana uwezo wa kufanya kazi katika mahoteli, ukaweza kuzisimamia na ukahakikisha kwamba vijana wale katika sekta hizo wanafanya kazi zile ambazo wanaziweza na kuzimudu kielimu na kitaaluma, sijui hili umelifuatilia vipi.

Kwa hivyo, tungependa Mhe. Waziri suala hili utueleze hasa, hivi haya mahoteli yaliopo mengi yao tunaona kwamba wanaofanya kazi ni wageni zaidi kuliko vijana wetu ambao hawana kazi. Hivyo basi, ningeomba Mhe. Waziri suala hili unieleze hasa wewe unashirikiana vipi kuona kwamba sehemu za uwekezaji, vijana wa Kizanzibari wanapewa nafasi ya kwanza kuweza kupata ajira ikiwa ndio tatizo kuu la taifa na serikali. Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein ameiundia wizara maalum ili hili liweze kutatuka, kwa upande wako naomba Mhe. Waziri nilipate hili.

Vile vile Mhe. Waziri utuambie katika hizo ajira je, wamo ambao mikataba yao na utaratibu wao wa kazi unaufuatilia vipi ili kuona kwamba katika hizi ajira basi hawapati matatizo katika ajira hizo, kwani tumeona kwamba mahoteli mengi ambayo yanafanya kazi ambapo mengine tumeyafanyia uchunguzi tunazo kuwa wale ambao wapo na ni Wazanzibari wazawa, basi mara nyingi wanapata zile nafasi duni hata kama taaluma zao zinaruhusu kufanya kazi nyengine. Tumeona kuna watu wengi wao wametoka nje ya nchi yetu na wanafanya kazi.

Mhe. Spika, kwa ufahamu wangu katika sekta hii ya uwekezaji, mara nyingi anapokuja kuwekeza kama mtaalamu hapa hayupo, anapaswa basi apangiwe kuwa na mwenyeji miaka miwili anakaa naye. Naamini kwamba kwa miaka miwili kukaa na mwenyeji wake kufanya kazi, ikimalizika kwa vyovyote vile

tayari ameshapata huduma ile na mzawa anaendelea kuchukua nafasi ile na mgeni kuweza kuondoka. Je, wewe kwa upande wako Mhe. Waziri utatueleza suala hili umelifanya kwa utaratibu gani.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 60 Idara ya Ushirika. Kwa hapa Mhe Spika, niseme kwamba nampongeza Mhe. Waziri kwa kusema kwamba ana nia ya kuanzisha hii benki ya vyama vya ushirika, niseme kuwa napongeza sana, nadhani huduma zao sasa zitakuwa ziko karibu na ziko katika sekta ambayo imekuwa peke yake, itakuwa ni rahisi kupata utaratibu wao.

Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Waziri kwamba katika sekta hii ya ushirika kwenye Wilaya yangu ya Kaskazini B Unguja imekuwa na urasimu wa kutosha. Kwa kweli wananchi wamehamasika, wamejikusanya, wametimiza masharti na wameomba kwa muda mrefu hadi leo wengine wanafikia mwaka mmoja lakini hawajaweza kupata usajili, hili ni tatizo. Suala hili Mhe. Waziri ndilo ambalo nitazuia fungu lako, kwa sababu ya kwamba watu wangu wa Kaskazini B kwenye vikundi mbali mbali hawa wamefika mwaka mmoja na hawajapata usajili wa vikundi vya ushirika. Ikiwa ni azma ya serikali kwamba wajikusanye pamoja ili waweze kuwa rahisi kuwakwamua kiuchumi, lakini hujawafanyia usajili na hawawezi kupata haki zao za msingi. Mhe. Waziri maelezo ya bajeti yako ni mazuri, lakini kwa suala hili mimi naondoa shilingi.

Mhe. Spika, katika huo huo ushirika kuna vikundi mbali mbali ambavyo vimeanzishwa kwa msingi mzuri, lakini wana taaluma ndogo mbayo hawawezi kabisa kujiendeleza na kufikia malengo. Ningekuomba Mhe. Waziri vikundi vinaanzishwa kwa kasi kubwa na wengine wakasajiliwa kwa haraka, lakini matokeo yake baada ya muda mfupi shughuli hizo za kiushirika huwa haziendelei. Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri ulifanyie juhudi za makusudi kuona kwamba vikundi hivyo vinapewa taaluma na vinaweza kujiendesha wenyewe, nadhani lile lengo la kuanzisha vikundi hivi au ushirika huu ndivyo vitakavyoweza kufikia mahala.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 53 kuhusu Idara ya Mikopo. Hapa kwenye idara hii ya mikopo Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Waziri katika kiambatanisho nambari 4 nimeona kwamba kuna wilaya mbali mbali ambazo Mhe. Waziri amezipatia mikopo, lakini katika idadi ambayo kaifanya ya kutoa hizo fedha za mikopo, nimeona kuwa Wilaya ya Micheweni imepewa fedha finyu sana, kwa sababu tafiti nyingi zilizofanyika zinaonesha kwamba Wilaya ya Micheweni ndio wilaya maskini sana. Mimi nilidhani kwa kuwa wewe ni Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, basi nilijua hawa ndio utawapa kipaumbele ili kuona kwamba wamepata fedha nyingi zaidi kwa ajili ya kujikwamua na kujiongezea kipato ili kupunguza

umaskini. Lakini nimeona takwimu uliowapatia imekuwa ndogo mno kuliko wilaya zote. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba utakapokuja kufanya majumuisho yako basi unifahamishe labda umetumia vigezo gani ili hata Wilaya ya Micheweni ikapata fedha ndogo zaidi.

Mhe. Spika: Umalizie kwa dakika tatu

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante Mhe. Spika. Kwa kuwa Mhe. Spika, yale yote ambayo niliyakusudia kuyasema yamefika mwisho, basi niseme kwamba kwa hapa nilipofikia siwezi kuunga mkono hoja napunguza fungu langu mpaka pale Mhe. Waziri atakaponipa ufafanuzi wa kina juu ya kuwafanyia usajili vyama au vikundi vya ushirika, ambavyo vinakaribia mwaka mmoja sasa bado havijapata *registration*.

Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Panya Ali Abdalla naye atatumia muda mfupi kama waliotangulia na baadaye Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia tukaweza kukutana hapa asubuhi hii tukiwa katika hali ya uzima.

Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe ambaye umenipatia nafasi hii, ili niweze kutoa mchango wangu mdogo katika wizara hii.

Tatu namshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa hotuba yake nzuri na alivyoisoma kwa ufasaha mzuri kabisa yeye pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika Idara hii ya Mikopo ukurasa wa 53. Kwa kweli malengo yaliyowekwa ya mikopo inaonekana mikopo 1,000 ipatikane. Lakini kwenye utekelezaji tunaona kuna 193, ambapo Unguja ni 142 na Pemba ni 50 yenye thamani ya milioni 156,000,000/=. Mhe. Spika, hapa ninaona hata ile robo haikufikiwa ya yale malengo. Kwa hivyo, nataka nimuulize Mhe. Waziri kwa nini walikosa kufikia malengo na walikusudia watoe mikopo 1,000, lakini imetoka 193.

Vile vile nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba angalie katika huu utoaji wa mikopo pamoja na kuwa tunasema vikundi vinapata elimu ndogo, basi aangalie kwa sababu si watu wote ambao wanaoweza kufanya biashara.

Kwa hiyo, aangalie na afanye utafiti wa kina, ili zile fedha zikitolewa basi ziweze kutumika katika hali ambayo imekusudiwa. Kwa mfano, wako wengine wanakuwa hawajajipanga na ukiwapa fedha wanaweza kuharibu, lakini ni vyema afanye utafiti mwanzo na halafu akizitoa fedha, basi ajue anazipeleka kwa walengwa.

Mhe. Spika, nasema hayo kwa sababu wapo akinamama ambao ni wajasiri amali, ambapo kwa kweli ukiangalia wanajituma vya kutosha. Kwa mfano, ukipita katika mji au mashamba vijijini basi utawakuta akinamama wanajituma sana, na hivi sasa akinamama wengi utakuta wengi ni wauzaji wa samaki, ambao wanajitolea kufanya biashara hiyo.

Lakini bado serikali haijaangalia mazingira mazuri labda ya kuweza kuwaweka wafanyabiashara wale wakaweza kuwa na mahala pazuri pa kuweza kufanyia biashara, kila upande utakaopita utawakuta akinamama wanauza samaki na bado hawana mazingira mazuri ya kuweza kufanyia zile biashara zao.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aangalie kuwapatia mazingira ambapo wataweza akinamama wale kufanya biashara zao vizuri.

Nikiendelea na mchango wangu naomba nizungumzie kuhusu Mkoa wangu wa Kaskazini kuna akinamama ambao wanajishughulisha sana na biashara ya dagaa. Pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwapatia mikopo akinamama hawa na wanaonekana wanaendelea vizuri na biashara zao.

Hata hivyo, Mhe. Spika nimuombe Mhe. Waziri kwamba akinamama hawa bado wanahitaji elimu ya kutosha kuhusu hii biashara yao ya dagaa. Kwa kweli biashara ya dagaa inaonekana ni biashara yenye fedha nyingi, lakini bado wanakosa utaalamu wa kuweza kulihifadhi vizuri dagaa lile na likaweza kuuzwa hapa na nje ya nchi, kwa ajili ya kuweza kujipatia fedha nyingi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia akinamama hawa wanasumbuka na wanakuwa na changamoto kubwa wakati wa mvua kwa biashara ile ya dagaa. Kwa hivyo, serikali iangalie uwezekano wa kuweza kuwapatia chombo chochote ambacho kitaweza kuhifadhi dagaa lile wakati wa mvua, kwa sababu wanakuwa wanakula hasara kubwa sana.

Kwa maana hiyo, mimi naona tuwape moyo wale ambao tayari wamejitolea kutaka kujituma, basi tuweze kuwawezesha vizuri zaidi, ili waweze kuzalisha zaidi.

Sasa naomba niende katika Ajira ya Watoto ambapo wenzangu wameizungumza sana na mimi naomba niitilie mkazo. Mhe. Spika, niiombe wizara kwani ajira hii inaonekana sana katika ukanda wa pwani na masoko, yaani vijana hapo ndipo wanapoonekana kujishughulisha sana.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wizara iweze kuweka mikakati madhubuti, kwa ajili ya kufuatilia katika sehemu hizo na iwekwe marufuku kuonekana watoto wakati wa masomo ya skuli au chuoni.

Mhe. Spika, niende kwenye Kamisheni ya Kazi. Kwa kweli hapa niiombe sana serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba iweze kuziangalia vizuri sheria za kazi pamoja na mikataba ya kazi hasa kwenye sekta binafsi. Waajiri wa sekta binafsi wanawatumia vibaya sana wafanyakazi, hawajali muda wala afya pamoja na kazi kubwa maslahi madogo. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia kwako, kwani waajiri hawa huwa wanawaajiri wafanyakazi, lakini katikati ya mkataba basi mfanyakazi yule anaweza akasimamishwa kazi wakati tayari muajiri yule anakuwa ameshampeleka kwenye Mfuko wa *ZSSF*, sasa anapomkatisha kazi ina maana tayari ameshamkatisha yale mafao yake. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika nimuombe sana Mhe. Waziri kuliangalia sana hili; kwa kweli vijana wetu wanateseka sana hasa kwenye mahoteli ya watalii, kwa sababu wanawaamulia wanavyotaka wao, kwa kuwa wameshawaona ni wanyonge na hawa pa kupata kazi, basi na wao wanawafanyia hivyo. Kwa maana hiyo, serikali iendelee kuwalinda wafanyakazi hawa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nitoe mfano kwa Kiwanda cha Sukari, hivi sasa kinajishughulisha na shughuli ndogo ndogo na labda tunategemea mwezi wa Novemba wakaanza uzalishaji. Lakini utakuta mshahara wa watu wote uko sawa sawa, na pale hujui mtaalamu au mtu wa shambani analipwa kiasi gani? Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, alizingatie kwa sababu pale lazima waangalie watu wenye uzoefu, wataalamu, ili mishahara ile isiwe inakwenda sambamba kwa watu wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mchango wangu sio mkubwa na nilitaka niyaseme hayo na ninamuomba sana Mhe. Waziri, ili vijana wake waendelee kufanya kazi basi ni lazima awazungukie mara kwa mara, kwa ajili ya kuona mikataba inaendelezwa vizuri.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunakushukuru. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Salma Mohammed Ali, wakati Mhe. Amina Iddi Mabrouk anajitayarisha ambaye atakuwa ni mchangiaji wa mwisho.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pia nampongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba. Vile vile Mhe. Spika, nadhani Mhe. Rais aliuona umakini wa Mhe. Waziri, kwa sababu anao uwezo, tena anayo imani kubwa ndio maana akampa kuiongoza Wizara hii. Mhe. Spika, nayasema haya kwa sababu wizara hii ni muhimu na imebeba mambo mengi ambayo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kuzungumzia shughuli za kazi na ajira. Katika nchi hii kuna watu wengi, vijana na wanawake ambao hawana kazi na matokeo yake imepelekea vijana wengi kuzurura na kuingia kwenye vikundi viovu.

Vile vile kuna wanawake ambao hawana kazi na matokeo ya hali hiyo imepelekea wanawake hao kufanya kazi nzito kama vile za kubeba zege kwenye shughuli za ujenzi; na Mhe. Spika kubeba zege si kazi za wanawake. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie hili na aone uchungu kuona wanawake wa Zanzibar wanafanya kazi hizi na pia abuni kazi za heshima kwa wanawake wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kutokana na imani ya Mhe. Waziri nadhani ataliangalia sana hili, kwamba mwanamke kujitwika zege ni kazi ngumu na hasa ukizingatia wanawake tuna kazi kubwa majumbani. *(Makofi)*

Suala jengine ambalo nataka nilizungumze kwa ufupi kwa sababu wengi wamelizungumza ni kuhusu kazi kwenye mahoteli ya kitalii. Mhe. Spika, inasikitisha sana kwani kwenye mahoteli ya kitalii wanaofanya kazi ni watu kutoka nje, na hapa kwetu tuna vijana wa kike na wa kiume, ambao tayari wameshasoma kwenye Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar, lakini hawaajiriwi. Jambo hili linasikitisha sana Mhe. Spika, kwa sababu kijana ameshajitolea kusoma lakini ajira wanapewa watu wa nje na hii inaumiza sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze kwamba atawasaidia vipi vijana hawa kupata ajira sehemu zile.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka nilizungumzie ambalo limezungumza sana na nitalizungumzia kidogo tu ni kuhusu utaratibu mbovu wa upatikanaji wa mikopo. Kwa kweli upatikanaji wa mikopo hauko wazi na

unakwenda kwa kujuana, na hali hii pia inachangia hata kurejesha mikopo ikawa pia ni kujuana. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze kwamba ni vigezo gani wanavyotumia hata wengine wakapata mikopo na wengine wakakosa?

Sasa naomba niangalie kiambatanisho Nam. 1 kwenye ukurasa wa 100. Mhe. Spika, hapa ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa sababu katika ukusanyaji inaonesha Kamisheni ya Kazi wamevuka malengo, kwa hiyo nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na hii Kamisheni ya Kazi, kwa sababu wamefikia asilimia 758. *(Makofi)*

Kwa kweli Mhe. Spika, hapa wamejitahidi sana kwa sababu hata mara nyingi tukivuka malengo huwa pengine kwenye 110 au 120, lakini wao wamefikia 758. Mhe. Spika, hapa nawaomba wasijekuwa wagema kwamba tukawasifu na mwakani tukaja tukapokea taarifa kwamba hawakufikia asilimia 100. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri apokee pongezi na ajipange mwakani mwakani kupokea tena pongezi. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye kiambatanisho Nam. 4 kwenye ukurasa wa 107. Mhe. Spika, kiambatanisho hichi kinazungumzia kuhusu utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Kujitegemea kwa kipindi cha mwaka 2012/2013. Mhe. Spika, hapa inaonesha kwa upande wa Unguja wamepata mkopo wa shilingi milioni 112,000,000/=, lakini kwa upande wa Pemba wamepata milioni 44,000,000/=. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze je, ni sababu gani iliyosababisha hali hii au kule Pemba hakuna vikundi vinavyotaka mikopo?

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze kidogo ni kiambatanisho Nam. 8(b) ambacho kiko kwenye ukurasa wa 115. Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri ametuambia kwamba waliopata ajira za nje wanaume ni 55 na wanawake ni 160. Sasa hapa Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anifahamishe ni kazi za aina gani hizo wanazofanya wanawake huko nje, kwa sababu isijekuwa kazi ni ile ya kubeba zege ambayo tunayoikataa hapa. Vile vile anieleze je wizara yake ina uhakika gani kama wanawake hawa hawanyanyaswi, na ikiwa wananyanyaswa wizara yake wanawasiliana vipi na watu hawa? *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimalizie ukurasa wa 51 *paragraph* ya 41. Kwa kweli hapa nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa kuviwezesha vikundi vya ushirika kwa lengo lile walilomalizia la kusema kama hatima yake na wao waweze kutoa Zakka.

Mhe. Spika, unapomuwezesha mtu kwa ajili ya kutaka afanye ibada ni jambo kubwa, kwa hiyo hapa nampongeza sana Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Spika, hivi vikundi vilivyokuwa vinahitaji huu msaada ni vingi na vilivyopata ni kidogo. Kwa hivyo, Mhe. Spika namuomba Mhe. Waziri atueleze kwamba hivi vikundi vyengine ameviandalia vipi au amevifikiria vipi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa sababu hapa kuna na wenzetu wa *Sober House* ambao tayari wameshajikusanya na wamekusudia kutoka katika mazingira mabaya kusema kweli. Sasa hapa tayari wameshajikusanya na mara nyingi wanapotoka kule huwa wanarudia ile hali kwa sababu hawana uwezo.

Kwa hivyo, hapa ninamshauri Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ashirikiane na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuviangalia hivi vikundi aviwezeshe navyo, ili wawe na muelekeo watakapotoka wasirudie kule walikotokea mwanzo. *(Makofi)*

Baada ya mchango wangu huo mfupi Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunakushukuru. Sasa tumkaribishe Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia kuweza kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kutimiza kumi la pili.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa Zanzibar wanaondokana na umasikini.

Mchango wangu hautokuwa mkubwa sana, kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wengi wameshazungumza sana na wameshajikita kwenye maeneo mbali mbali, kwa hiyo niseme kwamba wengi wao wamenifilisi. Lakini kwa vile tupo hapa kwa ajili ya kuwakilisha wananchi basi naomba yale maeneo nitakayochangia mimi ni kwa kutilia msisitizo.

Mhe. Spika, katika kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 29. Kwa kweli hapa naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi zake ambazo anachukua katika kuhakikisha kwamba watoto wanaondokana na ajira mbali mbali, na hapa ametuelezea kwenye ukurasa wa 29 kwamba maeneo mbali

mbali kama vile Chumbuni, Mwanakwerekwe, Shaurimoyo wamehakikisha kwamba watoto wanawachukua na kuwapeleka skuli.

Hata hivyo, pamoja na jitihada hizi za Mhe. Waziri labda mimi niseme kwamba bado sijajua hasa tafsiri hii ya wanavyoshughulikia watoto inakuwa vipi, kwa sababu tatizo bado linaonekana lipo na linaendela siku hadi.

Lakini si hilo tu Mhe. Spika, pia yapo maeneo ambayo ya wazi pengine sisi sote tuliomo humu tunayaona yamejitokeza katika ajira za watoto mbali mbali. Kwa mfano, eneo la Marikiti sijaona humu Mhe. Waziri kulitaja moja kwa moja. Mhe. Spika, Marikiti kuna watoto wengi zaidi ambao wanatumiwa katika ajira za kupara samaki.

Mhe. Spika, pia maeneo ya wachunga punda katika suala la kuchimba mchanga. Tatizo hili ni kubwa mno na *impact* yake ni kubwa, kwa sababu ndani yake kuna uchafuzi wa mazingira. Kwa mfano, Mhe. Spika kama tutakwenda kwenye eneo la Mwanakwerekwe, ile ardhi ambayo tunaitegemea kwa kuzikia watu kama utapita Mhe. Spika imemong'onyoka yote, yaani hivi sasa ukienda pale utawakuta watoto wana gari za punda wanachimba mchanga tena kwa kasi mno.

Kwa hivyo, mimi naona bado serikali haijatilia maanani katika kuhakikisha kwamba watoto wetu wanaondokana na ajira hizi. Mhe. Spika, mimi kila ninaposimama huwa ninazungumzia suala zima la ajira za watoto. Sisi tuliopo hapa ni wazazi, ambapo tuko akinamama na akinababa, sasa unapopita majiani ukawaona watoto wetu jinsi wanavyotembea au wanavyozurura ovyo katika kufanya kazi, basi machozi yanaweza kukutoka.

Kwa mfano, ukienda Marikiti ya Mwanakwerekwe Mhe. Spika, unawakuta watoto wanatembeza maji ya kunywa, yaani wanauza, kwa kweli Mhe. Spika inasikitisha. Sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, pamoja na wenzangu wamesema kwamba Mhe. Waziri wizara yake itilie mkazo mno, na ikae ijipange kuona kwamba watoto wanaondokana na ajira hizi mbali mbali za watoto. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu na kama nilivyosema kwamba mchango wangu hautokuwa mkubwa. Sasa naomba nije katika suala zima la wizara kujitahidi katika kuwafundisha wananchi ujasiriamali. Mhe. Spika, ameeleza hapa Mhe. Waziri kwamba wizara yake imejitahidi katika kufundisha ujasiri amali katika mifugo, yaani ufugaji wa kuku, uchongaji na kilimo.

Mhe. Spika, mimi naona bado kuwa ufugaji na kilimo na ardhi tunayo, lakini ardhi hiyo inatumika kwa namna nyingi, kwa sababu ardhi hiyo hiyo

inatumika kwa kilimo, ujenzi. Kwa hivyo kama tutawahamasisha wananchi wote waingie katika eneo la kilimo, basi mimi naamini kwamba serikali au wananchi kwa ujumla hawatoweza kupata soko.

Kwa mfano, hivi sasa tunao msimu wa mazao ya machungwa, lakini utakwenda Marikiti pale utakuta machungwa yanazagaa, yanaoza na hatimaye yanaonekana mtu pengine au mfugaji au mtu wa kilimo anakula hasara, na hii inatokana na kuwa soko bado Zanzibar liko finyu.

Mhe. Spika, mimi naona serikali kuna maeneo muhimu zaidi ambapo kama ingejikita basi pengine wananchi wetu wangeweza kujitatua na umasikini eneo la uvuvi. Mhe. Waziri kwenye kitabu chake hajaonesha kuhusu eneo la uvuvi kama serikali italitumia ipasavyo, basi kweli wananchi wetu wataondokana na umasikini.

Mhe. Spika, eneo la uvuvi bahari ni kubwa na wala haina mwisho, kwa hiyo hata kama tutawachukua vijana 1,000 au 2,000 tukawatie kwenye bahari, kwa ajili ya kuvua basi kweli watavua na watapata kuuza na hatimaye wataweza kujikwamua na umasikini, jambo la muhimu vijana hawa ni kuwapatia nyenzo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, zamani kama tunakumbuka ilikuwa hata kama samaki pengine watavuliwa wengi bado tunaweza tukawafanya ng'onda na mtu pengine kwake anakwambia hasa siku ya Jumapili leo nasonga ugali kwa ng'onda. Lakini siku hizi hakuna, pengine kuna vizazi vipya vinavyozaliwa kama utamuuliza samaki wa ng'onda anamjua atakwambia hamjui. Vile vile samaki wa nguru wanapovuliwa kwa wingi na zamani ilikuwa nguru wale wanatiwa chumvi nyingi wanaanikwa na wala hawaharibiki.

Kwa upande wa mazao machungwa yanaharibika. Kwa hivyo, Mhe. Spika namuomba Mhe. Waziri tuingie hili eneo la uvuvi na bahari yetu Mwenyezi Mungu ametujaalia kwamba tunayo ya kutosha na wenzetu wanaitafuta na vijana hao si lazima kuwapeleka katika meli kubwa, hata hivi vidau tu vidogo vidogo kama tutawawezesha, basi vijana wetu wanaweza kufanya kazi nzuri na wataweza kujipatia ajira na wataondokana na kuzurura mitaani. *(Makofi)*

Sasa nije kwenye suala zima la kuwapatia vijana wetu mikopo na kwamba Mhe. Waziri anajitahidi katika suala hili. Mhe. Spika, hili ni jambo zuri na wananchi wetu kwa kweli wana-*appreciate* kwamba wizara tunayo hivi sasa ya uwezeshaji. Lakini Mhe. Spika ukiangalia pengine wizara na serikali kwa ujumla, kwamba tunaweza kuwa na vikundi vya wanachama pengine 40 mpaka 50. Kwa hivyo, vijana wale kama utawapa …

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwaombe wale wanaotoka nje wakumbuke kwamba muda mfupi Mhe. Waziri atafanya majumuisho na ningependa tupate *quorum* ya kutosha.

Mhe. Mjumbe malizia.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, ahsante. Kwa hivyo, serikali katika hizi *programs* mbali mbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi, basi serikali inawapa fedha pengine vikundi vya watu 50 au 40. Vile vile serikali hiyo hiyo pengine watu wale wanawapa shilingi milioni 1,000,000/= au 2,000,000/=.

Sasa tuangalie je, fedha zile kweli zinawasaidia wananchi katika kuwatatua na umasikini, kwa sababu Mhe. Spika lazima tukubali kwamba biashara ni kipaji na wala sio kila mtu anaweza kufanya biashara, na ndio maana utaona tunawapa wananchi fedha, lakini hatimaye tunalalamika kwamba fedha zile hazijarejeshwa, kwa sababu biashara ni kipaji na kwamba sio kila mtu ambaye anaweza kufanya. Mhe. Spika, serikali tukae na tuangalie njia mbadala ya kuona kwamba wananchi tutawasaidia vipi.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika naomba nimshauri Mhe. Waziri kwamba sasa wakati umefika kwa serikali kuanzisha viwanda vidogo vidogo na halafu viwanda vile vitawasaidia wananchi kuwapatia ajira, kwa sababu inaonekana kwamba hali ya kuwapa vikundi haina *impact* kuwa wanafanikiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naamini kwamba Mhe. Waziri ni mtu mwenye busara pamoja na wataalamu wake, basi wakae chini waone na waandike kwamba labda hivi sasa serikali tuanzishe viwanda vidogo vidogo tofauti, na halafu wale wananchi wetu tuwavute, ili waweze kupata ajira pamoja na kuwasaidia kuwaondosha na umasikini.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba mchango wangu hautakuwa mkubwa, isipokuwa ni mdogo tu kwa sababu mengi tayari yameshazungumzwa na kubwa mimi nilikuwa nataka kutoa msisitizo tu. Kwa hivyo, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri kulikuwa na vikundi mbali mbali naona kama kuna vyengine vimeondoka, lakini walikuja kujumuika na kusikiliza bajeti ya wizara yao, sasa sina hakika kama bado wapo pale.

Lakini kulikuwa na wageni kutoka Jimbo la Kikwajuni, ambao ni wageni wa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Mwenyekiti wa Baraza; nao walikuwa ni

6 na sina hakika kama wapo wakiongozwa na Bi Vista Borafya Silima, na kama wapo basi niwaombe wasimame inaonekana wameshaondoka. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe nilitaka mutambue kwamba walikuwepo kwa ajili ya kusikiliza bajeti hii na walichelewa kidogo kufika. *(Makofi)*

Baada ya hayo sasa niwakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hivyo, sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha asubuhi ya leo kuendelea kujadili Hotuba ya Wizara yetu ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa wale ambao wako nje basi naomba sasa waingie ndani, kwa ajili ya kumsikiliza Mhe. Waziri akifanya majumuisho na hatimaye kumaliza shughuli hii.

Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, niwashukuru Wajumbe wote ambao wamechangia Hotuba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, jumla ya Wajumbe waliochangia kwa kusema ni Wajumbe 18 na waliochangia kwa maandishi ni Wajumbe watano (5). Kati ya Wajumbe hao, Wajumbe wote isipokuwa wawili tu ndio ambao wamesema hawakuunga mkono hotuba yetu. Lakini *inshaallah* natarajia mpaka nitakapomaliza maelezo yangu basi watakuwa wameshaiunga mkono hotuba yetu. Wametumia uwezo wao na nafasi za kidemokrasia na wana haki ya kutetea wananchi katika majimbo yao.

Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako niwashukuru Wajumbe wote kwa ujumla, waliozungumza, walioniletea kwa maandishi na waliosikiliza kwa sababu na wao wana mchango mkubwa sana katika suala zima la kuimarisha Sekta hii ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Naomba kwa sababu maalum nimpongeze sana Mwenyekiti, Mhe. Mlinde Mabrouk Juma Mwenyekiti wa Kamati yetu. Kuna mmoja alipokuwa anakwenda kutoa taarifa ya Kamati yake akasema huyu Mheshimiwa hasemi sana lakini inaelekea akisema atasema kweli.

Mhe. Mlinde kweli alipokuja alitoa taarifa nzito za kimsingi na nakushukuru sana kwa kipindi kifupi ambacho umeiongoza Kamati hii basi tumekwenda

vizuri sana. Kama tulivyokuwa sisi tukiwasilisha bajeti hii, tuliwasilisha kwa dakika 40 na yeye kawasilisha kwa dakika 15. Kwa hivyo kamati imefika ndipo na wizara ipo katika kamati inayohusika. Niruhusu Mhe. Spika, niwataje wale wote ambao wamechangia, nao ni kama wafuatao:

1. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Kazija Khamis Kona
4. Mhe. Marina Joel Thomas
5. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
6. Mhe. Hamza Hassan Juma
7. Mhe. Salim Abdalla Hamad
8. Mhe. Ali Salum Haji
9. Mhe. Mohammed Haji Khalid
10. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
11. Mhe. Farida Amour Muhammed
12. Mhe. Fatma Mbarouk Said
13. Mhe. Rufai Said Rufai
14. Mhe. Salma Mussa Bilali
15. Mhe. Ashura Sharif Ali
16. Mhe. Panya Ali Abdalla
17. Mhe. Salma Mohammed Ali
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk

Waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:

19. Mhe. Nassor Ali Salim
20. Mhe. Abdi Mossi Kombo
21. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
22. Mhe. Abdalla Juma Abdallah
23. Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Kama yupo Mheshimiwa ambaye amechangia namuomba radhi basi aniandikie ki-*note* naye nimtaje vile vile.

Hoja nzito zilizozungumzwa ni nyingi na zinahitajia ufafanuzi wa kina. Wizara hii ni mpya ina umri wa miaka miwili na nusu na kidogo, lakini namna ilivyochangiwa na baadhi ya Wajumbe ni kama wizara ambayo ipo karibu miaka kumi, vidonda vya siku nyingi zimeletwa hapa vitibiwe. Hoja ambazo nimeziona ni hoja 12 za kimsingi, nitajaribu kutoa ufafanuzi wa kila hoja. Pale ambapo nitataja hoja, nitataja baadhi ya Waheshimiwa ambao wamechangia lakini kwa sababu maalum na kutokana na mchango mzito alioutoa. Mhe. Mshimba naomba yeye nitamuweka mwisho hata kama

alikuwa wa mwanzo, kwa sababu ilibidi nikatafute vitabu, ma-*dictionary* makubwa makubwa ya sheria ili kuangalia kwa njia gani naweza nikamjibu rafiki yangu ili roho yake ikarudi kurejesha mabalozi wake aliowahamisha kwenye ofisi yangu.

Mhe. Spika, Mhe. Mshimba amehamisha ofisi za kibalozi katika Wizara ya Kazi na urafiki uliokuwepo wa Maalim Harouna na yeye umetoweka kwa kipindi cha miezi mitatu. Natarajia mpaka nikimaliza hotuba hii basi mabalozi wale watawarejesha na tutaendelea na uhusiano wetu kama kawaida. Nadhani zile shilingi zimeanza kurejeshwa sasa Mheshimiwa.

Suala la msingi ambalo nataka nilianze mwanzo na kwa sababu la kidini na zito ni suala la mfuko wa Zakka. Naomba univumilie kidogo Mhe. Spika, nisome muongozo wa shughuli za Zakka Zanzibar. Kitabu hiki kimeandaliwa na Ofisi ya Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba chini ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa kushirikiana na Jumuia ya Taasisi za Kiilamu Zanzibar. Hawa ni Mashekhe wakubwa wamekutana. Naomba nisome utaratibu unaohusika katika utoaji wa pesa hizi za Zakka. Ni vizuri Waheshimiwa tukazisikiliza tukazielewa. Humu ndani kuna nyengine zimeandikwa katika lugha ya Kiarabu, nyengine kwa Kiswahili, mimi nitazisoma hizi za Kiswahili.

Waheshimiwa wengi wamezungumzia utaratibu wa utoaji pesa hizi za Zakka, ni sawa wala sioni kama ni tatizo kuzijadili. Wengine walipendekeza pesa hizi zipelekwe Misikitini, wengine watafutwe mafukara na masikini, wengine wapewe vikundi hivi hivi vilivyopewa kwa sababu vikundi hivi zinavyopewa sio kama ni matajiri ni maskini vile vile. Kila mmoja alikuwa na jinsi anavyoona yeye alifahamu.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu mambo ambayo yameandikwa kwenye kitabu hiki na nina hakika baada ya maelezo haya hata majumuisho yangu ya mfuko wa Zakka basi hayatokuwa yanahitajika zaidi. Mhe. Abubakar naomba ukae tayari kwa sababu naweza nikakosea kidogo hapa na wewe ndiye Mufti wetu humu ndani.

Namna Zakka inavyotolewa

Zakka itatolewa kwa utaratibu utakaowekwa na mamlaka inayoshughulikia Zakka. Utaratibu huu unaweza kutofautiana kwa kuzingatia mazingira, mahala, hali na aina ya watu wanaopewa zakka hiyo. Utaratibu ni lazima uzingatie lengo la Zakka kwa kila kundi.

Lengo la Zakka kwa masikini na mafukara ni kuwapa mtaji wa kuondosha umasikini na ufukara wao na sio kuwapa chakula au pesa za chai. Hivyo kiwango kinachotolewa kiendane na malengo ya Zakka. Aidha kunahitajika upatikane ushauri wa kuwaongoza wapewaji ili wazitumie vizuri fedha na mali wanazopewa katika kujiletea maendeleo na sio kuzifuja.

Inahusika Maeneo ya Kupewa

Misaada unaweza kutoa Zakka katika biashara, au msaada wa ujuzi na uwezeshaji katika ujasiri amali.

Kuwekeza Katika Mali za Zakka

Ni vyema mfuko wa Zakka ukawa na fedha ambazo zitawekezwa ili zijizalishe na kufanya mfuko uwe endelevu katika kukidhi mahitaji ya wahusika na kuchangia maendeleo ya kijamii.

Miradi Yenye Manufaa Kiuchumi

Hii ni miradi yote inayopelekea kupunguza umasikini na kuwafanya watu wawe na uwezo wa kutoa zakka; mfano wa miradi hii ni uwekezaji katika viwanda, uvuvi, kilimo, ufugaji na biashara kupitia uwezeshaji na wajasiri amali wadogo wadogo na wakati wa kuwajengea uwezo kielimu na kifedha na ndivyo Wizara ya Kazi Uwezeshaji Kiuchumi kwa kushirikiana na Wakfu na Mali ya Amana tulivyoshauriana"

Kwa hivyo hayo ni maelezo yaliyotufanya sisi tukashirikiana na wenzetu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Tumepata mashirikiano mazuri sana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Mhe. Spika, amini Mungu kwamba vikundi vile vya Ushirika tulivyovipa walishukuru Mungu na vimeanza kufanya kazi nzuri. Hata vile vikundi ambavyo vyengine Waheshimiwa wamevizungumza vimeletwa, tumetumia utaratibu wa Kamisheni ya Wakfu, Maafisa Ushirika wamekwenda wenyewe Wilayani katika vikundi vyote wamekipitia kimoja hadi kimoja. Kwanza kwa upande wetu ni vile vikundi ambavyo vilisajiliwa na vikapata usajili ndio iliyokuwa *criteria* kubwa. Mambo mengine ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na hatimaye vikajitokeza vikundi vile.

Naomba Waheshimiwa tuwe wastahamilivu tumeanza na vile vikundi vyote kama Mhe. Salma alivyosema na vyengine ambavyo hatukuvipatia. Basi vile tutavipa kipaumbele katika awamu hii inayokuja tukijaaliwa. Hatutoi kwa sababu ya kumridhisha kila Mwakilishi katika Jimbo lake. Tunatoa kwenye

vikundi vile kama viko vitano au sita lakini vimejipanga vizuri, vimekaa vizuri, vimejisajili na vinafanya kazi ambayo inaweza kuleta matarajio tutavisaidia. Kwa hivyo Jimbo moja wanaweza wakapata 10 wengine wakapata viwili kutegemea kwa jinsi tunavyoweza kuvisaidia vikundi vyetu vya ushirika.

Maana yake sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuwe tayari kwenda tukawasaidia wana ushirika. Nasema kuna mtaalamu tumemleta kutoka India alikuwa Rwanda yupo, kenda Gando kule. Mheshimiwa wangu amezungumza hapa, nikashukuru kazi aliyoifanya kule Mhe. Bikame alizungumza hilo. Yule, Mtaalamu Ms. Rajim yupo hapa, hebu twendeni Gando tukatizame Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo) kazi kubwa aliyoifanya pamoja na wale Wawakilishi wa viti maalum waliyoifanya kule.

Jamani tutumie nafasi hii Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi siku niliyosema kwamba tuleteeni orodha ya vikundi ili na mimi niangalie uwezekano wa kukusaidieni wenzangu. Wallahi wengi hawakuleta mpaka leo na hapa unakuja kusimama sasa unalaumu. Tutendeane haki jamani kidogo. Mimi napenda kuwa shirika, sina upendeleo, sina ubaguzi, simbagui mtu kwa itikadi yake wala kwa rangi yake. Nikianza kubagua nitizameni hivi nilivyo mimi si mtanibagua zaidi. Kwa hivyo sera hiyo haipo. Hili nataka kidogo nije kumtolea taaluma rafiki yangu Mshimba. Nataka nije nimpe taaluma kwa sababu katumia maneno mawili mazito sana. Namwambia kwa nia nzuri kabisa, ili tukimaliza hapa wale mabalozi uliowahamisha uwarejeshe bwana hakuna haja ya tofauti sisi ni wamoja. Sisi ni wamoja tushirikiane Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaendesha nchi yetu. Lakini nakuweka mwisho tulio kidogo Mhe. Mshimba utaridhika na hayo nitakayokueleza.

Mhe. Spika, hoja zilizojitokeza likiwemo na suala la ajira. Ikiwemo suala la mikataba kwa wafanyakazi katika sekta binafsi. Mikataba ni hii miaka miwili ndiyo tumeanza kuiendea mbio kuifanyia kazi. Mikataba ilikuwa haipo na mpaka leo tunaamini na tunakubali kwamba baadhi ya taasisi hawajawapa mikataba wafanyakazi wao, tumefanya kazi kubwa.

Mhe. Mshimba, aliposema kwamba itafsiriwe kwa Kiswahili, tumefanya hivyo na sasa hivi mikataba ipo kwa Kiswahili ipo tayari. Nakushukuru sana kwamba umeliona hilo. Kwa sababu wanapowapa mikataba ya kizungu wanawafunga funga wafanyakazi wetu matokeo yake masikini haki zao na fursa zao wanazikosa. Hapa naliunganisha na ajira za Wazanzibari katika mahoteli. Nitakuja kutoa takwimu huko mbele, lakini vijana wetu waliopita Maruhubi pale wameshahitimu wengi na mimi nilikuwa mgeni rasmi, Mhe. Said Ali Mbarouk alinialika pale.

Vijana wengi wamepata mafunzo mazuri kwenye Chuo cha Utalii. Nikatangaza siku ile nikasema natoa *signal* kwa Mameneja wa Mahoteli, Wakuu wa taasisi mbali mbali kwamba sasa waliowapa mikataba wageni ambao kazi zile zinaweza zikafanywa na Wazanzibari. Mikataba ile hatutoirejea tena na hatutotoa kibali, lazima tuhakikishe kwamba Wazanzibari tunawapa fursa hiyo ya kwanza na wanaajiriwa ndugu zetu. Hata nina takwimu zaidi ya vijana 400 tumeanza kuwapeleka kwenye ajira hizi za mahoteli. Tutalifanya hilo tutaliendeleza, ndio kwanza tumeanza.

Mimi nimewafukuza wageni wawili nchi hii kwa kutumia uwezo wa kisheria kwa kushirikiana na Uhamiaji kwa kuwadhalilisha Wazanzibari. Kamati yetu ya Mifugo ile iliyoondoka iliyomaliza muda wake walikwenda kwenye hoteli fulani badala ya kupokewa na binaadamu wakasukumiziwa mbwa pale, wakafurushiwa. Mhe. Asaa na wengine labda wanakumbuka katika hoteli hiyo. Yule kapewa masaa 24 kaondoka. Kuna mfanyakazi mmoja wa kigeni alikuwa hoteli ya Neptune, alifanya vitendo nje ya madili ya Kizanzibari, tumempa masaa 24 ameondoka. Taarifa zile nililetewa ofisini kwangu, tunapokuja kuzungumza hapa ukinambia kuna mtumishi wa kigeni anawadhalilisha Wazanzibari kama mimi hujaniletea ofisini kwangu utakuwa hukunitendea haki.

Nakuombeni sana Waheshimiwa, tusingoje kwenye vikao kama hivi tukasema yale madukuduku yetu. Njooni Ofisini kwetu ya Wizara ya Kazi hata paa haijatiwa kama unaona tabu kupitia kwenye milango pitia kwa juu utafika tu kwangu mimi. Tatizo liko wapi? Unakuja kumbana Waziri mshahara wake unataka kuuchukua kwa sababu mgeni yule anawadhalilisha Wazanzibari. Lakini hujaniletea hilo, unaishia kwa maafisa wangu. Kama maafisa wangu hawakutendei haki njoo unambie na wao pia nitawachukulia hatua.

Mhe. Spika, naomba tuelewane kwamba tumekuja hapa kuja kusaidiana haipendezi, tukakusanya matatizo yote huko ukaja ukambambikia Waziri hapa. Jamani akili vichwa ndio hivi hivi, tuna mengi vichwani mwetu. Na mimi mmoja katika Mawaziri kama walivyo Mawaziri wanzangu wote tunakukaribisheni kwenye maofisi yetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nikisikia kuna Mwakilishi, hata kama kuna wageni 100 nitakupa fursa wewe.

Mhe. Mshimba ushakuja ofisini kwangu si mara moja wala si mara mbili na yale uliyajia yote Wallahi nimekutengenezea na saumu yangu hii. Inakwenda kwendaje kwa hili jengine basi tu kwa sababu ya kuhamisha mabalozi imekuwa balaa tena jamani, haifai. Mie nafurahi leo unacheka mbele yangu kama hivi, Wallahi nafurahi nataka ucheke mpaka mwisho ukiondoka hapa fat-ha.

Mhe. Spika, tumejitahidi tatizo jengine ni la ajira za watoto nitalizungumza. Kasema hapa ajira za watoto Mhe. Amina kalizungumza vizuri, tusifikirie lile la kubanja kokoto tu, wanapara samaki, wanapara miwa, wanafanyishwa kazi ngumu lakini pia wale wanaowapa punda wale watoto vile vile wakawakimbiza. Kazi zozote ambazo zitamdhalilisha mtoto mdogo umri ambao hauwezi mtoto kufanya kazi zile zote ni kazi tunaziita ni ajira mbaya. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapiga marufuku, ajira zote za kuwadhalilisha watoto.

Mhe. Spika, *Save the Children* imefanya kazi ya ziada, tumeshirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, maafisa wao tumewarejesha skuli, watoto karibu 398 na tuna mpango wa kuwarejesha zaidi ya idadi hiyo mpaka wale 5,000 wote tuwarejeshe maskuli wapate elimu kama wananchi wenzao, lakini hili sio la Mwalimu Haroun Suleiman peke yake, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna jukumu katika maeneo yetu. Tushirikiane na Masheha wetu, tushirikiane na maafisa wetu wa elimu, ili tuwatafute vijana hawa na tufanye kila litakalowezekana tuwarejeshe katika utaratibu ule wa skuli.

Mheshimiwa mmoja amesema hapa kuwapa mikoba na mabuku haijatosha, lakini si ndio tumeanza? Walikuwa hawapewi hata mabuku na sare hawapewi, lakini ndio tumeanza. Familia zile za wazee tumewasaidia tumewapatia nyenzo za kuwasaidia kimaisha vile vile, kwa sababu hali zao ni masikini mno. Hata baadhi yenu mkasema zile pesa za Zakka basi tuwape wale watoto ambao wanahangaika wanafanya kazi mbaya ambazo wazee wao ni masikini. *Inshallah* katika vifungu vya fedha vinavyokuja hivi tunajitahidi, familia zile nazo tuziangalie kwa uzuri zaidi ili nazo zijisikie kidogo katika maisha yao.

Mhe. Spika, hawa Waheshimiwa wanafahamu kwa hiyo sihitaji kwenda ndani sana, nitakwenda juu juu tu. Ufafanuzi baadhi ya vifungu ni Mhe. Mahmoud peke yake nimletee makabrasha yake *Inshallah* tukimaliza kikao nitampa ataridhika wala hakuna mashaka.

Vikundi vya Ushirika. Heeh! Mheshimiwa wangu unanikatalia shilingi kwa sababu vikundi vyako havijasajiliwa. Leo nakwambia hivi mimi nipe wiki moja tu nakuhakikishia vikundi vyako vyote vitasajiliwa *Inshallah* bila ya matatizo yoyote. Na huyo Afisi ambaye amekukwamisha kama hajanipa sababu maalum basi mimi na yeye tukijaaliwa. Kwa sababu katika eneo ambalo nalalamikiwa sana ni vikundi vya ushirika, maafisa wangu wanawacheleweshea watu, wananyanyasa watu hawa waliokuwa Wilayani. Kama wamechoka kazi basi mimi nitatafuta wengine, lakini mpaka nihakikishe kama kweli kahusika yeye.

Tatizo lilokuwepo Mheshimiwa unatakiwa wakati mwengine ukamilishe taratibu, lete hiki lete hiki, sasa kama hujapeleka utakaa mwaka mmoja au miaka miwili. Ninachokuombeni Waheshimiwa tufuatilie kwa pamoja sote, tuleteeni vikundi hivyo na viwe vimekamilisha taratibu, kawaida pale siku mbili au tatu haizidi. Mimi walikuja wananchi wa Jimboni kwangu, wakanambia tumekwenda Wilayani kule tumehangaishwa. Nikawauliza mmehangaishwa vipi. Wakasema mara tunaambiwa hivi mara tunaambiwa hivi, mara tutoe pesa hizi. Wakati pesa zilizotajwa zilikuwa ni kiwango kikubwa kuliko kile cha kawaida cha elfu thalathini (30,000).

Nikamtaka Mkurugenzi niletee Afisa wa ushirika, akanambia nakuomba asije mbele yako, nitamalizana naye mimi. Akazungumza naye ni kweli alitaka pesa za nyongeza pale. Sasa hayo yanawezekana siyakatai, lakini Mheshimiwa naomba sana ile shilingi irejeshe haraka ili tuweze kuishi maisha mazuri kama wewe unavyoishi tukijaaliwa. Nadhani utakuwa umeridhika. Kwa ujumla vikundi vya ushirika hivi vinahitajia vyote tuvisajili lakini pia si vyema tukawa na utitiri wa vyama vya ushirika vingi. Tujikusanye pamoja wenzetu wa Fuoni wamejaribu kufanya hivyo, wenzetu wa Gando wamefanya hivyo na SACCOS nyengine zimefunguliwa funguliwa katika maeneo mbali mbali. Tuandae utaratibu tuvikusanye pamoja ili tuendelee kuzungumza na wahusika ili tupate misaada.

Mhe. Hamza Hassan Juma, alizungumza Sera ya CRDB; waliweka ahadi kusaidia na mabenki haya. Nitakuja kukupa takwimu jinsi CRDB walivyoweza kusaidia SACCOS zetu mbali mbali na hatimaye leo wananchi wetu tayari wanazungumza suala la umasikini kama la kihistoria hivi na tutafika hapo. Hasa uanzishwaji wa Benki ambayo nitakuja kuizungumza baadaye.

Mhe. Spika, kwa ujumla nataka niende kwenye maelezo ya undani kidogo sasa hivi kwa watu fulani fulani. Mhe. Mshimba nimesema bora nimuweke mwisho kwa sababu nahitajia maelezo maalum kwake yeye. Suala la kutembeza watalii limezungumzwa na wengi, mimi nakubali. Mwaka jana liliulizwa hili, nakumbuka Mhe. Ismail Jussa Ladhu alilizungumza hili kwamba hawa watembeza watalii, kwanza historia yetu ya Zanzibar hawaijui.

Mheshimiwa hili naliahidi tutalifanyia kazi ya uhakika kabisa. Sio ile kazi inayojulikana kama *business as usual*, wala hatutokwenda kulikalia kitako, tukilikalia kitako halitokuja juu hili. Tuhakikishe kwamba Wazanzibari tuna ma- *graduate* wazuri tu wamemaliza skuli sasa hivi hawajapata ajira, kuna vijana wamemaliza diploma na wengineo. Tutawaandalia *program* maalum tuwaelimishe na ikiwezekana tuwapatie mafunzo ya historia ya Zanzibar ili waweze kuwatembeza watalii.

Mhe. Spika, wageni pia tutawafuatilia mmoja mmoja lakini suala hili bahati mbaya halipo kwenye Mamlaka ya Wizara yangu ni Wizara ya Utalii. Bahati nzuri nikimaliza mimi tu anakuja Waziri wa Utalii, sasa naomba tuhamishe maswali mengi ya utalii tumngojee Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo) atawasilisha. Namuahidi mimi niko tayari kushirikiana naye kuhakikisha kwamba tunawaweka Wazanzibari katika kutembeza wageni.

Mhe. Spika, mawakala binafsi wa ajira. Tumejitahidi, hivi sasa kuna taasisi sita za mawakala hao, wameshasajiliwa kwa lengo la kuisaidia serikali katika kukuza ajira kwa vijana wetu. Wanafanya kazi vizuri Mheshimiwa. Kwenye kitabu changu cha bajeti nimeeleza na nimetoa takwimu ni vijana wangapi wamepatiwa kazi na hivi sasa waliokwenda nje pia ni wangapi wamepatiwa kazi.

Mheshimiwa mmoja aliuliza wanafanya kazi gani huko? Swali gumu kidogo, lakini wengi wao ni wahudumu wa nyumbani, madereva na kazi nyenginezo. Lakini tumehakikisha kazi wanazozifanya ni halali mikataba yao. Kama wamekwenda nje mambo yamebadilika tuletewe taarifa, tuna barua mbili kutoka Oman na tuna barua mbili kutoka Saudi Arabia zimeletwa na mabalozi wetu.

Mwaka jana nilisoma hapa barua ya kutoka Saudi Arabia jinsi ya manyanyaso wanayofanyiwa Wazanzibari, wafanyakazi wetu wanapokuwa nje. Wakati ule ilikuwa Wizara yetu ilikuwa haijaweza kuratibu shughuli hizi vizuri. Imefika wakati mfanyakazi wa majumbani anafanyishwa kazi saa 24, aamke alfajiri awakogeshe watoto, awape chai, awapeleke skuli, anangoja nyumbani aje aandae mambo mengine, kufua nguo, kupiga deki na mambo mengine kama hayo na zaidi ya hayo na mengine mengi.

Nyumba ile aliyepewa ajira ile akiondoka yule tajiri wa pale basi anamuachia jirani yake sasa. Yaani imekuwa kama ah! Sitaki kutumia neno la kitumwa tumwa kwa sababu ni baya kidogo. Nitumie neno la kwamba inakuwa wamepata mtumishi, sasa wanamfanya kama ni kitambaa cha kujifutia mikono, hivi inakuwa haipendezi. Tumechukua tahadhari na wale wote waliohusika tumechukua hatua za kufaa na hatutarajii tena madhila kama yale. Ikiwa kama Waheshimiwa mnayo taarifa kwamba manyanyaso hayo yanaendelea njooni munione mimi. Tutawasiliana na mabalozi wetu moja kwa moja na hatua kali zitachukuliwa.

Mhe. Spika, hapo mwanzo kulikuwa kuna utaratibu wakifika tu paspoti wananyang'anywa, simu wananyang'anywa. Eeh! Sasa umekwenda kufanya kazi za majumbani basi hata kuwasiliana nyumbani wasifanye mawasiliano

hayo, hatukubali. Kwenye mikataba yetu ya sasa hivi ya Kiingereza na Kiswahili yote tunaweka wazi maeneo ambayo yanawajibika. Tumependekeza sasa hivi kuwa na kifungu maalum cha kuchangia Mfuko wa ZSSF wanapokwenda kupata ajira kama hizo ili ziwasaidie kwa hatima yao ya huko mbele.

Mhe. Rufai Said Rufai ulitaka maelezo ya Qatar ni hayo tunafuatilia zaidi. Kama Kenya wamewarejesha sisi hatujapata taarifa hizo kwamba Kenya wamerejesha. Isipokuwa najua *Philippines* na nchi za *Far East* kuna wakati walirejesha vijana wao kutoka Falme za Kiarabu kutokana na matatizo kama haya, mpaka serikali zikaingilia kati, Mawaziri na Viongozi Wakuu wakaingilia kati wakasawazishana. Kama itatokea Wazanzibari wana tatizo kama hili mimi niko tayari. Hata ikibidi kwenda nitakuja kukuomba na wewe tufuatane pamoja ukanisaidie hiyo kazi ya huko. Kwa sababu hatutaki kudhalilishwa na Mhe. Mshimba kalizungumza sana wanadhalilishwa huko na wanadhalilishwa hapa, lakini kama wanadhalilishwa hapa tuleteeni, walioleta tumechukua hatua, hamjatuletea hatuwezi kuchukua hatua.

Mhe. Spika, tumeweka taarifa hizi ili zisaidie naomba uniruhusu niyasome haya kwa sababu yana takwimu ili niwasaidie Waheshimiwa Wajumbe.

Wizara inakubaliana na ushauri wa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, suala la wazalendo kupewa ajira katika maeneo yetu, wala hatuna pingamizi na hilo. Haki yake tumpe pale anapofanya vizuri tumpongeze na pale anapokosea tutamuelekeza. Wizara hii inakubaliana na wazo lake, serikali kwa ujumla katika utafiti uliofanywa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi ZIPA na ripoti yake imepatikana mwaka 2012 inaonesha kwamba

Wazanzibari walioajiriwa kwa nafasi za wataalamu (*skilled*)	4,315
Kutoka Tanzania Bara	1,676
Kutoka Nje ya Tanzania	316

Kwa hivyo hapa Wazanzibari walioajiriwa wenye utaalamu ni 4,315 na si nambari za kubahatisha tu. Mimi sikubali nambari za kuletewa ninahakikisha na mimefuatilia na nimehakikishwa kwamba ni kweli.

Unskilled taarifa zinaonesha kwamba Wazanzibari	2554
Tanzania Bara	1071
Mgeni kutoka nje ya nchi	0

Katika hizi sekta au nafasi ambazo si za kitaalamu hakuna mgeni aliyekuwa ameajiriwa hapa.

Kwa nafasi za Uongozi (*Management*).

Ripoti inaonesha Wazanzibari waliokuwa wana nafasi za Utawala 302 kutoka Tanzania Bara waliopewa nafasi hizi 93 na wageni ni 315, hapa wageni ni wengi kwa sababu ni zile taaluma maalum, na hii taaluma maalum nazo tunazifuatilia, kama taaluma hii tutahakikisha kwamba wapo Wazanzibari basi mikataba yao ikimalizika tu watawachukua wazanzibari katika nafasi ile hilo tutalifuatilia kwa nguvu zetu zote.

Hivyo nafasi mbili za awali zinaonesha Idadi ya Wazanzibari kuwa kubwa ikilinganishwa na wengine. Wizara kwa sasa imo katika juhudi ya kuimarisha kitengo cha utoaji wa taarifa la soko tunakusudia kukusanya taarifa zaidi kwa lengo la kuwasaidia Wazanzibari kuajiriwa kwenye taasisi lipo ndani na nje ya nchi. Tumeanzisha kituo chetu pale cha kujiorodhesha ili tuweze kujua wangapi wanahitaji ajira.

Mhe. Bikame kuna wakati ulizungumza kwamba ni vizuri Wizara hii ingeshirikiana sana na Wizara ya Ustawi wa Jamii, ni kweli na mimi na Mhe. Zainab tunashirikiana sana, lakini Mhe. Mshimba yeye alisema nadhani alikusudia Wizara hii iwe bora iwe na utaratibu maalum, kwa hivyo ingehamishiwa kwa Mhe. Zainab kwa sababu yeye ni mwanamke jasiri sana Mwalim Haroun Bado hajaiva, kwa hivyo yeye angepumzishwa akatafutiwa kazi nyengine nadhani ndio ilikuwa dhamira au sijui kama alikusudia vipi lakini alitaka masuala haya ya vijana, wanawake mambo ya kusaidia vikundi vya ujasiri amali vyote vihamishiwe huko, sasa mkinihamishia sekta zote mimi si nitatafutiwa kazi nitakwenda kwetu Makunduchi kwenda kukaa.

Lakini mimi ninachofanya hata suala la ajira za watoto mimi si jukumu langu kuwashughulikia watoto wadogo huduma zao mbali mbali, mimi ninalozungumza zaidi suala la ajira mbaya za watoto ni suala la *labour* tu. Huduma za watoto, Ustawi wa Jamii kila kitu kwa Wizara inayohusika, na hawa vikundi vya akinamama Mhe. Zainab anavyo kweli ni vyake, lakini linapokuja suala la uwezeshaji pesa ziko kwetu sisi na hili jukumu la Wizara si dogo, hata hawa vijana Mhe. Mshimba aliyesema wawezeshwe hizi pesa baada ya kukaa kwa Mwalim Haroun zipelekwe kwa mwanamme jasiri huyu Mhe. Zainab *hansard* yako ndivyo inavyosema hivyo. Sasa nitajitahidi nionekane jasiri kidogo ili nimridhishe rafiki yangu kwamba nimefanya na tumejaribu kadri inavyowezekana kushirikiana na wenzetu. Kuna vijana hawa wanaopanda maua ya *rossela* wanaofanya kazi kule Tunguu Waheshimiwa wamesema tuwawezeshe, jitihada tuchukue, tumetoa pesa *not less 17 million* tumewapa lakini haikufanyika vizuri. Sasa hatuwezi kutoa pesa za serikali ikawa mahali hapana tija.

Na mimi ninashukuru upande mmoja Wizara ya Fedha hawakutupatia pesa zote kwa wakati mmoja na tungezitoa pesa zile *in millions* zingepotea bure bure, na pale ambapo wamefanya vizuri tutawaongeza. Kuna Mheshimiwa alizungumza suala la masilabi yale tumejenga manne tu na tulitaka tujenge kumi hapa pana matatizo. Shirika la Umeme wanasema hapa hamuwezi kujenga kwa sababu panapita waya wa umeme mkubwa. Manispaa wanakwenda pale wanasema hapa ndipo panapotufaa. Tumekaa tunasubiri Manispaa, Shirika la Umeme, Wizara ya Tawala za Mikoa wakae watuletee pesa zipo tunashukuru sana. Mhe. Omar ametoa fedha kwa kiasi kikubwa katika kusaidia miradi hii, lakini matatizo yetu wenyewe mimi ninazo pesa tu lakini si dhamana ya manispaa na *alhamdulillahi* ninamshukuru sana Rais kuamua pesa zile na Waziri wangu wa Fedha huyu kuamua pesa zile azilete Wizarani kwetu. Tutazisimamia vizuri na tutaendelea kuzisimamia na tuhakikishe pale ambapo pana tija tutapeleka pesa, pale ambapo pana matatizo tutarekebisha matatizo halafu baadae tutawasaidia kwa pesa.

Mhe. Kazija aliuliza swali moja hapa hapa pana mahesabu kidogo, mwaka juzi ananambia Mhe. Ismail nimfahamishe kidogo kwa sababu alipokuwa darasani alikuwa hodari kiasi. Katika urejeshaji wa mikopo ile mfano ya AK, JK tumeona kwamba kwa kipindi cha mwaka kwa mfano 2010 Mhe. Kazija nataka unisikilize vizuri; 2010 mpaka 2012 pesa zote ambazo zimerejeshwa kama zilikuwa zirejeshwe 500 zimerejeshwa 300, lakini kwa miezi kumi hii zimerejeshwa 80, kwa hivyo nasema mbona huku nyingi huku ziko kidogo zile ni za miaka 2 hizi tulizoziweka hapa ni za miezi kumi tu. Sasa usione kwamba huku kuna 41 huku kuna 100, ndio zile 100 ni kwa sababu zimeanzia kule tunasema ni *commulative* zimeendelea mpaka zimefika pale tukatoa kile kiposho cha miezi kumi ndio tukakiweka pale, kwa hivyo tusione kidogo hapa pana mahesabu kidogo na kwenye zile takwimu zile *tables* mkiziangalia vizuri zitakusaidieni sana na zinahitajia kidogo utulivu kuzisoma. Nambari zina matatizo wakati mwengine zinaweza zikakubabaisha.

Mheshimiwa ajira za watoto zimechangiwa na wengi sana hapa Mhe. Salma, Mhe. Rufai, Mhe. Bikame, Mhe. Mlinde, Mhe. Kazija, Mhe. Hamza, Mhe. Ashura, Mhe. Amina. Nimelitolea maelezo ya kutosha suala hili sitarajii kwamba tutapata masuala ya nyongeza, lakini Mhe. Salma wazo moja zuri sana kwamba watoto hawa wakisharejeshwa skuli kuwe na ufuatiliaji ili wasije wakarudia tena sawa na lile suala la madawa ya kulevya na wale ambao tunawaweka katika *sober houses* tujitahidini sana na sisi upande wa Wizara yetu tumeliingiliaje suala hili la *sober houses;* tunawasaidia tunatoa mafunzo kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na walikuja maskini ya Mungu wakalalamika kwetu sisi wakatwambia sisi hata familia zetu zimetukataa hawajatuamini bado, tukachukua jukumu kwamba tutashirikiana nao na *inshaallah* tukimaliza mwezi mtukufu wa Ramadhani tutapitia familia

moja moja ili kwenda kuwaombea radhi wale watoto ambao wamekataliwa katika familia zao ili tuwarejeshe na wajihisi kwamba ni sehemu ya wananchi wa nchi hii.

Sasa na suala hili la kwamba watoto hawa wasije wakarejea nasema tena suala letu sote tushirikiane kwa pamoja, wizara peke yake haitoweza kufanya hivyo, lakini tushirikiane Wizara ya Ustawi wa Jamii na sisi Wawakilishi ili tuweze kufanya kazi vizuri zaidi. Amependekeza jambo moja zuri sana mimi naliunga mkono Mheshimiwa tuanzishe vikamati hivi vya huko ajira mbaya katika kila Wilaya, hili tunalichukua tutakwenda kulifanyia kazi kwa umakini sana, ili tukishirikiana na wahusika tuweze kuunda hizo kamati ili kuwatafuta hasa wale watoto kila sehemu walizo.

Mhe. Mlinde, Mhe. Kazija alizungumza suala zima la ajira hizo mbaya za watoto, na sasa hivi tumeshakuwa hatua hizo na maelezo ni hayo Mhe. Spika.

Mhe. Marina nadhani suala lile la kibajeti na ameuliza suali zima la kwa nini Wilaya nyengine kuna pesa nzito nyengine ziko hivi, inategemea na maombi yanayokuja. Anasema *ndege anayeamka mapema ndiye anayekula vizuri zaidi*. Sasa sisi wajibu wetu kuwaelimisha wanoomba wanaleta hata hapa tuliposema pale Wawakilishi walete vikundi vyao wengine hawakuleta mpaka leo, walioleta wamenufaika. Sasa siku ile natoa pesa zile za zakka Waheshimiwa ndio wakaja siku ile wakasema na mimi vikundi vyangu ikawa kazi kubwa, Mungu ametusaidia.

Mhe. Spika, suala la wafanyakazi wanaokwenda nje mikataba yao tumesema kwa urefu na kwa makini kabisa kwamba tunaiangalia hatutokubali kuona wakati wowote ule kwamba Mzanzibari ananyanyaswa anapokwenda nje.

Mhe. Spika, katika hatua nyengine ya kuwalinda na kuwahakikisha wafanyakazi hao ndio nimesema tumeshapeleka majina yao karibu majina 200 sasa hivi wako katika mfuko ule wa huduma za jamii au ustawi wa jamii wa ZSSF.

Mhe. Mahmoud naomba unisamehe kidogo nitasema jambo hapa si kwa nia mbaya, wewe ninakujua ni Mwakilishi makini, hodari unafuatilia Jimboni kwako. Sasa nataka unisikilize haya maelezo ninatakayosoma halafu utanambia.

Kuhusu kikundi cha *Zanzibar Youth Icon* kilichopo Kikwajuni Jimbo la Mhe. Mahmoud ni miongoni mwa vikundi vya vijana ambavyo kwa mara mbili vimepatiwa mafunzo ya kazi nje nje. Ulisema hatuwapatii mafunzo tujitahidi kuongeza hivi, na hivi sasa mimi nakwambia mara mbili tushakuja kwa lengo

la kuwajengea uwezo juu ya kuunda wazo la biashara, kuanzisha biashara na kujaza mpango wa biashara ambapo vijana 85 katika Jimbo lako wamenufaika Mheshimiwa. Kwa madhumuni ya kuwaendeleza vijana hao kujiajiri na kuajiri wengine ili kupunguza umaskini wa kipato. Wizara yangu inakusudia hivi karibuni kuwapatia vijana hao mafunzo mengine juu ya kutengeneza sabuni, kuwafunza shughuli za upishi na ujasiri amali.

Aidha kwa kuwa Jimbo hilo la Kikwajuni iko *Saccos bank* wizara pia itatoa mafunzo ya ushirika kwa vijana ili wanufaike na huduma za benki hiyo, Mhe. Mahmoud madogo hayo?

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Haji Khalid wa Mtambile nadhani ndio anaingia sasa hivi alisema na bora nimalize hapa hapa; Mtambile kule hakuna kikundi hata kimoja kilichopata, nitakuja orodha vikundi vyake vinne vya Mtambile. Mheshimiwa tuchukue utaratibu wa kutembelea kwenye majimbo yetu kila baada ya muda tusikae sana, kwa sababu ukikaa sana yanafanyika mambo unakuwa huna habari sasa jitahidi Mheshimiwa kama tulivyo sote tuna hamu ya kuwasaidia watu wetu, vikundi vinne. Inawezekana pengine kikundi chako kimoja au viwili havikubahatika navyo *inshaallah* katika mpango unaokuja vitanufaika usiwe na wasiwasi.

Mhe. Hamza alisema ajira hizi zinatolewa kificho, Mhe. Spika, akasema kwake yeye hawajaenda. Hivi sasa Wizara chini ya kitengo cha soko la ajira Mhe. Hamza kimeandaa utaratibu wa kukusanya taarifa za ajira na kuwaarifu vijana mara zinapotokea, tunaweka pale na matangazo, mabodi yapo Mheshimiwa siku nyingi hujaja wizarani kwangu, kuna mabadiliko makubwa pale kuna kitengo tumekiweka maalum na mabao ya matangazo yapo pale ili vijana hawa na wanakuja wanajiorodhesha na ndio inasaidia, inapotokea nafasi za mahoteli nafasi nyengine tunawapeleka wanaohusika wanafanya kazi.

Na huyu bibi wa miaka 7 aliyehangaishwa kweli kesi hii tunaijua na *you are right,* lakini kwa nini bibi huyu usingeniletea mimi moja kwa moja kwa ajili ya kumuhudumia hizo shughuli zake. Lakini suala hili kama ulivyosema wewe mwenyewe hivyo vyama vya wafanyakazi ilikuwa badala ya kutetea wengine na wao wangejali kwamba maslahi yake huyo bibi. Mheshimiwa wizara yangu imeshalifanyia kazi suala hili na tayari tuko katika hatua nzuri na ninakuhakikishia kwamba hivi punde bibi huyu atakuja kukushukuru kwa kazi nzuri tuliyomfanyia tukijaaliwa.

Mheshimiwa kwenye sehemu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, kuhusu kuwapatia mtaji vijana, kuwapatia mafunzo jambo hili ni la msingi na wizara tutajitahidi kushirikiana na Waheshimiwa hawa ili kuendelea kutoa mafunzo

na kuwajengea vijana hawa. Mheshimiwa huyu mtaalam aliyekuja huyu Mr. Rajiv kama kaweza kufanya kazi nzuri Gando, kama kaweza kufanya kazi nzuri maeneo mengine Waheshimiwa hebu niaminini kwamba njooni pale wizarani mnambie tu nikupangieni ratiba kila Mheshimiwa Jimboni kwake mtaalam huyu nimpangie angalau siku tatu tatu aende. Mtakuja kukaa baada ya miaka miwili mtakuja kusema mabadiliko makubwa yaliyotokea katika maeneo yetu, na yuko kwa ajili yetu, huyu jamaa anajituma kweli kabadilisha mazingira kule Gando. Na bahati nzuri sijamchukua Makunduchi huyu nafasi bado naziacha wazi mkichelewa chelewa nitampeleka.

Lakini ninachosema kwamba tutumieni fursa hizi tulizokuwa nazo zitatusaidia sana, tukilalamika tu Waheshimiwa kwamba taaluma ndogo, taaluma ndogo, kama sisi ndio watoa taaluma ninakuombeni tushirikiane. Wengi wanakuja Waheshimiwa wawili wameniomba nifanye ziara.

Mhe. Mahmoud kanambia na wengine wamenambia, Mhe. Ali Salum kaniomba nawahakikishia kwamba nifanye ziara na *inshaallah* nitajitahidi nije jimboni huko nifanye ziara na nimeshasema maombi ya Waheshimiwa kama kumi na moja wameniomba kwamba nifanye ziara baada ya mwezi mtukufu wa Ramadhan. Lakini nawaomba wanipe muda kidogo kwa sababu *inshaallah* nitakuwa na harusi ya mtoto wangu ambapo baadae nitakuletea mualiko Mhe. Spika, nikimaliza shughuli tu basi nitaanza shughuli ya ziara vile vile. Nawaomba Waheshimiwa waje wahudhurie shughuli hiyo.

Kuhusu vijana wa kazi nje nje msije mkasema Waziri anatanguliza mialiko ili atulainishe hapa aa! Vijana hawa wanafanya kazi nzuri sana, angalia ukurasa wa 19 na 20 kwenye kitabu chako katika hotuba ya bajeti yangu utaona mambo ambayo wanafanya vijana hawa. Mafunzo waliyotoa kwa wenzao na wao wenyewe wameunda ushirika wao unajishughulisha na kutoa huduma mbali mbali. Aidha wengine wanajishughulisha na kilimo; kwa kuthamini juhudi zao Wizara imekuwa karibu nao na kuendeleza kuwapatia mafunzo na ushauri ili waweze kutekeleza shughuli zao vizuri.

Vyama vya Ushirika. Waheshimiwa wengi kweli wamechangia hapa Mhe. Hamza hapa ulipokuwa unachangia uliweka kwa jumla mambo lakini ulizungumza suala la meli za Iran na mambo ya bendera yale, sasa Mhe. Rashid Seif analingojea kwa hamu sana suala lako atakusaidia. Kwa sababu mimi si jukumu langu kweli, kwa sababu pamoja na masuala mengine lakini lilijitokeza suala la meli sijui ilikuwa na sababu gani lakini nadhani suala zima la utaratibu wa kusaidia kupata ajira kwa Wazanzibari katika maeneo hayo.

Lakini kwa vile naliunga mkono suala la ajira lakini suala la jawabu ya meli hiyo kwa nini sasa hivi zimeondoshwa au hazipeperushi bendera basi naomba tumngojee Mhe. Rashid Seif ana hamu kuja kujibu suala hilo nina hakika.

Kuhusu vyama; tunashukuru Mheshimiwa mashirikiano mazuri hadi mwezi Juni 2013 vyama 410 vimesajiliwa tunawaomba Waheshimiwa kuangalia taratibu za kisheria ndio pale niliposema kwamba taratibu za kisheria kuvisajili vyama hivyo ili tuweze kushirikiana vizuri.

Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile hebu tutizame vikundi vya Mtambile ambavyo vimenufaika halafu kama sivyo utakuja kupiga mguu unambie hivyo sivyo. *Mtawakal Cooperative* milioni moja, Sebushari milioni mbili, Kisima Mchele milioni mbili, Vijana wenye ulemavu Kengeja milioni mbili, milioni saba zimekuja Jimboni kwako Mheshimiwa. Sasa hatuwezi kukidhi mahitaji yote wakati mmoja na hivyo vilivyobakia *inshaallah* tutafanya utaratibu.

Kuhusu kuendeleza mashirikiano ya benki ya CRDB. Mhe. Hamza tumeendeleza mashirikiano hayo, jumla ya *Saccos* 6 kwa upande wa Pemba zimepata mtaji wa shilingi milioni 982 Pemba peke yake pamoja na huduma za kujengewa makaunta kwenye *saccos* zao. *Saccos* hizo Mheshimiwa ninazitaja ili zijulikane Mwambe *Saccos* wamepewa milioni 300 hawa, Jitambue *Saccos* milioni 450. Vijana *Saccos* 68 milioni. Tujuane *Saccos* 71 milioni, Tuishi kwa Usalama *saccos* 11 milioni.

Sasa milioni 972 CRDB peke yao wameweza kuzitoa. Mheshimiwa tuishukuru sana na tuipongeze benki ya CRDB wanafanya kazi kubwa kweli, mimi siwapigii debe lakini kwa kweli wana *deserve* na sote humu tuko huko Idara ya Mikopo. Mifuko ya AK na JK, takwimu zinaonesha kama marejesho tokea tulipoanza fedha za mfuko huo katika *column* ya mwisho kama nilivyoeleza pale nilipotoa ufafanuzi na pesa hizi za JK na AK Mhe. Waziri wa Fedha ananisikia, na akipenda anaweza kuja kutoa ufafanuzi wakati kama ikitokea hoja hiyo, kwamba sasa hivi maamuzi ya Serikali kupitia Wizara ya Fedha na benki kwamba sasa pesa zile za mfuko wa AK na JK zije moja kwa moja chini ya Mamlaka ya Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Pesa hizo tutazikusanya zikishakuja wakati wowote pamoja na mfuko wa kujitegemea, pamoja na mfuko huu ambao Mhe. Rais atauzindua kwenye mwezi wa Septemba uwezeshaji ambao tushakusanya pesa nyingi tu, ndipo pale lile wazo la kuanzisha benki ya ushirika tunaiita *community bank* tutapoianzisha sisi, na ninamuomba Mhe. Zainab kwa hili Wizara ile ambayo ina majukumu ya kuendeleza wanawake wana mpango wa kuanzisha benki ya wanawake. Lile wazo la kuwa na tawi wenzetu wa Tanzania Bara kulileta Zanzibar mimi sina tatizo nalo lakini kwa kuanzia acha tuanze na benki hii, *community bank;* ambayo itahusu wanawake, vijana na watu wote ili waweze

kufanya shughuli zao za kilimo, uvuvi na ufugaji kwa uzuri zaidi na kuwapatia mikopo hiyo haraka iwezekanavyo.

Nimefanya ziara kwenda India nimekutana na Waziri na tumezungumza suala hili la benki ya ushirika njia gani ambazo wanaweza kutusaidia, wameanzisha *community bank* vile vile hawakuziita benki za ushirika na zimeleta tija kubwa. Na nina hakika tukishawekeza pale kama bilioni tatu mpaka nne sisi serikali nina hakika kupitia Wizara yetu ya Fedha itachukua dhamana ya kuongeza pale tuwe angalau na bilioni nane mpaka kumi tuanze kutoa huduma hizo za benki, na sisi Wawakilishi tutafaidika katika maeneo yetu. Tuungeni mkono katika hizo na wakati Mhe. Rais atapozindua mfuko ule na ninawaambia Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi waalikwe na tutakualikeni na mambo yatakuwa mazuri siku hiyo tukijaaliwa, hatutotangaza kila Mwakilishi atapata kiasi gani lakini siku hiyo kila Mwakilishi atasema atachangia kiasi gani.

Mhe. Spika, nadhani kwenye mikopo hatuna upendeleo anayekuja, anayeomba kwa utaratibu tutampa, Mhe. Abdalla Juma kanipa kidogo na ndio kawaida yake hawa watu walio kimya kimya hawa masuala yao yanakuwa mazito kidogo. Anaambiwa mjasiri amali wa Darajani, sasa Waziri anayehusika na masuala ya Manispaa hayupo, wa Manispaa, sasa samahani yupo najua alikuwa Pemba, kwa hivyo Mhe. Spika, Waziri katika hotuba yake alieleza mambo mengi sijui kama hili aliulizwa, hakuulizwa tuje tumtafutie wakati muafaka tuje tumuulize lakini moja nalikubali kwamba kuna njia ya kuweza kuwakusanya wale ndugu zetu wale basi angalau tukaanza kuwapatia mafunzo na tukawatafutia maeneo muafaka ili waweze kufanya biashara yao vizuri zaidi.

Hilo tutaweza kushirikiana na wenzetu wa Manispaa ili kutoa taaluma zaidi kwa sababu wale wanafanya biashara sasa hivi hawana taaluma yoyote na wala hawajui taratibu za biashara zinavyokwenda, anayewahi ndio anafanya hivyo hivyo biashara anakwenda anauza. Sasa mimi sitaki kulizungumza suala hili la biashara za wajasiri amali wa Darajani lakini tunajua ni muhimu na inawezekana tukashirikiana na wenzetu tukaweza kuwapatia mafunzo hayo.

Mheshimiwa kuhusu mikopo hii na mifuko hii tumefanya mikutano mingi na PBZ na tumesaidiana na tuna utaratibu wa kukutana nao kila mwezi ili kuhakikisha kwamba wanatusaidia utaalamu.

Mhe. Hamza la CRDB ndio hilo nishalijibu sina haja ya kuendeleza lakini aidha Wilaya ya Micheweni, kuna Mheshimiwa mmoja aliyesema Wilaya ya Micheweni hakuna watu wanaotaka kusaidiwa? Wizara hii kwa kushirikiana

na CRDB tumepeleka milioni 175 kwenye ushirika wao. Sidhani kama kuna Wilaya Kipekee katika ushirika iliyopata pesa hizo kwa ujumla, tusilete dhana sana kwamba labda huku Pemba , huku Unguja hapana, ikitokezea si kwa nia mbaya kutokana na utaratibu ulivyo. Kuna Saccos ya Micheweni wamepata milioni 175 na *alhamdulillah* wajasiri amali mbali mbali na wananchi wa pale wanafaidika na SACCOS hii.

Mhe. Ali Salum nadhani alisema kwamba viwanda ndio *solution;* viwanda hivi Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tushirikiane nao waanzishe viwanda ajira zitapatikana.

Mhe. Rufai suala la masilabi umelizungumza nimeshalitolea ufafanuzi kwamba tushirikiane na Manispaa pesa zipo hatuna matatizo ni kukaa na watu wa Shirika la Umeme katika yale maeneo ambayo wanataka kujenga basi tuwape, lakini *speed* ya kutumia pesa hizi ni ndogo. Sisi kazi yetu kutoa pesa, Wizara ya Mifugo tumewataka watafute boti mbili, bahati mbaya sana za uvuvi mpaka dakika hii hatua hiyo haijachukuliwa wameshafikisha hatua nyengine lakini kwetu halijatufika.

Wizara ya Utalii kutembeza wageni hawa ambao ninasema sasa Wazanzibari tutawapatia mafunzo kuna pesa maalum, Waheshimiwa wengi wamezungumza suala la kuwapatia mafunzo pesa zipo nyingi tu tena ili tuweze kuwasaidia.

Kupitia Wizara ya Ustawi wa Jamii kilimo cha mboga mboga wanawake walipangiwa kupata shilingi milioni 100 na wamepatiwa milioni 66 kazi iliyobakia sasa hivi ni kufuatilia kujua kuwa pesa hizo zinatumika vizuri au vipi.

Wizara ya Habari walitengewa shilingi milioni moja, katika suala hilo hilo la kutembeza wageni na mambo mengine wametumia kumi na saba tu milioni. Sasa tutashirikiana ili kuhakikisha kwamba pesa hizo zinatumika na vijana karibu 152 wanajishughulisha na shughuli hizo Unguja na Pemba.

Wafugaji wadogo wadogo; Mheshimiwa mmoja kazungumza suala la uvuvi hapa lipo hapa Mhe. Amina suala la uvuvi tumelizungumza hapa kwenye kitabu na tumesema tutawaendeleza wafugaji wa kuku, mbuzi, ng'ombe na wengineo na serikali imetenga shilingi milioni 150 tumetoa milioni 85 tayari kuwaendeleza wavuvi, wakulima na wafugaji hao.

Kuna milioni 400 zilipangwa kwa ajili ya kununua boti hizi za kwenda bahari kubwa limechukua muda mrefu lakini pia boti iliyoletwa bei yake ni kubwa mno, wenzetu wa Wizara ya fedha wametushauri hatuwezi kununua boti

milioni 300 na wakati boti za milioni 20 za kwenda maji hayo hayo kwenda kuvua, tunaweza tukapata 10 badala ya 2 hizo. Kwa hivyo tunafanya mazungumzo na Wizara ya Fedha na Wizara husika ili kuhakikisha kwamba suala hilo tunalimaliza katika bajeti hii tukijaaliwa.

Mhe. Spika, nimejitahidi sasa naomba kwa sababu maalum nimsaidie ndugu yangu kidogo samahani kuna Waheshimiwa wengine wamenipa maandishi, lakini kwa vile muda ulikuwa ni mdogo nitajitahidi nitapopata nafasi Mheshimiwa na naona muda utaniruhusu kidogo nitakuja kutoa ufafanuzi kidogo kwa baadhi ya Waheshimiwa ambao wameleta kwa maandishi.

Mhe. Mshimba wakati anachangia hotuba ya Mhe. Zainab na hata hotuba ya Maalim Haroun ametumia neno la ubaguzi kidogo amesema kuna mhindi mmoja kafanya moja, mbili, tatu na mimi vile vile hapa katika hotuba yangu ukasema huyu wa *Zanzibar Petroleum* ukamtaja kwa kabila lake. Jamani nchi hii haina ubaguzi hivi ndivyo Mungu alivyotuumba hatuwezi kujibadilisha. Mhe. Mshimba wewe una marafiki wengi sana wa kihindi na mimi ninawajua. Sasa unaposema muhindi huyu anawadhalilisha watu ulipotaja mtu wa Kenya humtaja kama Mkikuyu, nani, ukataja Mkenya. Sasa na huyu ungesema mgeni huyu kutoka nchi za nje au kutoka India angalau ungeleta sura hiyo.

Sasa kuleta ukabila tukaanza kudharauliana hapa haileti tija, mimi nchi yangu hii haijanibagua miaka 40 ninaitumikia serikali hii, mimi katika maisha yangu keshokutwa tarehe 24 Julai, Mhe. Mshimba ninatimia miaka 60. Mwaka jana nilisoma bajeti tarehe 24 Julai siku niliyozaliwa mimi, sasa leo sijazaliwa bado niko siku mbili niko tumboni, lakini naweza kusema.

Mimi nchi hii haijamdharau mtu wa kabila lolote, nilifika hatua mimi mpaka kugombania Urais wa nchi hii na nikasema nisije nikahukumiwa kwa rangi yangu nihukumiwe kwa matendo yangu, hivi ndivyo Mungu alivyoniumba na sitoweza kujibadilisha. Sasa unaposema Dr. Shein awaondoe Mawaziri waliokuwa hawamsaidii, Wizara mbili tatu umesema Mawaziri hao waondolewe, Maalim Haroun huyu na Mheshimiwa mwengine huyo na mwengine wote wakiondoshwa nani atabakia Waziri? Lakini nani anatoa Uwaziri? Kwanza Mwenyezi Mungu ndiye anayetoa uwaziri, hakuna fundi, hakuna mganga, hakuna yoyote ambaye anaweza kutoa uwaziri, na alipoichangia bajeti yangu katika kipengele kile alisema kwa nguvu zake zote mawaziri hawa waliokuwa hawamsaidii mimi ninashukuru Mungu, nimepata heshima kubwa sana na cheti kilichotukuka kilichotoka UNESCO na medali nikapewa kutokana na utendaji wa kazi. Kuna cheti kimetoka Marekani cha kushukuru mchango wangu wakati nilipotoa katika sekta ya elimu. SUZA hivi karibuni katika *graduation* yao walinitunukia cheti kwa mchango mkubwa nilioutoa katika nchi hii katika suala la elimu. Kwa wananchi wa

Jimbo la Makunduchi wamenipigia kura huu mwaka wa 13 hawajanibagua, na *wallahi* niko kwenye saumu hii Mhe. Spika, wananchi wa Makunduchi hawakufurahia tamko lile, hawakufurahi kusema kwamba Rais awaondoe Mawaziri waliokuwa hawamsaidii akimaanisha wakati anachangia bajeti yangu ni mimi, kama wao wameniamini miaka 13 kwa sababu tu ya matatizo fulani fulani, mimi nikikosewa humwambia mtu yakisha yameniishia nasamehe, mimi Mhe. Spika, nakuheshimu sana.

Mhe, Spika, mimi namwambia Mhe. Mshimba, nina ukereketwa wa nchi hii kuliko wewe. Mimi nimejiunga na Afro Shirazi miaka mingi iliyopita, nimebakia mwanachama wa CCM mtiifu tena, Chama changu kimenichagua Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa tena kupitia Baraza hili Mheshimiwa na wewe nina hakika ulinipa kura yako vile vile, vipindi vitatu mfululizo, basi sifai tu kuwa kiongozi naambiwa niondoshwe? Atakayeniondosha ni Mwenyezi Mungu na Dkt. Shein anatujua Mawaziri wake na kuna sifa zinazochaguliwa Mawaziri, usifikirie tunachaguliwa tu, kuna mambo yanaangaliwa mengi. Sasa kama mimi nilikidhi mahitaji yale kwa kipindi hiki basi sawa na *inshaallah* itapofika wakati wako utakuja kufika wakati huo *inshaallah*.

Kuna mama mmoja Mhe. Spika, alisifia hapa uwezo wa Mawaziri wa Zanzibar wanavyofanya kazi kutoka Marekani, na wakaambiwa wakati ule Rais Karume na Dkt. Shein kwamba Serikali yako inafanya kazi vizuri, na Serikali ya Umoja wa Kitaifa hii imempa sifa kubwa, tujengeni *spirit* ya kupendana. Ikiwa Mwakilishi kila mmoja ataposimama akisema Waziri huyu hafai, Waziri huyu hafai, tusimsaidie kazi zile Rais, Rais ana njia nyingi za kutuona sisi, ana sehemu kubwa anatuona, tunayofanya yote haya, tunayofanya sisi na mnayoyazungumza nyinyi yote anayajua. Sasa Mhe. Mshimba, dhambi ya ukabila ikianza kutumika ukisema muhindi yule, yule hanyanyasi kwa sababu yeye ni muhindi ni tabia yake binafsi, ni khulka yake si kwa sababu ya uhindi wake.

Nasema tena Mhe.Spika, sikusema hili kwa sababu mimi nimezaliwa kama yeye aah! Mie muhindi lakini wa Makunduchi, lakini leo ukianza kuniita muhindi mimi kwa mas-hara Mhe. Spika, he! Muhindi wewe mbaya sana wewe, hata akinambia sawa wala sihamaki, lakini unapomtaja katika kikao kama hiki jamaa yule. Lakini nakuhakikishia Mheshimiwa tumemuandikia barua ya onyo na barua zake ninazo hapa na kopi nitakupatia si leo wala jana tunajua tabia yake na hatutokuwa tayari kwamba awanyanyase Wazanzibari pale, na kama anaendelea Mheshimiwa nakuomba uje ofisini kwangu, kwa sababu nina hakika mabalozi wako utawarejesha ofisini kwangu njoo, *wallahi* nakuahidi kwamba tutachukua hatua za kufaa, na kama kumuhamisha hata

siku ya pili ataondoka, lakini hatukubali awanyanyase Wazanzibari pale, awanyanyase wafanyakazi wetu.

Mhe. Spika, sisi tunafanya kazi kwa pamoja, Baraza hili tukianza kutumia ukabila, rangi na dini hatufiki mbali, si dhambi mimi kama nimezaliwa hivi, si dhambi kama mkristo amezaliwa mkristo kwamba yeye ni mkristo, si dhambi kwamba mtu amekuwa Muarabu amekuwa Mngazija si dhambi, tuepukane na maneno yale, hichi ni chombo kikubwa, nchi hizi zinazotusaidia watu hao. Huyo mtaalamu aliyekwenda Gando naye ni muhindi, sasa je tumhukumu kwa sababu huyu ana tabia nzuri, kama huyu ana tabia mbaya si kwa sababu ya uhindi wake ni kwa sababu ya tabia zake tu. Na Mhe. Mshimba, nakuhakikishia mimi *wallahi billahi* nitakuwa tayari nileteee ushahidi wake wa kutosha, tunafanya kazi, na sisi upande wa Kamisheni ile na tunahakikisha kwamba dawa yake iko jikoni.

Nadhani Mhe, Mshimba mimi hilo ninataka nikusaidie nikupe nasaha na ushauri wa bure, kwamba nakuomba sana turudi kwenye laini zetu za kuchangia katika kuleta maendeleo, tusifike katika hatua kama hizo nakuomba sana, ule mshahara ulinizuilia, nimekufahamisha haya kwa sababu ya kukupenda, ningekaa nalo rohoni ingelikuwa sikutendei haki. Na kwa sababu ulilisema hadharani ukamtaja yule mtu na mimi nataja hadharani ili lilieleweke suala hilo.

Mhe. Spika, kuna matatizo ya ujumla ambayo Waheshimiwa wameniletea kwa maandishi na kwa haraka haraka sijui kama nitawahi lakini Mhe. Ismail, ameeleza hoja ya wakala wa zamu, sasa huu ni mtihani kidogo. Mama huyu amechukua fedha za watoto wa kizanzibari wanyonge, na mama huyu namshukuru sana Mhe. Mshimba, amezungumza jambo moja zuri sana hapa, alisema amefanya haraka kukusanya fedha akazichukua fedha za wanyonge. Mheshimiwa nakushukuru sana kwa hilo na nakuomba tushirikiane mimi na wewe ili tusafishe majina kwa sababu jamii huko nje inaelewa vibaya, pesa hizi ndio zile ambazo tunazipigia kelele za wavuja jasho, wanyonge, masikini wa nchi hii wamechangishwa laki tatu tatu hawa, mamilioni ya fedha yamekusanywa, jamani huu si utendaji mzuri wa kazi.

Kwa hiyo Mhe. Ismail suala hili ni mtihani kidogo, *we need some time*, Mawakala sita hawa tunakwenda nao vizuri sasa hivi tunashukuru Mungu. Tumemfutia kwanza usajili wake kabisa tumefuta kwamba sasa hatoruhusiwa, lakini tatizo lenyewe hii barua imekwenda wapi, kwa sababu hatumuoni na tukimpigia simu hatumpati, sasa wale ambao wanamuelewa nawaomba watusaidie watuletee ili tushirikiane naye ili kuhakikisha suala hili tunalimaliza.

Mhe. Spika, nakubaliana na suala lile la Zantel. Kwa kiasi kikubwa tatizo lilokuwepo *Zantel* mwaka jana na mwaka huu limepunguka sana, bado tumebakia na matatizo, wamebadilisha *management* yao pale *administration* yao pale kaja mwengine inabidi sasa tuanze upya. Sasa mimi nikwambie tu kwamba haya yote haya pamoja na suala hili la usalama wake kwamba halikujitokeza huku na huku, ukiniachia na *inshallah I promise you* kwamba nitakuletea kwa maandishi taarifa zote hizo, kwa sababu muda wa kulieleza ulikuwa ni mdogo kwa sababu umeniletea *last minutes* na sikuweza kuchukua majumuisho haya haraka haraka, nimelikumbuka hili la zamu pamoja na hilo la usalama wa afya kazini, pamoja na Waheshimiwa wengine wote waliochangia nawashukuru sana.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuniachia muda wa kulizungumza suala hili kwa urefu na kwa makini, sina nia mbaya wala sikusudii kumtolea uvivu mtu yoyote hapa kwa nia mbaya, nilichofanya ni kwamba nimefanya kwa nia safi, roho safi na naomba wale Waheshimiwa wawili walionizuilia shilingi yangu wanirejeshee, ili wakiirejesha shilingi hiyo nitatekeleza hayo waliyoyataka niyafanye pamoja na kwenda kupambana na huyo mtu ambaye anawanyanyasa Wazanzibari, na wengine wengi ambao wanafanya mambo ambayo si ya kawaida ya kuzuia vikundi vya ushirika visisajiliwe.

Mhe. Spika,mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi, wananchi wa Jimbo la Makunduchi wanaiunga mkono hotuba hii na maelezo haya, lakini pia niwashukuru sana Watendaji wangu Mheshimiwa Katibu Mkuu wangu, Kamishna, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara, kwa kweli Mheshimiwa wanafanya kazi nzuri, ni miaka miwili na nusu tumefika hatua hii bado tunahitajia muda wa kufanya kazi na *inshaallah* hata ukimalizika mwisho wa mwaka huu basi nina hakika tutakuwa tumefika mahali pazuri na suala la umasikini sasa tutakuwa tunajadili kama ni historia, lakini tunahitajia mashirikiano ya pamoja.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa na kuafikiwa)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lilijadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

27 WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA USHIRIKA

Kifungu 0701	Idara ya Usalama na Afya Kazini	20,000,0000/=
Kifungu 0801	Kamisheni ya Kazi	800,000,000/=
Kifungu 1001	Idara ya Ushirika	10,000,000/=
Jumla ya Fungu		**830,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	424,308,000/=
Kifungu 0401		

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaomba tu kutoa maelezo tu kidogo. Alipokuwa Maalim anatoa ufafanuzi hapa na majibu yetu juu ya suala la hususan kikundi ambacho kimo ndani ya Jimbo langu na baadhi ya maeneo mengine alitoa maelezo kwamba pale katika Jimbo kuna watu 86 ambao wameonekanwa na wakapata zile ajira, lakini pia eneo la Muwambe kuna kima fulani ambacho kilikuwa kimepatikana na maeneo mengine. Nilitaka Mhe. Waziri, atusaidie tu wanapokuwa wanasaidia katika yale maeneo yetu aweze kuwashirikisha Wawakilishi kwa sababu wao ndio ambao wanakuja hapa kuhoji na kupata maelezo, sasa nikitaka Mhe. Waziri, atuthibitishie tu namna akavyowashirikisha katika mambo kama haya pasi na kukosekana Mawaziri katika sekta zao.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Wala Mheshimiwa si tatizo hilo, muhimu tukiwapelekea taarifa waje tu basi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi katika fungu lenyewe moja nilianzia nilisema kwa hapa nitamnyang'anya mshahara, lakini pamoja na majibu yake Mhe. Waziri, na mimi ninaomba Mhe. Mwenyekiti, kutoa muhutasari kidogo tu kwa mujibu wa taratibu.

Mhe. Mwenyekiti, sikuwa na nia mbaya ya kusema nilete ubaguzi hata kidogo, lakini kisemo cha Makunduchi na Kaskazini maisha yote inakuwa lugha zinatafautiana labda niseme hivyo. Nilichokusudia mimi kusema kuwa muhusika muhindi kutoka Kenya ambaye ni *supervisor* wa pale, na mwengine nikasema wa *United Petroleum* kutoka India wanawanyanyasa wananchi, labda kusema hiyo kunyanyasa wananchi ndio kosa, nakiri ni kosa sitokuwa na tatizo ikiwa ni hilo. Lakini ni kweli marafiki zangu wengi wahindi wala sisemi uongo, lakini panapo haki niseme isiwe kuwa mtu rafiki yangu tena anyanyase watu na mimi ninyamaze kimya na huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhan, na wewe mwenyewe umeona hapa tumeshinda kidogo na ukatupa kura sisi tulioshinda, ujuwe sisi wengine masharifu, nilichosema mimi kilikuwa na haki kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena nilichokisema mimi uhakikishe kile kilikuwa kina haki kwa wananchi, Wazanzibari kuwatetea haki yao, na leo imedhihirisha Mheshimiwa watu kidogo tu watatu tuliosema tumekataa hotuba hii na wewe ukatamka ukasema tumeshinda, ujue hii ni neema kwa Mwenyezi Mungu, na nilichosema na mimi sharifu! Lakini vile vile kwa kumalizia hapa

Mhe. Mwenyekiti: Ngoja niseme kwanza, unajua ulimi unapoteleza huomba radhi, kama nilivyoomba radhi mimi na wewe ukiomba radhi yamekwisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na ulimi umesema umeteleza sasa na mimi namalizia. Lakini Mheshimiwa nilichosema ni kweli kuwa watu hawa katika masheli ya mafuta haya wananyanyaswa kiasi kikubwa sana, na naomba sana Mheshimiwa wangu asifikirie kama niko katika kauli ya ubaguzi, nakubaliana na yeye kwamba ni mkereketwa na mimi nakubaliana na mtetezi wa wananchi, ukereketwa wangu niko katika utetezi wa wananchi, yeye mkereketwa kwenye Chama, sawa nakubaliana naye, lakini na mimi mkereketwa kupitia wananchi, siwezi kuona haki ya wananchi inakwenda vibaya nisiseme, hilo sitokubaliana nalo.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema sasa ni kwamba ili nimrudishie shilingi hapa kuna Kamati yake. Mhe. Waziri, alituambia kuwa watu ambao wako wengi sana waliofanya kazi, mimi nataka kumwambia Mhe. Waziri, kwamba bado kauli ile uambatane na kamati pamoja na mimi ukitaka si lazima ili tusafishe idadi ambayo aliyoitamka yeye hapa kwa wafanyakazi Wazanzibari kwenye Mahoteli, hii imenipa shaka kubwa sana inawezekana umetumiwa kwa kompyuta, kompyuta inaweza ikadanganya. Kwa hiyo naomba sana shilingi yangu kutaka kuirudisha kuwa nikusikie kauli yako kuwa Kamati hiyo husika ya Utalii unaikabidhi kazi hiyo ili kufanya *research* ili kupata idadi kamili, kwa sababu bado Wazanzibari si kweli kwa idadi uliyopewa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Nimefurahi kweli, imebakia senti moja tu labda kurejeshewa ile shilingi. Mhe. Mwenyekiti, hakuna matatizo, mimi nimesema niko tayari kushirikiana naye Mhe. Mshimba na kamati itafanya kazi hiyo kwa pamoja, tukimaliza shughuli zetu tutakwenda kufuatilia watendaji wangu na kuna maeneo mengine nakuhakikishia hayo ni matatizo hasa, nataka tufuatane mimi na wewe na hao Wawakilishi wengine wa Kamati sote tukafanye kazi ili kuhakikisha Wazanzibari wanapata haki zao, usiwe na mashaka ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na kauli yake lakini kama nilivyosema kuwa Mawaziri sitomtaja Waziri yoyote, nasema *inshaallah* Mwenyezi Mungu akujaalieni Mawaziri muwe na kauli kama hii ya leo iliyotamkwa hapa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Nasema hivyo kuwa nakubaliana na kauli ya Mhe. Waziri na naiondosha shilingi nangojea tuende pamoja, na hilo mimi sitomuacha asinifungie mlango tu ofisini kwake.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii Mhe. Waziri akanisaidia ufafanuzi wa ziada. Mhe. Mwenyekiti mimi sina matatizo kama nilivyosema mwanzo na bajeti hii ya Wizara, lakini kuna hoja ambayo niliizungumza kuhusu masuala ya zile meli ambazo zilizosajiliwa kwa jina la Zanzibar, na inaonesha sijui pengine labda masuala ya *ECO* au vipi kwamba sikungumzia masuala kwamba meli ambazo zinazopeperusha bendera na labda pengine nyengine zimeondoka au vipi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu zaidi ilikuwa katika masuala ya ajira, na ndio maana nilijaribu kumtaja Mhe. Rashid Seif, siku ile ambaye ni Waziri wa Miundombinu, kwa sababu najua Mhe. Mwenyekiti, huwa na utaratibu kabla ya kumuita Waziri muhusika huwa vile vile tuna Mawaziri wengine ambao huwa unawapa nafasi na wao kutoa ufafanuzi, mimi ningelitegemea zaidi lile suala kama Wizara ya Kazi angelishirikiana na Wizara ya Miundombinu ili tukapata kujua hasa katika zile meli ambazo zinazopata vibali kwa jina la Zanzibar.

Na niliuliza ni kweli kwamba kuna kifungu katika makubaliano ambacho kinachosema kwamba kila meli itachukua angalau vijana watano wa Zanzibar? Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Waziri wa Miundombinu hakujibu, na mimi kulisubiri suala hili siku ya Wizara ya Miundombinu, mimi Wizara ya Miundombinu nina buti kama nane na sijui kama utakuja kunipa hizo zote.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ndio maana haya mambo mengine tunapunguza punguza kabisa ili tuje tupate nafasi kuzuia yale mafungu ambayo yenye

nyama zaidi. Hii tulikuwa tunataka kujua kwamba je katika hii mikataba hizi meli zinazosajiliwa je kuna kifungu ambacho kinachotoa haki kwa Wazanzibari kuajiriwa katika zile meli? Na kama kuna kifungu hicho ziko nafasi ngapi? Lakini sasa Mhe. Waziri wa Miundombinu hakutoa ufafanuzi na Mhe. Waziri wa Kazi na yeye inaonesha watendaji wake walihisi kwamba haliko katika mikononi mwao. Kwa kuwa kuna suala la ajira basi bado Mhe. Waziri wa Kazi hili suala liko chini ya mikono yake naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hili suala linahitajia mashirikiano, na Wizara hiyo ya Miundombinu bado, lakini suala la ajira mimi nakubaliana naye Mheshimiwa kwamba kuna haja, kwa sababu hizi meli zinapokuja hapa zinasaidia sana kuwapatia ajira ndugu zetu na tuvute subira Mhe. Hamza, meli ya Serikali inakuja na sio ndogo na hii nina hakika itachukua vijana wengi sana kufanya kazi kwa kuwapatia ajira.

Lakini pamoja na hayo yote mimi nitashirikiana sana na Wizara ya Miundombinu ili kuona na kuhakikisha kwamba meli hizi ambazo zinapeperusha bendera isije ikageuka yule jamaa badala ya kusema kupeperusha akasema bendera inapepesuka, sasa hizo meli zinazopeperusha bendera basi tuhakikishe kwamba vijana hawa tunawapatia ajira katika meli zile na wanafanya kazi.

Palikuwa panahitajika pafanyike kazi ya ziada kwa sababu hili suala halipo moja kwa moja kwangu, na kuna taratibu za kisheria ambazo itabidi tuzitekeleze na zifuatwe, mimi sina mamlaka hayo ya moja kwa moja kuingilia katika ajira ambazo zinahusika katika mambo ya bandarini pale, itabidi lazima tushirikiane na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kujua maeneo gani ambayo tunaweza kusaidiana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana Serikali yetu iwe inatusaidia sana, unajua tunapoteza muda mwingi sana kuhangaika kutafuta taarifa, taarifa kama hii wakati hizi meli zinasajiliwa Zanzibar kwa jina la Zanzibar, sio kwamba lazima zisajiliwe hapa lakini tuna *agent* wetu ambaye anasajili hizi meli basi alau kuweza kupata taarifa tunasubiri mpaka ije ile Wizara yenyewe husika, ni sawa lakini mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba sana Mhe. Waziri wetu mpendwa Mhe. Mwalim Harouna kwamba hili suala tunaomba walifanyie kazi kwa ziada.

Mimi najua kwamba meli ya Serikali itakuja, lakini Mheshimiwa tunapotumia jina la Zanzibar ikiwa tunakosa fursa zozote za ajira ndani ya meli zile, na tuliambiwa kulikuwa kuna meli zaidi ya 80, ukichukulia watu watatu watatu tu nane mara tatu ishirini na nne watu karibu mia mbili na arubaini,

Wazanzibari wangapi hao wangelikuwa wameshaondoka. Sasa mimi nadhani hawa watu ambao wanatumia majina yetu, makampuni wanaotumia majina yetu wanafaidika na jina la Zanzibar, basi ni vizuri na sisi tukajenga hoja au kuangalia maslahi ya Wanzanzibari katika masuala haya ya ajira.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani nikubaliane na Mhe. Waziri, atawasiliana na Wizara ya Miundombinu, lakini vile vile suala hili nitaomba Mhe. Waziri asije akanisubiri kwenye buti, maana kama nilivyosema buti nina nyingi, ili Mhe. Waziri wa Miundombinu aje anisaidie ndani ya maelezo yake wakati atakapokuwa anakuja kutoa majumuisho hapo baadae. Naomba tuendelee

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti 118,083,000/=
Kifungu 0501

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niungane na wenzangu kumshukuru na kumpongeza Maalim wangu Maalim Haroun Ali Suleiman; Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbali mbali ambazo nilizozitoa ambapo mimi nilitoa kwa maandishi Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda kushindwa kuweza kuchangia kwa kuzungumza.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja ambazo nilimpelekea na akazungumza alipokuwa anafanya majumuisho ni suala ambalo mimi nilikuwa nikilisimamia takriban mwaka wa tatu huu suala la wafanyakazi wa *Zantel,* na katika majibu yake amelizungumza. Lakini pia amenisaidia hapa kwamba ameletewa na watendaji wake baadhi ya yafuatayo kwa ufupi naomba niyasome kwa sababu hayakuingia katika *hansard* pale, tunasema suala la *Zantel* lina wafanyakazi 107, fedha zinazodaiwa ni 1,595,000,000/= madai yao kufanyishwa kazi miaka mitatu bila ya kupewa mkataba wa maandishi, kupatiwa mkataba wa miezi sita bila ya kurudia na kutolipwa mafao na madai wakiwa kazini.

Mhe. Mwenyekiti, haya majibu ambayo nimeyaangalia, yanakiri kwamba Kitengo kinachosimamia migogoro kazini imelipokea suala hili tarehe 8/5/2012 huu ni zaidi ya mwaka sasa. Katika kitabu chake Mhe. Waziri, kasema kwamba wamejitahidi kufupisha muda na kuna baadhi ya mambo wameweza kumaliza ndani ya wiki tatu, hili Mhe. Mwenyekiti, kama ninavyosema limepokelewa katika kitengo hichi kwa mwaka mmoja na mimi nimelileta katika Baraza hili tangu 2011 mara ya mwanzo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba mimi katika hili Mhe. Waziri, na yeye anajua kwamba hata katika maelezo yangu sikumwambia kwamba ninataka

kumzuilia shilingi wala kukwamisha bajeti yake, lakini nataka tuone tunatenda kwa watu wetu. Suala hili limeshachukua muda mrefu, na inajengeka fikra kwamba uongozi wa *Zantel* tunauogopa, na pamoja kwamba wanalipa kodi kubwa hapa Zanzibar lakini na mambo mengine inawajibika na sheria za nchi hii na wanapaswa kuzilinda haki za watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kufungua mjadala upya na vielelezo niliwahi kumpa Mhe. Waziri, lakini ninataka kutoa mfano mdogo tu katika ile kunyanyaswa kwao, wale ambao walikuwa Mwalimu Haroun aliahidi kwamba atalifuatilia suala lao na kulinda ajira zao waliachishwa kazi baada ya kishindo chote kile chini ya shinikizo kubwa kwamba watalipwa haki zao, lakini zile haki zenyewe zilikuwa hazieleweki. Lakini mfano mdogo ninataka kumpa ni suala zima la mafao yao baada ya kuacha kazi.

Mhe. Mwenyekiti, walipoachishwa kazi walipewa barua hii inaonesha kwamba katika ZSSF fungu lao lililokuwepo ni 705,000/= lakini walipokwenda ZSSF wamekuta kuna 130,000/=

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kuna vitu ambavyo vinakosa maelezo mengi sana, ningemuomba suala hili Mhe. Waziri, anipe majibu hapa kwamba baada ya kuwa nimeeleza hapa kwa miaka miwili mfululizo sasa anatupa muda gani kwamba lile litamalizwa na watu hawa kupatiwa haki zao.

Mhe. Mwenyekiti linatia unyonge sana kwamba hawa ni Wazanzibari kama nilivyosema madai haya yako mengi sitaki kuchukua muda mrefu kuyasoma, lakini nilitaka kujua suala hili kwa ujumla wake Wizara yake imelipanga lini italimaliza. Kwa sababu imeshachukua miaka miwili tangu kulileta hapa Barazani halipati majibu.

Mhe. Mwenyekiti, na kama walivyosema hatua za kisheria wamechukua, wameandika katika kitengo chake cha utatuzi wa migogoro limekuwepo pale na taratibu zote zimefuatwa kwa nini linakwama, tunaiogopa *Zantel* ama vipi?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumsaidia Mhe. Ismail Jussa, kwanza Waziri mimi simuogopi mtu yeyote katika utendaji wa kazi, namheshimu tu na nazungumza naye kwa lugha ambayo tufahamiane. *Zantel* mimi siwaogopi hata kidogo, nimeshawaita zaidi ya mara tatu au nne, tatizo la *Zantel* leo unazungumza na *director* huyu baada ya miezi mitatu washamleta mwengine unaanza upya, tunakaa miezi mitatu tunataka kuli-*solve* hili tatizo wanamleta kiongozi mwengine.

Hivi juzi kaja mwengine mpya yule aliyeondoka tuliyezungumza naye yote yale hayupo. Kaja jamaa mmoja nishazungumza naye na hata hawa walioachishwa kazi Mheshimiwa wamepatiwa haki zao zote na walikuja jopo la jumuiya hii wanaoshughulikia wafanyakazi hawa ofisini kwangu, wakanambia Mhe. Waziri tunakushukuru matatizo yetu asilimia kubwa yamepungua bado kidogo tu, tunakuomba haya utumalizie. Nikasema kwa hatua tuliyofika sasa hivi wizara hatuwezi kuyasimamia sisi, Kitengo hiki cha *DHU (Dispute Handling Unit)* tumekianzisha na nashukuru Mwenyezi Mungu watu wamepata muamko wanakitumia sana.

Hata Mhe. Makame Mshimba alipokuja na tatizo lake la wafanyakazi wake watatu kwenye kitengo kile naye aliwasifia sana wafanyakazi hawa, vijana watatu walikuwa na matatizo yao yote yalitatuliwa na hata kwenye taarifa yake alishukuru sana kwamba kitengo kile kiwezeshwe, kizidishiwe mambo fulani fulani ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi, ndivyo utaratibu unavyokwenda. Lakini kitengo hiki kina uhaba wa wafanyakazi Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tunataka kila wilaya tuwapeleke angalau wawili lakini hatuna wataalamu, wale ni wataalamu wenye sifa za mambo ya sheria na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Sasa tumejitahidi kuchukua hatua hiyo, tumeshapeleka *DHU* ikitoka huko kama bado malalamiko yale yapo inakwenda kwenye Mahkama ya Kazi na sheria hizo zinawaruhusu, wale waliokuwa wanashtaki kwamba mambo yao hayajakaa sawa waende Mahkama ya Kazi. Kwa hivyo, sisi upande wetu tunapeleka ndani ya *DHU* tutafika wakati tutawashauri.

Sasa muda wa mahkama hatuwezi kuamua sisi Mhe. Mwenyekiti, ni mahkama yenyewe itakapoamua kulitatua tatizo hili, lakini sisi upande wetu tutalisukuma zaidi ili kuhakikisha kwamba jambo hili linamalizika haraka iwezekanavyo. Nikitoa muda hapa ni *commitment* nitashindwa, lakini namuahidi mwanafunzi wangu kwamba nitajitahidi suala hili kwa kushirikiana na *DHU*, kwa kushirikiana na Mahkama ya Kazi na Mwanasheria Mkuu atatusaidia njia gani tutumie ili haki zao wananchi hawa wapate kama ilivyokuwa kawaida.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo. Mhe Mwenyekiti mimi naelewa nia njema aliyonayo Mhe. Waziri, lakini hoja kwamba uongozi wa *Zantel* unabadilika kila siku mimi nashindwa kuikubali kwa sababu moja tu Mhe. Mwenyekiti. Ofisi ipo na taasisi inaendelea anayebadilika ni mtu. Kwa kawaida hasa mambo kama haya ambayo yanaandikwa anayerithi ofisi anarithi na mafaili yake. Sasa tukiambiwa kwamba akija mtu mpya maana yake anataka kusema kuwa tunaanza upya, hatuanzi upya Mhe. Mwenyekiti. Sasa kama wao wanafanya namna hiyo

itakuwa wao wanatafuta visingizio vya kukiuka kufuata sheria za kazi na kulinda haki za watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, hawa watu walichukuliwa kwa ahadi kwamba wataajiriwa wakafanyishwa kazi bila ya mkataba. Nikalileta hapa wakamuahidi Mhe. Waziri nakumbuka nilikwenda mpaka ofisini kwake akanionesha mpaka *e-mail* alizokuwa kaandika nyengine siku ile ile niliyoileta ile hoja kutaka majibu wakaahidi kuifanyia kazi. Kazi waliyoifanyia kwamba watawalipa haki zao wakatafuta utaratibu wa kuwafukuza kazi, sasa washawafuta kazini sawa, haki zao wapewe basi, haki zao pia wanadhalilishwa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama ninavyosema tukienda na hoja hizi kwamba wao wanabadilisha *CO* kila siku kwa hivyo wanakuja na hoja mpya tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu. Kwa hivyo, mimi bado nataka nimuombe Mheshimiwa hili halijafika sehemu ya kwenda mahkamani huko alikokusema yeye ambako kuna taratibu zake, liko katika *DHU*, Kitengo cha Utatuzi wa Migogoro ambacho katika hotuba yake kakisifu kuwa kinatumia muda mfupi wa kumaliza migogoro. Hii tangu imepokelewa Mhe. Spika, Mei mwaka jana tayari ni mwaka mmoja na miezi miwili (miezi 14). Sasa nasema kama hakutajengeka dhana hapa kwamba hawa tunawaachia wafanye wanavyotaka, na yako mengi ya *Zantel* mengine yanakuja katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tunaisubiri kwa hamu hapa.

Lakini ninachosema Mhe. Mwenyekiti, kwamba hili linalohusu haki za wafanyakazi kwa nini *Zantel* inatufanyia hivi? Kampuni ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa. Kwa hivyo, hizi hisa ni hisa za wananchi wa Zanzibar halafu iwafanyie hivyo Wazanzibari! Na haya Mhe. Mwenyekiti, yako hapa Zanzibar tu, huko walikohamishiwa Bara huyakuti mambo kama haya, wanawadhalilisha Wazanzibari tu. Sasa kwa nini kampuni ambayo inaendeshwa sehemu fulani na fedha za walipa kodi wa Zanzibar inawafanyia hivyo Wazanzibari. Naomba bado Mhe. Waziri namheshimu sana mwalimu wangu hili anipe ahadi litachukua muda gani kumaliza suala hili, akakae na uongozi wake wa *Zantel* walimalize suala hili Mhe. Mwenyekiti, naomba sana maelezo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, kuna *develop* nyengine hapa, naambiwa kwamba kutoka *DHU* sasa hivi ishaondoka pale ishakwenda Mahkama ya Kazi. Sasa nilisema taratibu Mhe. Mwanasheria Mkuu anisaidie, kesi ikishakuwa Mahkama ya Kazi kama Waziri ninayo mamlaka ya kutoa muda wa kumalizika suala hili? Au kwa sababu ni Mahkama ya Kazi na inashirikiana na Wizara ya Kazi kwa sababu *management* yake ni ya Mahkama Kuu mimi nashirikiana nayo. Zamani sheria ilikuwa inasema hata yule Mwenyekiti wa Mahkama ile ya

Kazi nilikuwa namteua mimi au napendekeza mimi kwa kushauriana na Jaji Mkuu, lakini sasa hivi Jaji Mkuu ndiye anayeteua moja kwa moja yule ambaye baadae Mhe. Rais anamteua.

Kwa hivyo, sasa atusaidie, mimi ningependa limalizike leo hili suala sitaki migogoro na nataka nikiondoka wizara ile sikuacha kesi huko nyuma za matatizo ili atakayekuja nimwachie aendelee vizuri. Kwa hivyo, naomba ushauri wa Mhe. Mwanasheria Mkuu anisaidie suala hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri alivyotangulia kueleza kwamba suala kama limeshafikishwa mbele ya Mahkama ya Kazi kwa utataribu wa sasa hivi kwa mujibu wa sheria Mahkama ya Kazi ni Divisheni ya Mahkama Kuu. Kwa hivyo, sawa sawa na suala lile kuwa liko mbele ya Mahkama Kuu. Hivyo, utaratibu wake ni wazi kwamba Mhe. Waziri hawezi kuliingilia, lakini kama zilivyo taratibu za kiutawala anaweza akauliza liko wapi na pale ambapo panahitajika *intervention* ya kiutawala labda Mhe. Jaji Mkuu kushirikiana na Mhe. Waziri kuweza kusaidia suala hilo likatekelezwa kwa haraka kwa yale mambo ambayo yanahusiana na masuala ya kiutawala.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sitaki nipoteze muda wa Kamati yako hii ya Matumizi. Mimi kwa taarifa ambazo ninazo kutokana na hawa vijana na wakili wao anayewawakilisha ni kwamba bado kesi haijafunguliwa, lakini nitafuatilia sitaki kukaa hapa nikavutana. Ninachojua walitoa *note* ambapo barua ninayo hapa ya tarehe 13 Februari, 2013 ambayo ilipokelewa mpaka na uongozi wa wizara, kuna saini hapa ambayo ilikuwa inatoa *note* kuwa wasipolipwa haki zao itachukuliwa hii kama ni *note* kwamba watafungua kesi katika Mahkama Kuu. Kwa hivyo, hilo wasiwasi sina.

Lakini katika hii barua Mheshimiwa moja ambalo linatuhumiwa ni kwamba Kamisheni ya Kazi imekuwa ikishirikiana na Uongozi wa *Zantel* kuweza kuwafanyia khiyana wafanyakazi hawa kuwafanya wakasaini makubaliano katika lugha ambayo walikuwa hawakuifahamu, matokeo yake wakafika katika tatizo hili ambalo wamelipata. Ile baada ya hatua ya mwanzo ya kwamba badala ya kuajiriwa wakasainishwa barua kwamba wamekubali wenyewe kuacha kazi watalipwa ile haki na malalamiko kama hayo yako mengi sana Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kuyaleta hapa mwaka jana.

Kwa hivyo, nasaema nitalifuatilia, lakini kama itakuwa imefunguliwa kesi katika Mahkama ya Kazi na mimi naheshimu najua utaratibu upo wala nisingeileta hapa kama najua hivyo. Kwa sababu najua likifika hapo halipaswi kujadiliwa, lakini kama litakuwa bado ajue kwamba Mhe. Waziri nitambana

yeye bado, tutapitisha bajeti lakini nitakwenda kumfuata Wizarani. Kwa sababu kama wanavyosema Waswahili nimelichukua kwa muda mrefu na linanisikitisha sana, kwamba katika chombo kama hiki cha wananchi ifike miaka miwili bado suala hili halipatiwi ufumbuzi. Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nasema tuendelee ahsante.

Kifungu 0501 Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka kwanza nimpe pole sana Mhe. Waziri kwa sababu kwa kweli haya mambo ambayo tunampigia buti sio kwamba ni mambo ambayo moja kwa moja yanagusa Wizara yake. Kwa sababu ni mambo ambayo yako nje ya wizara yake, lakini kwa kuwa wizara yake inashughulikia masuala ya kazi ina maana vile vitengo vimo ndani ya ofisi yake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri asione kwamba ah, jitihada zote ninazozifanya bado nazuiliwa, hili ni jambo ambalo tunataka kwamba watendaji wake wajitahidi kuweza kuyasimamia haya matatizo ambayo wamebebeshwa majukumu, wayasimamie nje ya wizara yao.

Sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la yule mama ambaye ni sekretari katika Ofisi ya *ZATU* kule Pemba. Kwa bahati Mhe. Waziri alisema sikumpeleka ofisini kwa sababu alichelewa kuja, kaja tayari chungu kiko jikoni Waziri anasoma na yeye ndio akaja. Sasa unajua sisi wengine tumekuwa kama *ATM* hatukai na kitu, tukikipata kitu tunakikabidhi kwa Mhe. Waziri. Lakini nashukuru sana kwa jinsi anavyolishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba kitu kimoja, Mhe. Mwenyekiti, huyu mama ameshateseka kwa muda mrefu zaidi ya miaka mitano anafanya kazi halipwi mshahara, tena hiki chama kama nilivyosema sio chama cha serikali ni chama cha wenyewe cha kutetea haki za wafanyakazi wao wenyewe wanawatesa wafanyakazi wao. Sasa hoja yangu iko hapa, kwamba hivi sasa yuko katika huu mgogoro lakini bado wamemsimamisha kazi kwa sababu ya kudai haki zake.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri atumie kifungu chochote ambacho kimo ndani ya sheria yake cha kuweza kuvidhibiti hivi vyombo vyengine visinyanyase watu, wamrejeshe kazini ili baadae wafuatilie na hizo haki zake nyengine tangu hicho kipindi cha nyuma. Kwa sababu kama sasa hivi wamemsimamisha kazi anatoka Pemba anakuja Unguja kuja kufuatilia masuala ya haki zake, huo uwezo wa kuja kufuatilia haki zake kila siku ataupata wapi wakati yeye hana ajira na mtu mwenyewe ni mwanamke. Mimi nadhani Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto pale kama angelikuwa na misuli kidogo tu basi angelikwenda mwenyewe katika hiyo Ofisi ya *ZATU* kule akamtetea huyu

mwanamama, kwamba anachapa kazi ndani ya miaka mitano lakini anashindwa kupata haki zake, na anadai haki zake wanamsimamisha kazi. Mimi nafikiri huu ndio udhalilishaji kuliko hata ule udhalilishaji ambao tunausema.

Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri hili akalisimamia kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba huyu mama anaendelea na kazi,, na baadae awe anafuatilia hizo haki zake zilizobakia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri atakuwa na maelezo sawa, lakini huo ulikuwa ni ushauri wangu wa ziada.

Mhe. Mwenyekiti: Ushauri na ombi la Mheshimiwa ni kwamba ufuatilie Mhe. Waziri kwa karibu zaidi ili tatizo liondoke.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani mwanafunzi anaweza akampa ushauri mwalimu wake, kwa hivyo hakuna matatizo, tutalifanyia kazi hilo kwa kushirikiana naye. Lakini tutamuomba na Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa sababu masuala haya yanamhusu mwanamama huyu basi tulifuatilie kwa karibu zaidi. Nitaangalia vifungu vya sheria vinavyonipa mamlaka na kuchukua hatua zinazofaa. Tatizo hapa ndio sasa hivi wanajifanya vyama vya wafanyakazi na haviko moja kwa moja kwa sababu vile vinafanya kazi kwa njia ya Utatu (*Tripartism*), *ZATU*, *ZANEMA* na Wizara ya Kazi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa inabidi tutumie mamlaka yetu kwa njia nyengine, tushauriane tutafute vifungu ili baadae tutizame kipengele gani kinaweza kuwabana. Lakini nadhani tutalitatua tatizo hili *on good way*, tutazungumza na watu wa *ZATU* au wale wafanyakazi tujue suala hili tunalimaliza. Na kama wamemzuilia kazi kwa sababu hiyo tu, nalo pia tutawaambia kwamba huo si utaratibu na wao kama ndio wanadai haki za wafanyakazi hawawezi kuwa wao wakawa wa mwanzo kuvunja sheria hizi. Kwa hivyo, tutajitahidi kufanya hivyo, *Inshaallah*.

Kifungu 0501 Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,554,866,000/-
Kifungu 0502 Idara ya Mikopo	198,174,000/-
Kifungu 0601 Idara ya Ajira	120,498,000/-
Kifungu 0701 Idara ya Usalama na Afya Kazini	82,251,000/-
Kifungu 0801	

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, hapa nilisema sana katika idara hii na hapa nilitishia vile vile kuzuia kifungu hiki. Lakini kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri ya kunambia kuwa anashughulikia

mikataba hiyo ambapo kuna mikataba tayari ameshafanyia *translation* ya Kiswahili na Kiingereza, lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri nina ushahidi huu hapa una Kiingereza kitupu mkataba huu wa *Zanzibar Petroleum*, mwenyewe masikini ya Mungu hajui chochote ameshapigwa bao hapa kwa mujibu wa mkataba huu, ningekuwa na miwani bila ya kupoteza muda ningejaribu kuusoma wote Mhe. Mwenyekiti, lakini naogopa sana kuula muda wako.

Ninachotaka kumwambia Mhe. Waziri bado wasimamizi wake hawajasimamia ipasavyo hasa katika maidara mengi sana hasa *private sector*. Nina ushahidi huo pamoja na mingine ipo, lakini kwa kuwa amekubali mwenyewe kwa njia moja au nyengine kuwa yumo katika hatua za kufanya hivyo, basi naomba sana na hili naomba sana niwarudishie kamati yako ili iweze kusimamia hili. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli wanaonewa vibaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, asili ya kusema kesi moja hapa nikakisifu sana kitengo ulichokisema ambayo ni tajiri mmoja ambaye anafanya mambo ya *Zanzibar Flower* kule kwetu Kiwengwa, amefanya mikataba haitambulikani mbele wala nyuma na nashukuru sana kitengo chako hicho kuwa bado kimo katika *process* ya kutaka kumsaidia. Halikadhalika na hawa wameteua mkataba mwengine mbali ya *example* ya mkataba huu niliyokuonesha ambao huu ndio *complete*, lakini kuna mikataba mingine mtu anaachishwa kazi anaambiwa kwa mujibu wa kifungu cha mkataba lakini mkataba wenyewe hakuuona.

Mhe. Mwenyekiti, hili bado nasema hivi, kuwa namuomba Mhe. Waziri bado arejee tena kwa kamati yake imsaidie kazi na usimamizi nikiwemo na mimi. Kwa sababu ukweli Mhe. Waziri anadanganywa danganywa kusema ukweli ulivyo, anadanganywa hasa Mhe. Mwenyekiti, hilo ukweli tuseme, anadanganywa na watendaji wake hawamuambii ukweli. Mimi nina ushahidi wa kutosha kwa asilimia mia moja, naomba sana Mhe. Waziri akubaliane tena na kauli yangu anijibu hapa kuwa hii kazi itakwenda sambamba na kamati yake nikiwemo na mimi niliyeibua hoja hii Dr. Mshimba. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, hili hata halihitaji kamati, hilo tatizo alilonalo aniletee kesho nakuomba ruhusa hiyo saa tatu nikae naye Mhe. Makame Mshimba kule ofisini kwangu aniletee pamoja na huyo mwenye matatizo tulifanyie kazi mara moja limalizike hiyo hiyo kesho tukijaaliwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana nalo na naunga mkono kwa asilimia mia moja ahsante sana Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kwenye hotuba hii ya Waziri niliona kwenye muhtasari wa mapato kuna vyanzo vyake vya mapato ikiwa moja ni vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa Kigeni. Nilitaka kujua ni vibali vingapi vimetolewa kwa wafanyakazi hawa wa Kigeni.

Vile vile nilichangia kwenye Kitengo hiki cha Utoaji wa Elimu juu ya Sheria za Kazi. Kwa sababu elimu hii imetolewa kwa mjini tu, mbali Pemba sikuona kwamba imetolewa elimu hii, na kwa sababu wananchi ili wafahamu sheria za kazi ni vizuri Wizara iandae vipindi tofauti tofauti. Kwa hivyo, nataka kujua ni kwa nini kwanza elimu hii imetolewa kwa mjini tu mashamba hamna, wakati kuna mahoteli mengi tu. Vile vile vipindi vikawa ni kidogo kwa *ZBC* inavyotoa pamoja na *Bomba FM*. Kwa hivyo, nilikuwa nataka maelezo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, hili suala la idadi ya wafanyakazi nilitoa takwimu pale lakini labda ni ubinadamu tu, nadhani nilisema kama sikosei ni 431 ndio takwimu zenyewe. Lakini hili suala la pili sikumuelewa vizuri labda anisaidie kidogo kulieleza tena, anakusudia kwamba suala la mambo ya Kamisheni ya Kazi sheria za kazi hazieleweki. Kama ni suala zima la kutoa taaluma hilo nakubaliana naye, *unless* iwe kuna masuala mengine aliyokusudia anifahamishe.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mimi Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia ni kuhusu hii elimu, kwanza kuwa ni jambo la muhimu kupatikana ili kujulikana juu ya sheria za kazi. Sasa nimeona huku katika hotuba yake kuwa elimu hii imetolewa kwa baadhi ya mahoteli ambayo ni *Coconut Hotel*, Skuli ya *Al-Hidaayah* Chukwani, lakini bado kuna maeneo mengi ambayo yanahitaji kwenda kupewa elimu. Sasa nilikuwa nataka kujua ni kwa nini kwamba elimu hii imetolewa kwa mjini tu wakati mashamba kuna maeneo mengi zaidi ambayo yanahitaji pia kupewa elimu huko.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Nimemuelewa Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hapa tumeanza tu Mheshimiwa, juhudi hizi zinaendelea na *Inshaallah* tutajitahidi huko wilayani na mikoani kote tufike haraka iwezekanavyo ili wapate taaluma hii.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika orodha ya mambo ambayo nimeona Mhe. Waziri anipe maelezo ni suala hili la migogoro ya kazini ambayo ilikuwa katika Kamisheni ya Kazi. Sasa moja nashukuru katika majibu aliyonipa limegusiwa hili suala la mfanyakazi wa hoteli ambayo iko katika Jimbo langu, hoteli inayoitwa Two, Three, Six; Hurumzi Hotel, ambayo kuna wafanyakazi 38. Kwa mujibu wa maelezo yake anasema suala

hili limepokelewa katika kitengo cha *DHU*. Sasa nilikuwa naomba maelezo mafupi katika hili kwamba kasema madai ni mishahara ya miezi mitano kuanzia Februari hadi Juni 2013. Sasa unagundua ni kwamba wamiliki wa hoteli hii wana kesi tano Mahkama Kuu Vuga, ndio wawekezaji tulionao Mhe. Mwenyekiti hao katika nchi yetu, wana kesi tano Mahkama Kuu Vuga, kuwepo kwa kesi hizo kumeathiri uendeshaji wa hoteli wafanyakazi hawajafukuzwa wala kukatishwa mkataba, sasa hapo ndipo ninapotaka maelezo Mhe. Mwenyekiti, pameandikwa muajiri ametiliana mkataba wa uendeshaji hoteli ili kunusuru hali.

Sasa sikufahamu Mheshimiwa hii katika kunusuru hali inanusuru hali hii vipi. Kwa sababu hawa wananchi wanyonge hawajalipwa mishahara yao miezi mitano, na nina hakika na huu wa Julai tunaozungumza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka anisaidie Mhe Waziri kwamba kwa sababu suala liko kwao hizi kesi hazihusiani na suala hili, hili lao limepelekwa katika kitengo cha *DHU* sasa huu mkataba wa uendeshaji unaathiri vipi haki za watu hawa kuweza kulipwa? Naomba maelezo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo nimepeleka pamoja na hili ni suala la wafanyakazi wawili ambao ni Bwana Maneno Ibrahim Shaaban na Abdalla Said Khamis nilimtajia katika mchango wangu Mhe. Waziri. Hili katika maelezo aliyokuwa kanipa halikuguswa na hili limehusisha wizara yake. Kwa sababu katika barua zao nyingi walizoandika wafanyakazi hao wawili waliokuwa *Vera Club* ambao wameumia wakiwa kazini walipata ajali mpaka leo hakuna maelezo. Kuna barua hapa pamoja na barua ya Kamisheni ya Kazi kuuandikia uongozi wa hoteli kutaka suala hili limalizwe na wapewe haki zao, lakini mpaka leo hawakupewa haki zao. Sasa nilikuwa naomba nipatiwe maelezo katika haya mambo mawili ambayo yote niliyajumuisha, pamoja kama ni hoja moja juu ya suala la haki za wafanyakazi katika maeneo mbali mbali naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, hili la kwanza kama tulivyosema kwenye taarifa tuliyompelekea ni kwamba tulitaka kunusuru ile hali, na ndio maana yakatokezea yaliyotokezea ili ikiwezekana huyu atakayechukua jukumu hilo sasa atatue matatizo hayo. Lakini imani yangu kwamba kwa mashirikiano yetu ya karibu kabisa sisi na *management* ya hoteli hiyo tutafuatilia kuhakikisha kwamba haki zao wanazipata mara moja na lisicheleweshwe tena. Kwa sababu taarifa nilizokuwanazo kwamba mkataba waliokuwa nao wafanyakazi hao kwamba haki zao hizo lazima wapatiwe hakuna sababu ya kuzichelewesha. Imani yangu kwamba wafanyakazi hao watapatiwa haki zao na kama mpaka sasa hivi hawajapatiwa namuomba Mheshimiwa basi aniletee

taarifa, kwa sababu taarifa nilizonazo haki zao hizo washapatiwa kama bado basi aniletee.

Kuhusu suala la *Vera Club* Ndugu Maneno Ibrahim ametibiwa kwa gharama za *management* ya hoteli na ametibiwa Muhimbili. Aidha, muajiri Ndugu Abdalla hajaripoti hoteli mpaka leo na hilo suala limekaribia kumalizika sijui kwa nini. Sasa Mheshimiwa atusaidie tu, kama kuna uwezekano tukampata huyu Ndugu Abdalla akaenda basi itakuwa hakuna matatizo tutaweza kumalizana naye. Kama keshaamua kwamba asiende kazini sasa *management* hawana tatizo kwa sababu itakuwa hawana jukumu, lakini tayari msamaha umeshapatikana na anatakiwa arejee kazini na yule aliyekuwa mgonjwa katibiwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hili la Hurumzi mimi mpaka nilipopokea ni kwamba bado hawajalipwa, lakini kama wamelipwa ndani ya kipindi hiki cha siku mbili tatu nitalifuatilia. Lakini kama hawajalipwa nikifuatilia nitawasiliana na Mhe. Waziri naomba anisimamie tu, kwa sababu inakaribia sikukuu *Inshaallah* kuwa mtu hajalipwa kwa miezi mitano mpaka sita hii inaweka hali ngumu sana, hata ukilipwa huo mshahara wako kwa mwezi na mshahara wenyewe ulivyo Mheshimiwa mkia wa mbuzi una mashaka yake, sikwambii kama hujalipwa miezi mitano mpaka sita. Hili nitalifuatilia.

Lakini na hawa wafanyakazi wawili nitamsaidia Mhe. Waziri kama alivyoomba, ingawa nina hakika zile nyaraka nilizonazo mimi na wao katika wizara yao wanazo. Hoja ya kwamba wametakiwa warudi kazini mmoja amerudi ni sawa, lakini katika huko kurudi ni kuwa suala la kulipwa haki zao ndilo ambalo lina matatizo.

Hili la Ndugu Abdalla ni kweli kwamba katibiwa katika Hospitali ya Muhimbili, lakini huyu matatizo yake makubwa na kama alivyosema Mhe. Waziri vizuri na watendaji wake wamem-*brief* vizuri katika hili, kwamba huyu ameathirika mpaka mguu Mhe. Mwenyekiti, ilibidi apelekwe India, na katika barua yake aliyoiandika hii ya mwisho ambayo ilipelekwa Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa sababu anahangaika kila pahala, keshaandika barua kwa Ofisi ya Makamu wa Pili, Wizara ya Katiba na Sheria, huko kwa Mhe. Waziri wa Kazi katika Kamisheni hii ya mwisho alipeleka tarehe 26 ana-*claim* kwamba bado kuna gharama nyingi ambazo alifanya kwa kutibiwa India ambazo Uongozi wa hoteli umekataa au umeshindwa kumhudumia.

Kwa hivyo, bado yako masuala lakini sasa ili kutokufanya hapa Baraza la Wawakilishi kuwa ndio pahala pa kuamua *(Melta Case)* mimi nitaomba hizi nizitoe *photocopy* halafu nimkabidhi Mhe. Waziri azifuatilie kesi zao zote

mbili hizi, za huyu Bwana Maneno Ibrahim Shaaban na Bwana Abdalla Said Khamis ambaye ukimuona Mheshimiwa hali yake inasikitisha sana, amepoteza mguu na si rahisi hata kufanya kazi tena Mheshimiwa, na pengine ndio maana hakuripoti kazini. Lakini kinachohitajika ni kwamba ukisoma mawasiliano inaonekana kwamba alitakiwa arudi kazini wakati anatibiwa na uongozi wa hoteli ulikuwa unayo taarifa. Kwa sababu katika barua zilizoandikwa humu zimo barua ambazo wameandikiwa uongozi wa hoteli, lakini ndio ile aliyosema Mhe. Makame Mshimba tuna tabia wawekezaji wengine wanaokuja hapa kwamba wanawafanya watu wa nchi hii kama vile si watu. Wanajua wa kuwatumia wakiwa wazima tu lakini inapokuja katika haki zao na matatizo hawawahudumii ipasavyo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hichi nitatoa *Photocopy* nimkabidhi Mhe. Waziri ili azifuatilie kesi zangu. Kwa sababu najua Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman ni muadilifu basi *inshaallah* atasimamia haki zao pamoja na haki zile za wafanyakazi wa Hurumzi Hoteli ambao nimekujawatetea. Lakini wengi orodha yao hawakai hata Mji Mkongwe. Lakini mimi ni Mwakilishi natetea wananchi wote wa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Kifungu 0801 Kamisheni ya Kazi 147,012,000/=
Kifungu 0901

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti wakati nilipokuwa nikichangia Mhe. Waziri alisahau hapa kunijibu ni suali dogo tu katika hii Idara ya Uendeshaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji wananchi Kiuchumi.

Tatu alisema kwamba ni kutanua soko la bidhaa la wajasiri amali wadogo wadogo. Nilitaka anifahamishe ni soko lipi hilo ambalo kwa mwaka huu wa fedha linataka litanuliwe ili wajasiri amali hawa wafaidike. Kwa sababu ninalolijua mimi kama moja liliopo pale Chake Chake kama ndio masoko yake ya *Sunday market* zinazotajwa ni pale *Barclays,* na ni eneo wapo pale wanajenga hivi wanafanya biashara zao halafu na kuondoka.

Sasa Mhe. Waziri nilitaka anifahamishe ni soko lipi alilokusudia kulipanua? Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, kweli aliuliza suali hilo na sikulijibu. Lakini sio kwa sababu sikutaka kulijibu jawabu ninayo.

Masoko yapo ya aina mbili hivi sasa tumeanzisha masoko haya ya Jumapili Unguja na Pemba. Lakini tumegundua tatizo letu kubwa tulokuwa nalo kwa

hawa wajasiri amali wetu na wafanyabiashara wetu bidhaa zao hazikidhi kiwango ambacho kinahitajika. Kwa hivyo, sasa hivi tunachofanya kupitia mtaalamu wetu huyu na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuengeza ubora wa bidhaa zile na hatimae kuziweka kwenye soko hasa kuanzia Jumapili. Lakini hata katika maeneo yao ambayo wanaweza wakafanya biashara zao kuweza huko huko kuwasaidia.

Tuna mpango sasa hivi pale Kisonge tulipoweka soko la Jumapili kwa kweli hapaoneshi kwamba kuna mvuto wa kibiashara. Tumo kwenye mazungumzo na tumeshaanza na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi tunakusudia kuzungumza na Waziri wa Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ ili eneo la Darajani pale penye eneo la *parking* ya magari hasa pale yalipokuwa yanakaa magari yetu ya zamani ya Makunduchi, angalau kwa Jumapili pale kama zilivyo nchi nyingi duniani maeneo kama yale basi hutumika kwa ajili ya soko la Jumapili.

Pemba tunashukuru soko lile linaenda vizuri ingawa halijaimarika sana. Kwa hivyo, suala hili hatuwezi kuliamua hili sisi mpaka tupate mashirikiano na wenzetu. Lakini kama tukikosa hapo basi tutasogea kwenye viwanja vile vya Malindi kuonana na wale wahusika ni kuona jinsi gani tunaweza kuwasaidia wafanyabiashara wetu.

La muhimu ni kuwapa taaluma za ufungaji bidhaa zao na tayari katika mipango yetu ya wizara suala hilo limo na nimelipa kipaumbele namna bidhaa zile ambazo tunapata ule ubora unaotakikana wa kimataifa.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo mazuri ya Mhe. Waziri naomba tuendelee.

Kifungu 0901	Idara ya Uratibu na Programu za Uwezesha Wananchi Kiuchumi	86,971,000/=
Kifungu 1001	Idara ya Ushirika	

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilizungumza Idara hii ya Ushirika katika urasimu wa kuwapa wanaushirika usajili wao.

Kwa kweli wananchi hao wamekosa fursa mbali mbali pale katika kupata misaada wakiwa hawakusajiliwa kwa mujibu wa sheria wanakuwa wanakosa haki zao za msingi, na haya waliyafanya kupitia ile kauli ya Mhe. Dr Ali Mohammed Shein kwamba wajikusanye pamoja ili huduma zao ziweze kuwafikia kwa urahisi zaidi.

Hivyo basi, maelezo ya Mhe. Waziri yalikuwa ni mazuri na niliyapenda. Lakini nipende kumuhakikishia tu kwamba kwa vikundi hivi vyote vimefuata utaratibu na vipo katika utaratibu kamili kabisa hawajapunguza hata sharti moja la usajili.

Hivyo basi, nimuombe kwanza Mhe. Waziri hili aliangalie kwa kina na kwa sababu ahadi aliyonipa yeye akipata tu majina baada ya wiki moja watakuwa tayari wamesajiliwa. Hivyo basi nashukuru na nasema tuendelee.

Kifungu 1001	Idara ya Ushirika	55,877,000
Jumla ya Fungu		**2,788,000,000**
Kifungu 0401	Idara ya Mpango	
	Sera na Utafiti	1,621,600,000/=
Kifungu 0801	Kamisheni ya Kazi	50,000,000
Jumla ya Fungu		**1,671,600,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha za Wizara yangu bila ya Mabadiliko yoyote, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza likubali makadirio hayo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia kukutana tena katika kikao hichi tukiwa wazima wa afya, pia nchi yetu ikiendelea kuwa na amani, utulivu na mshikamano.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu likae kama kamati ili lipokee, lijadili na hatimaye lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, kwa niaba ya viongozi na wafanyakazi wa Wizara yangu, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein, kwa uongozi wake wa busara, na juhudi zake kubwa anazoendelea kuchukua katika kuiongoza nchi kwa muelekeo wa kuiletea maendeleo ya ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii. Aidha, nawapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kushirikiana kwa pamoja na Mhe. Rais katika utendaji kazi za kila siku. Kwa pamoja nawatakia kila la kheri na baraka na kuwaombea Mwenyezi Mungu azidi kuwapa hekima, imani na busara waendelee kuiongoza nchi hii kwa kufuata misingi ya demokrasia na utawala bora – Amiin.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo napenda kumshukuru Mhe. Mlinde Mabrouk Juma; Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza lako tukufu na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kwa msaada na mashirikiano makubwa waliyoipa Wizara yangu. Napenda kuwahakikishia kwamba daima ushauri, mawazo na maelekezo yao tutayapokea na kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika**,** naomba pia uniruhusu niwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Gando kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza utumishi wangu wa ujumbe wa Baraza la Wawakilishi kwao, mfano mzuri wa mashirikiano hayo ni uamuzi wao wa kuanzisha mpango wa ujasiri amali wa Jimbo la Gando, mpango ambao umehamasisha uanzishwaji wa vikundi mbali mbali vya uzalishaji bidhaa ndani ya Jimbo la Gando. Ni matumaini yangu kwamba uzalishaji wa bidhaa hizo utakuwa ni wa kiwango kizuri ili kukimu soko kubwa lilioko katika sekta ya Utalii na hivyo kukuza kipato chetu na uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa niruhusu kutoa maelezo kuhusu muelekeo wa bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Katika maelezo hayo nitatoa vipaumbele vipya kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na uchambuzi wa malengo tuliyoahidi kutekeleza katika mwaka wa fedha 2012/2013 na utekelezaji wake. Kisha nitaeleza malengo ya mwaka wa fedha 2013/2014 ambayo Wizara imekusudia kuyatekeleza baada ya kupatiwa fedha tulizoomba.

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imeundwa kwa madhumuni ya kusimamia na kuratibu sekta kuu nne ambazo ni Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambapo ndani ya Wizara kuna Kamisheni mbili (2), Idara nne (4), Tume moja (1), Mashirika mawili (2) Vyuo viwili (2),

Mabaraza matatu (3), Bodi moja (1), Hoteli moja (1), Kampuni moja (1) na Ofisi kuu iliyoko Pemba. Taasisi hizo ni kama zifuatazo:-

i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
iii. Shirika la Utangazaji Zanziibar,
iv. Idara ya Habari Maelezo,
v. Shirika la Magazeti ya Serikali,
vi. Chuo cha Uandishi wa Habari,
vii. Tume ya Utangazaji,
viii. Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (ZMUX)
ix. Kamisheni ya Utalii,
x. Chuo cha Maendeleo ya Utalii,
xi. Hoteli ya Bwawani.
xii. Shirika la Utalii
xiii. Kamisheni ya Utamaduni na Michezo,
xiv. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale,
xv. Baraza la Kiswahili,
xvi. Baraza la Sanaa,
xvii. Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho,
xviii. Baraza la Taifa la Michezo,
xix. Kituo cha *EACROTANAL,*

Ofisi Kuu Pemba

Mhe, Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ilikadiria kupata shilingi 8,472,236,550/= kwa kazi za kawaida na shilingi 600,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Aidha Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,758,200,000/= zinazokwenda Mfuko wa Hazina na shilingi 1,742,800,000/= zinazokusanywa na kutumiwa na taasisi husika.

Mhe. Spika, jumla ya shilingi 6,770,071,872/= zilipatikana kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 80% na shilingi 508,086,215/= kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 85%**.** Aidha, Wizara ilikusanya shilingi 1,449,749,079/= sawa na asilimia 82% zilizoingia kwenye Mfuko wa Hazina na shilingi 1,632,118,555/= sawa na asilimia 94**%** ambazo zimekusanywa na kutumiwa na taasisi za Wizara, **(**Tafadhali angalia viambatanisho namba 1A, 1B, 1C, 1D na 2).

VIPAUMBELE VYA KISEKTA KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika**;** Wizara imeweza kujipangia mambo muhimu ya utekelezaji kisekta na kuwa kama vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2013/2014 vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo:-

SEKTA YA HABARI

Mhe. Spika; Mambo muhimu ambayo imejipangia katika sekta ya Habari kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni kama yafuatayo;

1. Kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za Habari na kwa wakati kwa njia ya magazeti pamoja na redio na Televisheni kupitia teknolija ya kisasa ya utangazaji wa digitali.

2. kutoa wahitimu wa kutosha wenye sifa (rasilimali watu) katika fani ya uandishi wa Habari na mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya soko la Habari nchini.

SEKTA UTAMADUNI

Mhe. Spika; Mambo muhimu ambayo imejipangia katika sekta ya Utamaduni kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni kama yafuatayo;

i. Kuchapisha na kusambaza majarida, kamusi na kufanya makongamano ya matumizi ya Kiswahili, kitaifa, kikanda na kimataifa.
ii. kukarabati na kuimarisha Makumbusho na sehemu za kihistoria kwa kiwango cha juu nchini.
iii. kutoa mafunzo kwa wadau wa kazi za filamu za sanaa ili kupata viwango bora zinazozingatia mila na silka za Wazanzibari.
iv. Kuwajengea uwezo wasanii kuweza kutoa kazi bora za sanaa mijini na vijijini na kuweza kupata soko kubwa ndani na nje ya Tanzania.

SEKTA YA UTALII

Mhe. Spika; Mambo muhimu ambayo imejipangia katika sekta ya Utalii mwaka wa fedha 2013/2014 ni kama yafuatayo;

1. Kuitangaza Zanzibar kuwa kituo bora cha utalii katika ukanda wa bahari ya hindi.
2. Kutoa mafunzo bora ya huduma za utalii na uongozi yanayoendana na soko la utalii kitaifa na kimataifa.
3. Kuimarisha huduma bora za hoteli nchini.

SEKTA YA MICHEZO

Mhe. Spika, Mambo muhimu ambayo imejipangia katika sekta ya Michezo mwaka wa fedha 2013/2014 ni kama yafuatayo;

i. **Kutoa mafunzo ya wataalamu wa michezo nchini.**
ii. **kuimarisha miundombinu ya michezo katika ngazi za Wilaya.**
iii. **kutayarisha mpango wa maendeleo ya michezo nchini.**
iv. **kuimarisha mashirikiano na taasisi za michezo za ndani na nje ya nchi.**

TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013 NA MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, Malengo tuliyotekeleza kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na tuliyopanga kutekeleza kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kiidara na taasisi zilizo chini ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Majukumu ya msingi ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi ni kusimamia shughuli zote za Utawala, Utumishi (Rasilimali watu), Maendeleo, wajibu na maslahi ya wafanyakazi wa Wizara na kusimamia udhibiti wa bajeti. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuongeza ufanisi wa uongozi na utawala katika taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa kusimamia na kutathmini utekelezaji kazi kwa watendaji wa Wizara.

ii. Kusimamia upatikanaji wa nafasi za mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wa Wizara ili kuwa na wafanyakazi watakaokuwa na ujuzi na uwezo katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

iii. Kuyafanyia matengenezo majengo ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuligeuza jengo la studio ya zamani iliyopo Rahaleo kuwa studio ya kisasa ya kurikodia muziki na filamu na kuufanyia matengenezo ukumbi wa juu wa Baraza la Wawakilishi la zamani ili kutumika kwa shughuli za mikutano za Wizara.

iv. Kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya ya ukimwi kwa wafanyakazi wa Wizara na taasisi zake juu ya athari na namna ya kuepusha maambukizi mapya ya ukimwi.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika**,** Idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo yake ya mwaka wa fedha 2012/13 kama ifuatavyo.

i. Idara imeweza kusimamia na kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya *internet, fax* na simu za ndani za ofisini pamoja na ulipaji gharama za maji, umeme, ununuzi wa mafuta na vilainishaji. Vile vile idara imeyafanyia matengenezo madogo madogo magari, kununua samani za ofisi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao.

ii. Idara imegharamia masomo wafanyakazi 12 wanawake (8)na wanaume (4) kati ya hao wafanyakazi watatu (3) ni wa ngazi ya Shahada ya Pili (Master), watatu (3) ni wa ngazi ya Shahada ya kwanza (Degree), na sita (6) ni ngazi ya Stashahada (Diploma)

lengo ni kuwaongezea ujuzi, maarifa na ubunifu ambao utapelekea kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. (Tafadhali angalia kiambatanisho namba 3).

iii. Idara imelifanyia matengenezo makubwa jengo la studio ya zamani iliyopo Rahaleo ili kuwatengenezea vijana mazingira mazuri ya kuendeleza sanaa zao, kujiajiri na kuweza kujipatia kipato. Aidha Idara imeweza kuufanyia ukarabati mkubwa Ukumbi wa juu wa Baraza la Wawakilishi la zamani ambao hivi sasa unatumika kwa mikutano ya waandishi wa habari na shughuli za mikutano mbali mbali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,111,070,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 979,834,420 /= sawa na asilimia 88**.**

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imejipangia kutekeleza malengo makuu matatu ambayo ni kujenga mazingira bora ya kazi yatakayowezesha Wizara kufanya kazi kwa ufanisi, kuwaongezea ujuzi na utaalamu watendaji kwa maendeleo ya Wizara na kuhakikisha kuwepo kwa mashirikiano ya uendeshaji na utawala ya Wizara. Katika kutekeleza malengo hayo Idara imepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 14, shahada ya pili fani ya Utawala wa Umma mmoja (1), Uchumi na Uongozi wa Fedha wawili (2), shahada ya kwanza fani ya Utawala wa Umma mmoja (1), Uhasibu wawili (2), Ugavi na Ununuzi mmoja (1) na Uongozi wa Biashara na Masoko mmoja (1) na Stashahada fani ya Utawala wa Umma mmoja (1), Utunzaji Kumbukumbu mmoja (1), Mawasiliano ya Habari na Uhasibu wawili (2), Mawasiliano ya Habari mmoja (1) na mmoja (1) Cheti.
ii. Kuwasomesha wafanyakazi 4 watakaohudhuria mafunzo ya nje ya muda mfupi katika nchi za China na India.
iii. Kuipatia ofisi kompyuta (*desk top*) mbili, (*laptop*) mbili na fotokopi moja.
iv. Kuipatia ofisi mafuta ya kuendeshea kazi za Wizara.

Mhe. Spika**,** ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, naomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 996,494,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kupanga, kutayarisha, kukagua, kuratibu na kutathmini mipango ya maendeleo ya Wizara, kupitia Sera, kufanya tafiti mbali mbali na kusimamia utekelezaji wake. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

i. Kuimarisha shughuli za mipango, sera na utafiti kwa kuwajengea uwezo watendaji wa vitengo vya Wizara na taasisi zake, kusimamia na kuratibu utafiti wa majina ya viumbe wa baharini na mazingira yao kwa ajili ya kuandika kamusi na kutafuta sanaa za jadi ambazo zinaanza kupotea Zanzibar.

ii. Kusimamia na kuandaa miradi ya maendeleo na kuratibu utekelezaji wa sera na matokeo ya tafiti kwa taasisi za Wizara.

iii. Kuwajengea uwezo na uelewa mzuri watendaji wa Wizara kuhusu masuala mtambuka ikiwemo jinsia na masuala ya watu wenye ulemavu na mazingira.

iv. Kuimarisha vitengo vya utafiti na takwimu ili kuweka utaratibu mzuri wa kupata taarifa na utunzaji wa takwimu kwa maendeleo ya Wizara.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

i. Idara imeweza kutayarisha na kuwasilisha mipango na taarifa za utekelezaji wa Wizara pamoja na kuratibu shughuli za sera na tafiti zinazoendeshwa na taasisi zilizomo ndani ya Wizara. Aidha Idara imeweza kuandaa mikutano ya robo mwaka kwa Maafisa Mipango na Watendaji Wakuu wa Taasisi kwa lengo la kujadili utendaji kazi.

ii. Idara imeweza kutayarisha Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa Wizara kwa mwaka 2013/14 hadi mwaka 2017/18 ili kuwa na mwelekeo mzuri wa utekelezaji wa shughuli za taasisi na Idara zilizomo ndani ya Wizara.

iii. Idara imeweza kufuatilia na kutathmini mipango na miradi iliyopo ndani ya Wizara na kwamba miradi hiyo imeweza kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Aidha Idara imeweza kuandaa warsha tatu kwa wadau wa sekta ya Habari, Utamaduni na Utalii kwa lengo la kujadili mipango, maendeleo na changamoto katika kuendeleza sekta hizi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 72,135,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 66,200,000/= sawa na asilimia 92.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO 2012/2013

Mhe. Spika; katika mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara imetekeleza Miradi mitatu (3) ifuatayo:-

Kampeni ya Uzinduzi wa mradi wa Dijital

Mhe. Spika; Lengo kuu la mradi huu ni kuwawezesha wananchi kuelewa mabadiliko ya kuhama kutoka mfumo wa zamani wa utangazaji wa habari wa analojia na kuingia mfumo wa kisasa wa dijitali kwa kuweza kutambua faida na athari zake.

Shughuli zilizopangwa na kutekelezwa

Mhe. Spika; Mradi uliandaa kampeni ya uhamasishaji wananchi kwa Unguja na Pemba. Katika kutekeleza lengo la mradi huo shughuli mbalimbali zilitekelezwa. Wizara ilifanya Uzinduzi wa kampeni ya digitali kwa kualika vikundi vya maigizo kikiwemo kikundi cha taarab, Ngoma ya kibati kwa ajili ya uhamasishaji. Pia kundi la wasanii maarufu nchini la kizazi kipya walipewa kazi ya kutengeneza wimbo wa digitali na kurushwa katika Redio na Televisheni. Pia iliweza kufanya warsha na semina mbili Unguja na Pemba, pamoja na utengenezaji wa slogans mbili na fulana 1,000 za uhamasishaji. Jumla ya programu kumi (10) zimetengenezwa kupitia TV na Redio.

Mradi huo ulipangiwa Shilingi 100,000,000/= na hadi kufikia Juni 2013 jumla ya shilingi 56,986,215 zimeingizwa katika mradi huu sawa na asilimia 57.

Ukarabati na Ujenzi wa sehemu za kihistoria na mambo ya kale.

Mhe. Spika**;** Lengo kuu la mradi huu ni kuwa na Makumbusho na sehemu za kihistoria endelevu nchini yenye hadhi ya kimataifa yatakayowezesha wananchi wengi na wageni kuweza kutembelea na kutumia sehemu hizo. Hatua mahsusi zilizopangwa na kuweza kutekelezwa ni pamoja na kuyapima na kuyapatia hati miliki maeneo ya kihistoria 8 Unguja na 14 Pemba. Kuweka mipaka maeneo ya kihistoria matano (5) Unguja na matano (5) Pemba. Kuyahifadhi kwa kuyafanyia matengenezo maeneo 7 Unguja na maeneo 7 Pemba. Kuyatangaza maeneo ya kihistoria kwa Kuweka mabango ya matangazo. Pia Wizara imekamilisha ukaguzi wa awali wa maeneo ya kihistoria ya Salhiya, bustani ya Salme, Nyumba ya Wareno Bambi, Pango la Kiwengwa, Kiwanda cha sukari Cheju na Pango la Bambi**.**

Gharama ya mradi huu ni shilingi 100,000,000/= ambazo hadi kufikia Juni 2013 jumla ya shilingi 51,100,000/= ziliingizwa sawa na asilimia 51.

Ujenzi wa Chuo Cha Maendeleo ya Utalii
Mhe. Spika; Lengo kuu la Mradi huu ni kuwa na miundombinu bora ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii nchini ili kufikia viwango vya juu vya utoaji wa mafunzo ya nadharia na vitendo ya huduma za hoteli na uongozi. Kazi zilizopangwa na kutekelezwa ni ujenzi wa ghorofa ya kwanza ambapo vyumba kumi na moja, zikiwemo ofisi kumi, ukumbi mmoja wa mkutano, ofisi ya pamoja na vyoo saba. Jengo hilo limeshawekwa miundombinu yote ya maji na umeme na kukamilika shughuli za uwezekaji. Hivi sasa jengo lipo katika hatua ya mwisho ya uwekaji milango, utiaji rangi pamoja na *tiles*.
Gharama ya mradi huu ni shilingi 400,000,000/= ambazo hadi kufikia Juni 2013 jumla ya shilingi 400,000,000/= ziliingizwa sawa na asilimia 100.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo makuu matatu nayo ni kusimamia Sera na mipango ya kisekta kwa maendeleo ya Wizara, Kuimarisha maendeleo ya Wizara kupitia matokeo sahihi ya tafiti na Kuimarika uwezo wa watendaji na utendaji kazi wa pamoja wa Kisekta kwa maendeleo ya Wizara. Katika kutekeleza malengo hayo Idara imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu mapitio ya sera za Utalii, Utamaduni na Michezo na kukamilisha Sera ya Mambo ya Kale.

ii. Kusimamia, kufuatilia na kutathmini Mipango, Sera na utekelezaji kazi za Wizara ndani na nje ya Zanzibar.
iii. Kufanya utafiti wa maeneo ya kihistoria, maendeleo ya sanaa na viumbe vya baharini.
iv. Kufanya mikutano na warsha za kutathmini na kupanga utekelezaji wa pamoja wa kisekta.
v. Kukamilisha matayarisho ya kuanzisha tovuti ya Wizara.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kufanikisha malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 kwa ufanisi, ninaiombea jumla ya shilingi 180,000,000/= kwa kazi za kawaida.

MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika; katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara inategemea kutekeleza miradi ifuatayo:-

Kutengeneza njia za kukimbilia za Uwanja wa Gombani
Mhe. Spika**;** Lengo la mradi ni kufanya Uwanja wa Gombani kuweza kukidhi viwango vya kimataifa. Hatua mahsusi za mradi zilizopangwa ni kusawazisha njia za kukimbilia pamoja na ununuzi wa lami utakaogharimu jumla ya shilingi 100,000,000/=.

Kuimarisha studio ya filamu na Muziki kwa kuipatia vifaa
Mhe. Spika; Vifaa vinavyotegemewa kununuliwa ni pamoja na *Sony xdcamex, Camera tripods, Camera cran, Track dolly, Lens fish eye, Digital video mixer, Digital audio mixer na Power amplifier*. Mradi huu unategemea kuingiziwa Jumla ya shilingi 80,000,000/=

Uhifadhi wa sehemu za kihistoria na mambo ya kale
Mhe. Spika; Lengo la mradi ni Kuwa na maeneo ya kihistoria yalio endelevu kwa maendeleo ya Utamaduni na Utalii.

Hatua mahsusi ni kuweza kuyapima na kuweka mipaka maeneo ya uhifadhi na kuyapatia hati miliki Unguja na Pemba, Kutangaza na kuendeleza maeneno ya kihistoria, uhifadhi wa mambo ya kale na sehemu za kihistoria Unguja na Pemba, kukusanya, kusambaza na kuweka mabango ya maelezo katika maeneo ya kihistora, kushajiisha jamii na kutangaza sehemu za kihistoria Unguja na Pemba, Kuanzisha maeneo mapya ya kihistoria na makumbusho mapya Unguja na Pemba, Kuwepo kwa maeneo bora ya kihistoria na mambo ya kale. Mradi huu unategemea kuingiziwa Jumla ya shilingi 230,000,000/=.

Mradi wa ujenzi wa vituo vya kutoa taarifa za usalama.
Mhe. Spika; Lengo la mradi ni kutoa msaada wa taarifa za utalii na kusimamia masuala ya usalama yanayohusiana na utalii. Hatua mahsusi ya mradi ni kujenga kituo kimoja kwa awamu ya kwanza pamoja na kufanya ununuzi wa vifaa kwa kituo hicho. Gharama za mradi huo ni jumla ya shilingi 100,000,000/=.

OFISI KUU PEMBA:
Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara Kisiwani Pemba. Ofisi hii ni kiunganishi katika kuhakikisha majukumu, malengo na shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba zinatekelezwa kama ilivyokusudiwa. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Ofisi hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazofanywa na taasisi zilizo chini ya Ofisi Kuu Pemba.

ii. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi.

iii. Kuendeleza mpango wa taifa wa kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi na kuratibu shughuli mtambuka za Ofisi Kuu Pemba.

iv. Kufanya matengenezo madogo madogo ya Ofisi Kuu Pemba, nyumba ya ofisi iliyoko Madungu na uwanja wa Gombani.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika**,** Ofisi kuu imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

i. Imeweza kuimarisha majengo ya Ofisi kwa kuweka madirisha mapya ya *"Aluminium*" na kupaka rangi ya "*ant-fungus*" ili kujenga mazingira mazuri katika sehemu za kazi na kuufanyia uwanja wa Gomboni matengenezo madogo madogo kwenye maeneo yaliyoharibika.

ii. Imegharamia masomo kwa wafanyakazi (11) katika kukuza viwango vyao vya elimu kati ya hao (4) ni ngazi ya Cheti na (7) ngazi ya Stashahada. (Tafadhali rejea kiambatanisho namba 3).

iii. Imeweza kusimamia shughuli za Ofisi Kuu na kukagua sehemu za kihistoria katika vijiji vya Gando, Tumbe, Vumawimbi, Pujini, Jambangome pamoja na kupitia mahoteli ya kitalii Chokocho, Fundo lagon, Matango na Mbuyu Mkavu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Ofisi Kuu Pemba iliidhinishiwa jumla ya shilingi 645,660,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 440,194,080/= sawa na asilimia 68.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe.Spika**,** Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Ofisi hii imepanga kutekeleza malengo mawili nayo ni kuhakikisha kuwa taasisi za Wizara zinashirikiana na kutoa huduma bora kwa jamii kwa maendeleo ya Wizara Pemba pamoja na kujenga mazingira bora yatakayoiwezesha Ofisi kuu Pemba kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo Ofisi kuu imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu na kufanya tafiti kwa kuimarisha kumbusho la Mkamandume na Misikiti wa Chooko.
ii. Kufanya Mikutano na wadau wa ndani na nje ya Zanzibar kwa ajili ya kukuza sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
iii. Kutayarisha vipindi vya sherehe ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.
iv. Utengenezaji wa njia ya kukimbilia uwanja wa Gombani.
v. Kushirikiana na Ubalozi wa Japan nchini Tanzania na Jumuiya ya Mchezo wa Judo hapa Zanzibar, kujenga jengo la mchezo wa Judo katika eneo la Uwanja wa Gombani Pemba, ambapo karibu shilingi milioni 500 zinatarajiwa kutumika.

Mhe. Spika**,** ili Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari,Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, naomba kuidhinishiwa shilingi 628,234,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 80,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

SEKTA YA HABARI

Mhe. Spika, Sekta ya Habari imeundwa na taasisi tano, Shirika la Utangazaji Zanzibar, Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali, Tume ya Utangazaji, Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (*ZMUX*) na Chuo cha Uandishi wa Habari. Majukumu ya Msingi ya taasisi hizi ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha jamii, kuratibu uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi na kutoa taaluma kwa waandishi wa habari.

SHIRIKA LA UTANGAZAJI

Mhe. Spika**,** Majukumu ya msingi ya Shirika ni kutoa habari, kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Shirika la Utangazaji la Zanzibar katika kipindi cha miaka miwili limekuwa ndani ya mageuzi makubwa, na kwamba bado limo ndani ya hali ya mpito kuelekea mageuzi kamili. Miongoni mwa mageuzi hayo ni:

i. Kuunganisha Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar na Idara ya Televisheni Zanzibar kuwa Shirika la Utangazaji Zanzibar.

ii. Kuunganisha shughuli za uhandisi, fedha, utawala, uhariri na utangazaji

iii. Kuanza kurusha matangazo kwa muda wa saa 24

iv. Kuanza kurusha matangazo kwa mfumo mpya wa Dijitali

v. Kufanya mageuzi ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar kwa kufanya yafuatayo:-

    a. Kutunga sheria mpya ya Shirika la Utangazaji Zanzibar

    b. Kuunda Bodi mpya ya Shirika la Utangazaji Zanzibar na kufanyia mageuzi muundo wa Idara na Uongozi wa Shirika

    c. Kununua vifaa vipya vya studio na mitambo mingine muhimu

    d. Kuimarisha matangazo ya Dijitali ndani na nje

    e. Kuimarisha hali ya kifedha ya Shirika ili liweze kujiendesha lenyewe.

Kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Shirika hili lilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha shughuli za utendaji wa Shirika katika ngazi ya uendeshaji na utawala.
ii. Kukuza viwango vya ubora wa matangazo kwa wasikilizaji na watazamaji wa ndani na nje ya Zanzibar.
iii. Kuanza majaribio ya urushaji wa matangazo kwa kutumia teknolojia ya dijitali.
iv. Kuimarisha sehemu ya ufundi ya Shirika kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China, ambapo tutaanzisha kitengo cha ufundi wa transmita, mixer na vipoza hewa.
v. Kukamilisha ujenzi wa kituo cha matangazo ya masafa ya kati (*Medium waves*) Bungi.
vi. Kukamilisha maandalizi ya muundo wa Shirika ikiwa ni pamoja na kuweka rasimu ya sheria ya Shirika la Utangazaji.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, Shirika la Utangazaji limefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Shirika limeweza kusimamia shughuli za utekelezaji wa kila siku kwa kulipia umeme, laini za simu kwa ajili ya matangazo ya moja kwa moja, kununua mafuta, vipuri, *mixer*, vifaa vya kuandikia na kusomea pamoja na kusimamia uendeshaji wa majenereta na magari. Vile vile limewapatia wafanyakazi stahiki zao za likizo na malipo ya muda wa ziada kwa lengo la kuimarisha shughuli za uendeshaji.

ii. Katika kuongeza ubora wa vipindi vyake vya kila siku, Shirika limeweza kutengeneza na kutangaza vipindi tafauti vikiwemo vya kuutangaza utalii kwa wote, Dini, Siasa, Elimu na Afya ili kuvutia watazamaji wengi zaidi. Aidha Shirika kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China wameweza kutoa mafunzo na vifaa kama vile mashine ya *Mixer*, Air *condition* na shughuli nyengine za kiufundi.

iii. Kwa kuhakikisha kwamba tunaenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya dijitali Shirika limeanza majaribio ya urushaji wa matangazo ya dijitali baada ya kupata fedha kutoka Serikali kuu. Na sasa wananchi wanafaidika na huduma mpya za matangazo hayo.

Aidha, Shirika limehamisha kumbukumbu kutoka kwenye kanda za analojia na kuzipeleka kwenye *CD* na *DVD* ambapo zitatumika kwa mfumo wa dijitali. Aidha, kuhusu ujenzi wa mnara wa kurushia matangazo Bungi utekelezaji wake umekamilika.

iv. Shirika limefanikiwa kuanzisha kituo cha kurushia matangazo ya dijitali ambapo wananchi wanapata fursa ya kuona matangazo hayo na kufurahia huduma hiyo tokea mwishoni mwa mwezi wa Februari 2013. Pamoja na mafanikio hayo Baraza lako tukufu liliweza kupitisha sheria ya kuanzishwa Shirika la Utangazaji ambayo tayari imeanza kutumika.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Shirika la Utangazaji liliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,016,224,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 1,611,857,366/= sawa na asilimia 80. Shirika lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 280,700,000/= na kufanikiwa kupata shilingi 210,326,283/= sawa na asilimia 75.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Shirika la Utangazaji limepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kutayarisha vipindi vyenye kuvutia wasikilizaji na watazamaji wa ndani na nje ya Zanzibar pamoja na kujenga mazingira bora ya kazi ili kuliwezesha Shirika kutoa huduma bora na zenye ufanisi. Katika kutekeleza malengo hayo Shirika limejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuweka vifaa vipya vya studio Unguja na Pemba.
ii. Kuandaa na kurusha hewani vipindi maalumu 52 katika maeneo makuu manne: Maendeleo ya Zanzibar katika kipindi cha 50 baada ya Mapinduzi ya 1964, Kupinga unyanyasaji wa kijinsia, Utalii kwa wote na Juhudi zinazochukuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mfumo wa umoja wa kitaifa katika kuleta maendeleo.
iii. Kununua gari moja ya kurushia matangazo ya moja kwa moja kutoka nje ya studio hasa katika sherehe na maadhimisho ya kitaifa.
iv. Kukamilisha utaratibu wa vipindi vya redio kupitia kwa msambazaji wa maudhui (*MUX*).
v. Kuwasomesha watayarishaji wa vipindi wanne katika ngazi ya shahada ya pili fani ya "*Program Production*".
vi. Kuanzisha mitandao minne ya kijamii (*facebook, twitter, blog* na tovuti) ya kupokelea taarifa na mawasiliano ya simu.
vii. Kufanya mageuzi ya muundo wa Shirika.

Mhe. Spika, ili Shirika la Utangazaji liweze kutekeleza malengo yake yaliyojipangia katika mwaka wa fedha 2013/2014, naliombea liidhinishiwe jumla ya shilingi 2,100,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kukusanya shilingi 280,000,000/=.

IDARA YA HABARI MAELEZO

Mhe. Spika, Majukumu ya msingi ya Idara ya Habari Maelezo ni kutoa elimu za maendeleo mijini na vijijini kwa kutumia gari la sinema, kuimarisha uhusiano mzuri kati ya Serikali na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi, kutayarisha na kutoa vielelezo katika mfumo wa picha, sinema na majarida kuhusu shughuli za Serikali na kusimamia Sheria ya habari Zanzibar.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuendelea kuwasomesha wafanyakazi, ununuzi wa vifaa vya kazi za ofisi, samani na kutengeneza vipindi vya maendeleo na utalii kwa wote.
ii. Kuweka tovuti ya Idara.
iii. Kuifanyia Marekebisho Sheria No. 5 ya Usajili wa Magazeti na vijarida ya mwaka 1988.
iv. Kuweka mbao za matangazo mpya. (*display boards)*

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Idara imeweza kuinua viwango vya elimu vya wafanyakazi wake kwa kuwapeleka masomoni wafanyakazi wanne (4) ngazi ya Diploma na mmoja Cheti, pia imewagharamia wafanyakazi watatu (3) kwenda masomoni nje ya nchi, (Tafadhali rejea kiambatanisho namba 3). Vile vile Idara imewapatia wafanyakazi wake stahiki zao za likizo.
ii. Idara pia imegharamia upatikanaji wa vipaza sauti seti moja, vifaa vya ofisini, mafuta na viti 6 vya ukumbi wa mkutano pamoja na kulipia umeme. Aidha, Idara imeweza kuchapisha "*posters*" la Baraza la Mapinduzi, picha za Rais Kikwete, kadi za waandishi wa habari (*Press Card*), albam za ziara za Naibu Waziri Mkuu wa China pamoja na kusafisha picha za sherehe za miaka 49 ya Mapinduzi ya Zanzibar.
iii. Katika kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia Idara imesimamia upatikanaji wa tovuti (*website*) kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wakati. Pia imetengeneza picha za kuweka kwenye mabango (*display boards*) kwa lengo la kutoa taarifa kwa picha na kutangaza matukio ya maendeleo kwa jamii. Aidha, idara imetafsiri Sheria Na. 5 ya Usajili wa Magazeti na Vijarida ya mwaka 1988 kwa lugha ya Kiswahili na mchakato wa kuifanyia mabadiliko unaendelea.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 267,500,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 206,369,476/= sawa na asilimia 77. Idara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 15,500,000/= na kufanikiwa kupata shilingi 15,037,500/= sawa na asilimia 97.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Habari Maelezo imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kuhakikisha wananchi wanapata taarifa muhimu kupitia njia za habari na mawasiliano na kuandaa mazingira bora ya kazi yatakayopelekea Idara kufanya kazi kwa ubora na ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Idara imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuandaa na kuratibu mikutano ya waandishi wa habari kuhusiana na matukio mbalimbali Unguja na Pemba.
ii. Kuonesha sinema vijiji 18 Unguja na 12 Pemba.
iii. Kuweka picha za matukio muhimu kwenye mabango (*Display Boards*).
iv. Kufanya machapisho na ununuzi wa picha za viongozi, Rais Kikwete – 300 na Marehemu Nyerere 54.
v. Kumalizia kuifanyia marekebisho ya sheria namba 5 ya Usajili wa Magazeti na Vijarida ya mwaka 1988.

Mhe. Spika, ili kukamilisha vyema malengo ya Idara ya Habari Maelezo katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, naomba kuidhinishwa jumla ya shilingi 313,660,000/= na kukusanya shilingi 18,000,000/=.

SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Shirika la Magazeti ya Serikali ni kusimamia uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Zanzibar, kuelimisha wananchi ili kukuza uelewa wao wa mambo, kutoa habari zenye kuhamasisha jamii na kushiriki kwenye harakati za maendeleo ya nchi. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Shirika la Magazeti ya Serikali lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha ubora wa magazeti ya Shirika kwa kuongeza idadi ya kurasa za magazeti ya Zanzibar Leo kutoka kurasa 16 hadi 20 pamoja na kuongeza idadi ya magazeti yanayochapishwa na Shirika la magazeti kutoka gazeti moja (1) la Zanzibar Leo na kuongeza jengine la Michezo na Utamaduni.
ii. Kukuza uwezo wa waandishi wa habari wa magazeti na wafanyakazi wa Shirika kwa kuwaendeleza kielimu ili kuwaongezea uwezo katika

utendaji wao wa kazi na kuongeza ubora wa makala, habari na matukio.

iii. Kuendelea kupanua wigo wa usambazaji wa magazeti yanayochapishwa na Shirika la Magazeti ya Serikali ndani ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, pamoja na kuliingiza gazeti katika tovuti (*website*) ya Shirika ili liweze kusomwa duniani kote.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, Shirika linapenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, gazeti limeweza kuwafikia wasomaji wengi zaidi kwa kuongeza maeneo ya usambazaji kama vile Mkokotoni, Nungwi, Uroa, Makunduchi, Jambiani kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba maeneo yaliongezeka ni Madenjani, Wete, Konde na Mkoani.

i. Katika kuongeza idadi ya magazeti yanayochapishwa, Shirika limeimarisha magazeti yake katika utoaji wa taarifa na upangaji wa habari zake. Uongezaji wa kurasa za magazeti ya Zanzibar Leo kutoka kurasa 16 hadi 20 unafanyika kila kunapoongezeka matangazo yanayochapishwa katika toleo husika. Aidha, kuanzia tarehe 1 Oktoba 2012 Shirika limeanza kuchapisha gazeti la wiki la habari za Michezo, Utamaduni na Utalii liitwalo "Zaspoti" na linaendelea kuchapishwa kila Jumatatu ambapo kwa sasa limeweza kuwavutia wasomaji wengi ndani ya Zanzibar na kwa baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara.

ii. Katika kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi mkubwa na kuongeza uzalishaji, Shirika limeweza kuwasomesha Wafanyakazi 10 katika ngazi tofauti ndani na nje ya nchi katika fani tofauti. Wafanyakazi hao wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ambapo wengine wanaendelea na masomo, (Tafadhali rejea kiambatanisho namba 3).

iii. Shirika limewapatia stahiki za likizo wafanyakazi wake. Pia Shirika limewapatia fidia ya ajali kazini wafanyakazi wake wawili. Aidha, Shirika limefanya matengenezo katika majengo iliyohamia ya *ZBC* Radio na limeshatayarisha waraka wa kutafuta wataalamu wa kutayarisha michoro (*design*), "*BoQ*" na "*Tender Document*" kwa hatua za ujenzi wa ofisi za Shirika huko Tunguu.

iv. Hatua ya utengenezaji tovuti 'website' ya Shirika zinaendelea kufuatia kutiwa saini ya Mou ya ushirikiano wa kitaaluma na kihabari baina ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na Shirika la Magazeti ya Serikali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Shirika liliidhinishiwa jumla ya shilingi 856,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013

imefanikiwa kupata shilingi 598,280,421/= sawa na asilimia 70. Shirika lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 500,000,000/= na kufanikiwa kupata shilingi 404,454,233 /= sawa na asilimia 81.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Shirika la Magazeti ya Serikali limepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kutoa magazeti yenye taarifa bora na kwa wakati muafaka ndani na nje ya Zanzibar na kuandaa mazingira mazuri yatakayoliwezesha Shirika la Magazeti ya Serikali kufanya kazi kwa ufanisi. Katika kutekeleza malengo hayo Shirika limejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuchapisha Magazeti ya kila Siku.
ii. Kuchapisha Magazeti ya kila wiki.
iii. Kusafirisha na kusambaza Magazeti ndani na nje ya Zanzibar
iv. Kufuatilia upatikanaji wa habari ndani na nje ya nchi pamoja na masoko mapya.
v. Kufanya malipo ya '*hosting'* ya tovuti (*Website*).

Mhe. Spika, ili Shirika la Magazeti ya Serikali liweze kutekeleza malengo hayo, naliombea kuidhinishiwa shilingi 856,000,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na kukusanya shilingi 500,000,000/=

TUME YA UTANGAZAJI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Tume ya Utangazaji ni kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi vinavyoanzishwa nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Tume ya Utangazaji ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu shughuli za Utangazaji kwa kutoa huduma bora za utangazaji nchini.
ii. Kuandaa na kuendesha kampeni ya kitaifa na kutoa elimu kwa umma juu ya mageuzi ya teknolojia ya utangazaji nchini ya kutoka katika mfumo wa Utangazaji wa Analojia kwenda mfumo wa Dijitali.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Tume ya Utangazaji imeweza kufanya mambo yafuatayo:

i. Kufuatilia vyombo vya utangazaji kwa kuzingatia sheria na kanuni za utangazaji kwa lengo la kuimarisha sekta ya utangazaji nchini.

ii. Tume imeweza kuendesha semina, warsha na kutoa mafunzo kwa umma kuhusu kuhama kutoka katika utangazaji wa analogi na kuingia kwenye dijitali. Aidha, imehamasisha jamii kupitia vipindi vya redio na televisheni pamoja na kufanya mikutano kwa wilaya zote za Pemba. Kwa upande wa Serikali, hatua zimechukuliwa za kuingia katika mfumo wa utangazaji wa dijitali kwa kujenga miundombinu na kuanza kurusha matangazo hayo.

iii. Tume imeweza kusimamia upatikanaji wa nafasi za masomo na mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi wake ambapo imelipia masomo wafanyakazi wawili ili kuwa na wafanyakazi watakaokuwa na ujuzi na uwezo katika utekelezaji wa kazi zao. Pia imetoa maelekezo na mafunzo mafupi kwa watangazaji wa vyombo vya utangazaji kuhusu maadili ya utangazaji, (Tafadhali rejea kiambatanisho namba 3).

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Tume iliidhinishiwa jumla ya shilingi 168,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 100,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 143,309,664/= sawa na asilimia 85 na shilingi 56,986,215/= kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 57. Tume imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 33,000,000/= na kufanikiwa kupata shilingi 45,142,000/= sawa na asilimia 137.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Tume ya Utangazaji imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kuingiza nchini teknolojia ya kisasa ya Utangazaji kulingana na viwango vya Afrika Mashariki na Kimataifa pamoja na kuweka mazingira bora ya kazi yatakayoiwezesha Tume kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Tume imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kufuatilia ugawaji wa mawimbi na udhibiti wa utendaji wa vyombo vya utangazaji nchini.

ii. Kuhudhuria kongamano la kitaifa la matumizi ya mfumo wa utangazaji wa dijitali.

iii. Kugharamia vikao vya bodi.

Mhe. Spika, ili kukamilisha vyema malengo iliyojipangia Tume ya Utangazaji katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, naomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 173,000,000/= kwa kazi za kawaida na kukusanya shilingi 44,000,000/=.

KAMPUNI YA UUNGANISHAJI MAUDHUI (ZMUX)

Mhe. Spika, ndani ya kipindi cha miezi minne, Zanzibar imeingia katika mabadiliko makubwa ya utangazaji wa dijitali. Mabadiliko haya yaliifanya Serikali yetu kuchukua maamuzi magumu tokea katika mchakato wa kupata kampuni ya kutuwekea miundombinu hadi katika ujenzi. Kuanzia Oktoba 6, 2012 Wizara iliingia katika pirikapirika hizo kwani tulilazimika kuwahi muda uliowekwa na Jumuiya ya Mawasiliano ya Afrika Mashariki (*EACO*) wa kuingia katika mfumo huo Desemba 31, 2012, lakini pia tulilazimika kufuata maagizo ya wajumbe wa Baraza lako tukufu wakati wa mjadala wa Bajeti yangu ya mwaka jana walioniagiza niharakishe kujenga miundombinu hiyo.

Mhe. Spika, tulipokuwa katika pirikapirika hizo kampuni kadhaa zilionesha nia ya
kushirikiana nasi katika kuendesha mfumo huo wa dijitali. Kampuni hizo zilitafautiana kibei, huduma ya vifaa ilivyotakiwa na kiteknolojia. Hivyo, katika kupata kampuni ya kuaminika, Serikali iliamua kuweka miongozo iliyopaswa kuzingatiwa. Miongoni mwa miongozo hiyo ni kutaka Miundombinu ya dijitali itayojengwa lazima iwe ni mali ya Serikali.

Aidha, iangalie uwezekano wa kutumia vifaa vilivyopo ambavyo vitafaa na bila ya kuvihamisha kwa lengo la kupunguza gharama. Katika kuhakikisha umadhubiti wa mitambo itakayonunuliwa, Serikali iliagiza vifaa vya studio vya *SONY, transmita* ziwe za *Rhodes & Schwaez* na miundombinu hiyo iwe ya teknolojia ya kisasa ya DVBT2 inayoruhusu kurusha matangazo ya "*High Definition"* yatakayotumika hapo baadae, kutoka matangazo ya "*Standard Definition*" ya hivi sasa.

Mhe. Spika, hatua ya ujenzi wa miundombinu ya Dijitali umegawika sehemu nne (4).

i. Kujenga miundombinu ya Dijitali – Hii ilipangwa kuanzia mwezi wa Oktoba 2012 hadi Januari 2013.
ii. Kuunganisha miundombinu ya Dijitali na vituo vya kupokea na kurusha matangazo – Hii ilipangwa kuanzia mwezi wa Februari 2013 hadi mwezi wa Juni 2013.
iii. Kukuza na kuimarisha Maudhui (*Content*) yanayorushwa kwa wateja na kuunda Taasisi ya usimamizi – Hii ilipangwa kuanzia mwezi wa Julai 2013 hadi Agosti 2013.
iv. Kuimarisha studio za matangazo za Karume House na Mkoroshoni Pemba. – Hii ilipangwa kuanzia mwezi wa Agosti 2013 hadi Oktoba 2013.

Mhe. Spika, Kampuni ya Agape ndio iliyopewa kazi ya ujenzi wa miundombinu ya Dijitali kwa thamani ya Dola za Kimarekani 3,921,625 kwa kutupa "*channel*" 36, na Kampuni ya Sony ndio tuliyokubaliana watujengee mitambo mipya ya studio ya Karume House na Mkoroshoni, kwa thamani ya Dola za Kimarekani 1,062,138.09 kazi ya ujenzi wa miundombinu hiyo imekamilika na ujenzi wa mitambo mipya ya studio bado haujaanza.

Mhe. Spika, kazi ya kuunganisha miundombinu ya Dijitali na vituo vya mawasiliano na kuimarisha mawimbi ya matangazo kwa wateja ni muhimu sana ili uwekezaji uliofanywa uwe na tija. Katika kukamilisha jukumu hili imelazimika kuchukuliwa hatua zifuatazo:

i. Kumpata mtaalamu mwenye ujuzi na maarifa ya kuendesha mitambo hiyo.
ii. Kupata ving'amuzi au *decoder* vitavyong'amua matangazo ya Dijitali kwenye televisheni za analojia.
iii. Kuimarisha maudhui (*content*) yatakayopitishwa kwenye mitambo hiyo.

Mhe. Spika, katika kukamilisha kazi hizo hapo juu, na kwa kuzingatia kwamba ndani ya Wizara yangu hakuna utaalamu wa kutosha wa kuendesha mitambo hiyo, Wizara ilikubaliana na mjenzi wa miundo mbinu hiyo mkataba wa uendeshaji wa mitambo ya Dijitali kwa muda wa miaka miwili. Katika kipindi hicho cha muda wa miaka miwili, Kampuni ya Agape itaendesha mitambo ya Dijitali, kulazimika kuleta ving'amuzi na kuuza kwa wateja. Aidha, katika kuimarisha maudhui yake, tumekubaliana kwamba itatoa mafunzo ya vitendo na nadharia kazini kwa vijana wa Kizanzibari ili baada ya muda wa miaka miwili ambapo mkataba wa uendeshaji utakuwa umemalizika, vijana wetu watakuwa wamejifunza vya kutosha kuweza kuendesha mitambo hiyo.

Mhe. Spika, katika kurahisisha mawasiliano baina ya Kampuni ya Agape na Serikali, na kwa sababu Shirika la Utangazaji haliwezi kuchanganya jukumu la utayarishaji vipindi na jukumu la msimamiaji mitambo ya Dijitali, tunalazimika kuunda taasisi maalumu inayojulikana kama *Zanzibar Multiplex Company* (*ZMUX*), Kampuni ambayo kwa sasa hisa zake zinamilikiwa na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo 60%, Shirika la Utangazaji (ZBC) 20% na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo 20%.

Mhe. Spika, kampuni hii iliyoanzishwa imekabidhiwa kazi tatu kubwa. Kwanza, kuendesha kwa ufanisi na kujitegemea kwa shughuli za kuunganisha maudhui kwa kutumia miundombinu ya dijitali. Pili, kuhakikisha ndani ya muda uliowekwa fedha zilizotumika kuweka miundombinu hiyo zinarejeshwa

Serikalini. Tatu, kuhakikisha Zanzibar inakwenda sambamba na mageuzi ya utangazaji yanayotokea duniani kila mara.

Mhe. Spika, wakati huu ambapo wananchi hawajaenea kupata ving'amuzi, Serikali imeamua ili wananchi wetu waendelee kupata matangazo ya televisheni, matangazo ya Dijitali na matangazo ya Analojia yatarushwa kwa pamoja kwa muda. Utaratibu huu ni wa gharama lakini kwa maslahi ya wananchi tumeamua kwenda nao.

CHUO CHA UANDISHI WA HABARI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Chuo cha Uandishi wa Habari ni kutoa mafunzo, ushauri na taaluma ya uandishi wa habari na tafiti kwa wanafunzi wa ngazi ya Cheti na Stashahada zinazozingatia mahitaji ya soko la ajira. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Chuo cha Uandishi wa Habari kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha ubora wa kiwango cha taaluma ya Habari itakayoendana na mageuzi ya teknolojia ya Habari duniani.
ii. Kutoa taaluma ya Uandishi wa Habari kwa taasisi za Umma na binafsi.
iii. Kuimarisha mazingira ya kazi na ya kusoma katika Chuo kwa wanafunzi.
iv. Kuimarisha utendaji kazi wa Chuo.

UTEKELEZAJI HALISI:

i. Katika kutoa taaluma bora ya uandishi wa habari Chuo kilitoa wahitimu 87, kati yao Stashahada 36 (wanawake 25 na wanaume 11) na ngazi ya Cheti 51 (wanawake 38 na wanaume 13).
ii. Chuo kimeweza kusimamia shughuli za utekelezaji wa kila siku kwa kugharamia uchapishaji wa vitabu vya ripoti ya baraza la Chuo na kuwapatia stahiki zao walimu wa muda, wafanyakazi na walinzi. Vile vile kusimamia upatikanaji wa vifaa vya ofisi, mafuta, umeme na Intaneti.
iii. Katika kusimamia upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi, Chuo kimegharamia vifaa vya kufundishia ikiwemo scana, "*Adobe creative software*" pamoja na "*printer*" 1 ya kuchapishia gazeti la Chuo ili kukuza uelewa wa mafunzo yanayotolewa.
iv. Chuo kimeandaa sheria za wafanyakazi, kanuni za sheria ya Chuo pamoja na muongozo wa matumizi ya fedha za Chuo ili shughuli za utendaji zifanyike kulingana na misingi ya sheria na miongozo iliyokubalika. Chuo kimesimamia upatikanaji wa masomo kwa wafanyakazi kwa kuwajengea uwezo wa kufanyakazi kwa ufanisi

zaidi kwa kumlipia mafunzo mfanyakazi mmoja (1) nchini China pamoja na kushiriki mkutano wa kimataifa wa madarasa ya lugha ya Kichina, (Tafadhali rejea kiambatanisho namba 3).

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Chuo kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 305,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 216,000,000/= sawa na asilimia 71. Chuo kilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 80,800,000/= na hadi kufikia Juni 2013 jumla ya shilingi 105,710,000/= zimekusanywa sawa na asilimia 131.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Chuo cha Uandishi wa Habari kimepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kuongeza wataalamu wa fani ya Habari na Mawasiliano ya umma wanaokidhi mahitaji ya soko la ajira pamoja na kuandaa mazingira bora ya kazi na kutoa huduma bora kwa wafanyakazi. Katika kutekeleza malengo hayo Chuo kimepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kukipatia Chuo kamera za kisasa mbili za digital (*steel & moving*).
ii. Kuupitia mtaala wa Chuo ili ukidhi mahitaji ya utoaji taaluma kulingana na wakati.
iii. Kukipatia Chuo mashine za kuhariria vipindi vya redio na TV na kuchapisha jarida la mafunzo ya vitendo.
iv. Kuratibu shughuli za mitihani Chuoni.
v. Kuwapatia mafunzo walimu wawili ngazi ya Shahada ya pili (*MA MASS.COM*).
vi. Kufanya mapitio na mabadiliko ya sheria ya Chuo ili kuifanya ilingane na mahitaji ya sasa na ya baadae.
vii. Kuandaa makongamano matatu ya kitaaluma juu ya tasnia ya habari na mawasiliano.

Mhe. Spika, ili kukamilisha vyema malengo ya Chuo cha Uandishi wa Habari katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, nakiombea kuidhinishiwa jumla ya shilingi 305,000,000/= na kukusanya shilingi 101,250,000/=.

SEKTA YA UTALII

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii inajumuisha Kamisheni ya Utalii, Chuo cha Maendeleo ya Utalii na Hoteli ya Bwawani. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kupanga, kusimamia, kuendeleza Utalii na kuitangaza Zanzibar ili Sekta hii iende sambamba na Sera na mikakati ya Serikali katika kufikia malengo makuu ya kuimarisha uchumi wa Taifa na kupunguza umasikini.

MALENGO YA SEKTA YA UTALII KWA MWAKA 2012/2013
KAMISHENI YA UTALII

Mhe. Spika, jukumu la Msingi la Kamisheni ya Utalii Zanzibar ni kupanga, kuratibu, kusimamia na kuendeleza shughuli za Utalii ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Kamisheni imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha mazingira ya kazi na wafanyakazi.
ii. Kuimarisha na kuongeza wigo wa vivutio vya utalii.
iii. Kutangaza utalii wa Zanzibar kitaifa na kimataifa.
iv. Kukuza shughuli za utalii ili kuwa endelevu kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na mazingira nchini.

UTEKELEZAJI HALISI:

i. Kamisheni imeweza kusimamia utekelezaji wa kazi za kila siku kwa kununua vitendea kazi kama vile vifaa vya usafi, kompyuta, mashine ya faksi, printa na televisheni pamoja na ununuzi wa mafuta, huduma za simu, *internet*, faksi. Aidha, Kamisheni imewapatia wafanyakazi stahiki zao kwa kuwapatia malipo ya likizo ili kuweza kuendesha ofisi kiufanisi.
ii. Katika kuimarisha shughuli za utalii Kamisheni imefanya matayarisho ya Mkakati wa Masoko, kupitia sera ya Utalii pamoja na kuandaa miongozo ya kamati za utalii za Wilaya.
iii. Kamisheni imewapatia wafanyakazi wake watatu (3) mafunzo ya muda mfupi nchini China na Japani. Vile vile imewapatia mafunzo ya Stashahada wafanyakazi watano (5), mfanyakazi mmoja (1) mafunzo ya shahada ya kwanza na wafanyakazi wanne (4) mafunzo ya Shahada ya Pili. Pia imeshiriki ziara ya mafunzo kwa wanafunzi katika vivutio vya Utalii, (Tafadhali rejea kiambatanisho namba 3).
iv. Kwa muda mrefu sasa Kamisheni imekuwa ikishiriki katika maonesho tafauti ya kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuitangaza nchi kiutalii. Maonesho hayo ni pamoja na Saba Saba mjini Dar es salaam, *BIT* Mjini Milan, "*World travel market"* na *ITB* Mjini Berlin. Maonesho mengine ni ya INDABA Afrika ya Kusini, *"Arabia Travel Market"* (*ATM*) Dubai pamoja maonesho ya *SMTV* Mjini Paris. Lengo la kushiriki ni kuitangaza Zanzibar na kuwavutia watalii wengi zaidi kutembelea hapa nchini pamoja na kuyaendeleza masoko hayo.
v. Jitihada nyingi zinachukuliwa katika kuwavutia watalii wengi kutembelea Zanzibar hasa wale wa daraja la kwanza. Katika jitihada

hizo ni kuweka vifaa vitakavyotumika katika kukusanya taarifa za kuweka daraja za hoteli (*Hotels inventory for classification*).

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Kamisheni iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,050,724,350/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 925,487,797/= sawa na asilimia 88. Aidha, ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,202,000,000/= katika mfuko mkuu wa Serikali na kufanikiwa kukusanya shilingi 1,055,601,195/= sawa na asilimia 88.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kamisheni ya Utalii imepanga kutekeleza malengo yake makuu matatu nayo ni kuifanya Zanzibar kuwa kituo bora cha utalii katika ukanda wa Bahari ya Hindi, kuhakikisha wananchi wengi wanashiriki katika shughuli za utalii ili kutekeleza dhana ya utalii kwa wote na kujenga mazingira bora ya kazi na kuiwezesha Kamisheni ya Utalii kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Kamisheni imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha ofisi za habari za utalii zilizopo Bandarini na Viwanja vya ndege.
ii. Kufanya ukaguzi wa miradi ya kitalii kwa lengo la kuhakiki ubora wa huduma zinazotolewa.
iii. Kuandaa mafunzo kwa watembezaji watalii juu ya utoaji wa taarifa sahihi za vivutio vya utalii.
iv. Kushiriki katika maonesho ya utalii ya Kitaifa na Kimataifa.
v. Kufanya ziara katika Visiwa vya Seychelles kwa lengo la kujifunza mbinu za utangazaji na uimarishaji wa vivutio vya utalii.
vi. Kufanya utafiti wa vivutio vipya vya utalii pamoja na uingiaji na utokaji wa wageni.
vii. Kuziwezesha kamati za utalii za Wilaya kusimamia majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, ili Kamisheni iweze kutekeleza malengo yake, naiombea iidhinishiwe matumizi ya shilingi 1,628,000,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na shilingi 100,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Aidha, Kamisheni imepanga kukusanya shilingi 1,202,000,000/= kwa ajili ya kuchangia mfuko mkuu wa Serikali kwa mwaka 2013/2014.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Spika: Wakati Mhe. Waziri anavuta pumzi kidogo, nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu tumuombee muda kwa *speed* hii anayokwenda

hatochukua muda mkubwa. Kwa hivyo, tuwekee utaratibu Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa sababu muda uliobakia hautoshi kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kumaliza hotuba yake ya bajeti, naomba Baraza lako tukufu litenge kando kanuni ya muda mpaka Mhe. Waziri atakapomaliza kusoma hotuba yake, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. Mhe. Waziri endelea.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII ZANZIBAR.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, jukumu la msingi la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar ni kutoa taaluma itakayowezesha kujenga rasilimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya kimataifa ili kuimarisha sekta ya Utalii Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha miundombinu ya Chuo ili kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi.
ii. Kuongeza idadi ya walimu 4 wenye taaluma bora, idadi ya wanafunzi 150 – 200, wafanyakazi 6 wenye utaalamu wa kisasa pamoja na kununua vifaa vya kisasa vya kusomeshea na kujifunzia.
iii. Kujenga mahusiano bora kitaifa, kikanda na kimataifa juu ya maendeleo ya taaluma ya utalii kwa kushiriki mikutano ya ndani na nje ya Zanzibar.
iv. Kushajiisha vijana wa Kizanzibari ili kuelewa dhana nzima ya utalii kwa wote.

UTEKELEZAJI HALISI:

i. Katika kuimarisha miundombinu, Chuo kimeendeleza ujenzi wa jengo la ghorofa moja la madarasa na ofisi za Chuo. Aidha, ujenzi wa vibanda vya kusomea na kupumzikia wanafunzi ambapo hivi sasa vinatumika na kuwaletea faraja kubwa wanafunzi umekamilika. Pia Chuo kimejenga ukuta kwa ajili ya kuzuia watu kupita katika

maeneo ya Chuo mara kwa mara pamoja na kuweka samani katika jengo jipya la Chuo.

ii. Katika kutoa taaluma bora ya Utalii chuo kilitoa wahitimu 223, kati yao Stashahada 44 (wanawake 20 na wanaume 24) na ngazi ya Cheti 179 (wanawake 78 na wanaume 101).

iii. Chuo kimeweza kuwapa fursa walimu ya kujiongezea taaluma zao kwa kuwapeleka masomoni walimu wawili, mmoja Shahada ya Pili katika fani ya Utalii na mwengine Shahada ya Kwanza katika fani ya Uhasibu. **(**Tafadhali rejea kiambatanisho namba 3). Aidha, kimeweka program ya kuweka kumbukumbu za wafanyakazi wa Chuo. (*Human Resource Data Base*).

iv. Ili kuwa na mbinu nzuri za kufundishia na kujifunzia, Chuo kimeweka vifaa vya maktaba kama vile rafu, "*counter*" na "*locker*" pamoja na vifaa vyengine kwa lengo la kuwawekea wanafunzi mazingira mazuri ya kujisomea.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Chuo kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 420,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 kimefanikiwa kupata shilingi 382,635,777/= sawa na asilimia 91. Pia kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 400,000,000/= kwa kazi za maendeleo na kupata shilingi 400,000,000/= sawa na asilimia 100. Chuo kilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 262,000,000/= na kufanikiwa kupata shilingi 295,000,700/= sawa na asilimia 113.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimepanga kutekeleza malengo makuu mawili: nayo ni kutoa wahitimu wenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya soko la ajira katika sekta ya utalii nchini, Afrika ya Mashariki na kwengineko na kuandaa mazingira bora ya kazi na kutoa huduma bora kwa wanafunzi na wafanyakazi. Katika kutekeleza malengo hayo Chuo kimepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kuwapatia wanafunzi moduli za kusomea stadi za mawasiliano katika shughuli za utalii (*English for Hospitality and Tourism Level I & II*).

ii. Kufanya mazungumzo na vijana wa kizanzibari kuwashajiisha kujiunga na Chuo kwa kuwaonesha shughuli mbali mbali zinazofanywa na Chuo katika Skuli 9 za Wilaya 9 za Unguja na Pemba.

iii. Kuwajengea uwezo walimu kwa kuinua viwango vyao vya taaluma, mmoja Shahada ya Kwanza fani ya Utalii na usafiri; watatu Stashahada fani ya Utalii, Ukarimu na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Mhe. Spika, ili Chuo kiweze kutekeleza malengo yake, naomba kuidhinishiwa matumizi ya shilingi 420,000,000/= kwa kazi za kawaida na kukusanya shilingi 280,000,000/=.

SHIRIKA LA UTALII

Mhe. Spika, Shirika la Utalii ni moja ya Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Aidha, kama waheshimiwa wanavyolifahamu Shirika hili, kwa kipindi kirefu hali ya kibiashara imekuwa sio nzuri kutokana na ushindani mkubwa uliopo katka sekta ya biashara ya Utalii hapa nchini.

Mhe. Spika, serikali kwa kutumia wataalamu na washauri mbali mbali, ilikuwa ikitafuta ushauri wa kitaalamu juu ya hatma ya shirika hili, ili kujua kama linaweza kuleta tija kwa taifa, na wakati huo huo ikizingatiwa changamoto kubwa inayolikabili shirika katika kushindana na sekta binafsi.

Mhe. Spika, kufuatia ushauri uliopatikana naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, serikali imeamua rasmi kulivunja Shirika la Utalii na hatua za kutekeleza maamuzi tayari zimeanza.

Mhe. Spika, zoezi la kukamilisha taratibu za kulivunja shirika tunatarajia kukamilika katika kipindi kifupi kijacho.

HOTELI YA BWAWANI

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Hoteli ya Bwawani ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea na programu yake ya kuwapatia wafanyakazi wake mafunzo ya muda mrefu na mfupi.
ii. Kuendelea kufanya matengenezo muhimu ya vyumba vya wageni na kumbi za mikutano.

UTEKELEZAJI HALISI:

i. Hoteli imeendelea na kazi ya kuviimarisha vyumba vyake kwa kuweka vigae katika vyumba vinne (4) na kufanya marekebisho madogo madogo ya vyumba pamoja na uwekaji wa waya wa mbu madirishani ili kwenda sambamba na soko la ushindani la sasa.
ii. Katika kusimamia upatikanaji wa vitendea kazi Hoteli imegharamia upatikanaji wa vifaa vya ofisini, vifaa vya usafi, mafuta ya "*petrol* na *diesel*" pamoja na kulipia ada ya masomo na likizo kwa wafanyakazi ili kuwaongezea ari ya kufanya kazi kwa bidii.

Mhe. Spika, Hoteli ya Bwawani kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 900,000,000/= na imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 826,953,622/= sawa asilimia 92 hadi kufikia Juni 2013. Aidha, hoteli katika mwaka wa fedha 2012/2013 imetumia shilingi 817,905,841/= sawa na asilimia 99 ya makusanyo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Hoteli ya Bwawani imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kupokea idadi kubwa ya wageni katika Hoteli ya Bwawani na kutoa huduma bora kwa wateja wa Kitaifa na Kimataifa. Katika kutekeleza malengo hayo Hoteli imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuitangaza Hoteli ya Bwawani kwa njia ya vipindi vya matangazo kupitia redio na televisheni, website na vipeperushi.
ii. Kuboresha huduma kwa wateja (wageni)
iii. Kuanzisha "*internet café*".
iv. Kuendesha mafunzo chini ya mshauri elekezi ya uwekaji takwimu sahihi za aina ya wageni wa Hoteli ya Bwawani.
v. Kufanya ukarabati wa vyumba 50 vya hoteli kati ya hivyo (10) vinahitaji ukarabati mkubwa na (40) ukarabati mdogo, kumbi (4) za mikutano, viyoyozi (10) katika vyumba vya hoteli na "*heaters*" (30).

Mhe. Spika, ili hoteli iweze kutekeleza malengo yake itahitaji kuidhinishiwa makusanyo ya shilingi 950,000,000/= na kutumia shilingi 841,000,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2013/2014

SEKTA YA UTAMADUNI NA MICHEZO.

Mhe. Spika, Sekta ya Utamaduni na Michezo imeundwa na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, Baraza la Kiswahili, Baraza la Sanaa, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za maonesho, *EACROTANAL* na Baraza la Taifa la Michezo. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kusimamia, kuratibu, kufufua, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za Utamaduni na Michezo Zanzibar.

KAMISHENI YA UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Spika, Majukumu ya msingi ya Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ni kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni na michezo hapa Zanzibar kwa kushirikiana na Idara na Mabaraza yaliyo chini yake. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa mkakati maalumu wa kuibua vipaji vya sanaa na michezo maskulini kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu.
ii. Kuimarisha uhifadhi na uendelezaji wa shughuli na maeneo mbali mbali ya Utamaduni.
iii. Kuweka mkakati maalumu wa kuimarisha na kuendeleza vikundi vya sanaa na Utamaduni.
iv. Kuwajengea uwezo makocha, walimu, maafisa na wataalamu wa michezo na utamaduni.
v. Kuimarisha miundombinu ya michezo katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Hatua zimechukuliwa kuimarisha vikundi vya sanaa za maonesho vya Taifa kwa kuvipatia vifaa pamoja na kuimarisha nyumba ya Sanaa ili iweze kutumika katika utoaji wa mafunzo ya sanaa kwa vijana.
ii. Timu za Taifa zimewezeshwa kushiriki mashindano ya Kimataifa kwa wanariadha watatu wa "*Special Olypmpic*" wa Zanzibar kwenda nchini Afrika ya Kusini, timu ya soka ya "*Zanzibar Heroes*" kushiriki katika mashindano ya Kagame yaliyofanyika Uganda pamoja na timu ya Jamhuri kushiriki mashindano ya klabu Bingwa Afrika.
iii. Katika kuongeza mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi na kufuatilia maendeleo ya utendaji kazi, Kamisheni imehudhuria kikao cha Afrika Mashariki nchini Uganda juu ya uanzishaji wa Kamisheni ya Kiswahili ambapo Makao Makuu ya Kamisheni hiyo yatakuwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Kamisheni iliidhinishiwa jumla ya shilingi 741,565,200/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 607,062,263/= sawa na asilimia 82.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kuendeleza shughuli za Utamaduni na Michezo nchini na kujenga mazingira bora ya kazi yenye kuleta ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Kamisheni imepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kuweka nyasi bandia Uwanja wa Amaan.

ii. Kushiriki mashindano ya kitaifa na kimataifa.
iii. Kutayarisha mpango wa maendeleo ya michezo –Zanzibar.
iv. Kuandaa Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari.
v. Kuipatia studio ya muziki na filamu vifaa vya kurikodia sauti na picha. (*video* na *sound system,digital audio mixer, power Amplifier, speakers, Active equalizer, computer system, Compressor, External hard disk, Headphone ATHAM50 na CD na memory card).*
vi. Kufanya mapitio Sera za Utamaduni na Michezo.

Mhe. Spika, ili Kamisheni ya Utamaduni na Michezo iweze kutekeleza malengo yake, naomba iidhinishiwe shilingi 1,362,204,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 80,000,000/= kwa ajili ya kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Idara hii ni kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza historia ya Zanzibar kwa kutumia makumbusho, na maeneo ya kihistoria. Pia kuelimisha jamii juu ya umuhimu na faida za matumizi ya makumbusho na mambo ya kale. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kupima na kuyapatia hati miliki maeneo ya kihistoria Unguja na Pemba.
ii. Kuimarisha majengo ya kihistoria kwa kufanya tafiti, kukusanya taarifa zake na kufanya matengenezo.
iii. Kuanzisha makumbusho mengine mapya.
iv. Kuimarisha vitengo vya ndani ya makumbusho na mambo ya kale kwa kuvipatia huduma na vitendea kazi.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Idara imeweza kuyatafiti maeneo ya kihistoria kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za kihistoria na utamaduni kwa kufanya ukaguzi wa awali wa maeneo ya kihistoria ya Salhiya, Bustani ya Salme, Nyumba ya Wareno Bambi, Pango la Kiwengwa, Kiwanda cha Sukari Cheju, Pango la Bambi, Mkamandume na Chwaka – Tumbe.
ii. Idara imefanya matayarisho ya maonesho ya kuzaliwa kwa Mvumbuzi Mashuhuri Dr. Living Stone na kununua vifaa vya kale na vya maonesho ya karne ya 21 kwa lengo la kukusanya vitu vya kale ili kupata taarifa katika uanzishwaji wa makumbusho.

iii. Katika kuzitangaza Makumbusho ndani na nje ya nchi ili kuvutia wageni na kutoa elimu kwa jamii, Idara imerikodi na kurusha hewani vipindi vya redio kupitia *ZBC* juu ya maeneo ya kihistoria ya Mji wa kale Chwaka Tumbe, Bandari Kuu kisiwani Pemba, Msikiti wa Kizimkazi, Pango la Mwanampambe lilioko Kajengwa Makunduchi, Kasri la Mtoni.

Pamoja na kuwatembeza wasanii katika maeneo ya kihistoria kama Makumbusho ya Kasri, Maruhubi, Mtoni, Kidichi, Kizimbani, Kizimkazi na Mangapwani na kufanya ziara za wanafunzi kwa lengo la kutekeleza dhana ya utalii kwa wote kwa kushirikiana na *ZBC TV* na Habari Maelezo, ambao wanasaidia kurusha taarifa hizi kupitia "*blog*" yao.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 475,358,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 100,000,000/= kwa kazi za maendeleo hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 402,618,608/= sawa na asilimia 85 kwa kazi za kawaida na shilingi 51,100,000/= sawa na asilimia 51 kwa kazi za maendeleo. Pia ilipangiwa kukusanya shilingi 210,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 116,554,201/= sawa na asilimia 56 hadi kufikia Juni 2013.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imepanga kutekeleza malengo makuu matatu nayo ni kuyaimarisha maeneo ya kihistoria ili yawe na hadhi ya Kitaifa na Kimataifa, kuvutia idadi kubwa ya wananchi na wageni ili watembelee maeneo ya kihistoria pamoja na kuandaa mazingira bora ya kazi yatakayowezesha Idara kufanya kazi kwa ufanisi. Katika kutekeleza malengo hayo Idara imepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kuhifadhi na kuendeleza maeneo matatu ya kihistoria: Chuini, Shakani Mtangani na kuyawekea uzio, maelezo ya kihistoria na kuyapatia hati miliki.
ii. Kukusanya takwimu za kiakiolojia na kuziweka katika mfumo wa taarifa kwa maendeleo ya Idara.
iii. Kutoa mafunzo kwa viongozi wa vijiji juu ya umuhimu wa uhifadhi wa maeneo ya kihistoria: Ole-Mandani, Mtangani, Chwaka-Tumbe, Fukuchani, Mangapwani, Bungi, Kuumbi na Mwanampambe.
iv. Kukusanya taarifa za kihistoria katika maeneo 20 Unguja na Pemba na kuzihifadhi kwa ajili ya kumbukumbu za vizazi vya leo na vijavyo.

v. Kuyatangaza makumbusho na mambo ya kale kwa kutengeneza, “documentary”, vipeperushi, ‘programu za Utalii kwa Wote’, kuchapisha majarida, kalenda, fulana, makala kwenye magazeti, televisheni na redio.
vi. Kufanya matayarisho ya awali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kujadili uingizwaji wa somo la ‘hifadhi ya urithi’ katika mitaala ya elimu.
vii. Kushiriki katika maonesho ya kitaifa na kimataifa.

Mhe. Spika, ili Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale iweze kutekeleza malengo yake naomba kuidhinishiwa matumizi ya shilingi 679,408,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na kukusanya shilingi 210,000,000/=.

BARAZA LA KISWAHILI:

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Kiswahili la Zanzibar ni kukuza, kushajiisha na kufuatilia matumizi na maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza hili lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kushajiisha na kuendeleza matumizi ya Kiswahili Kimkoa, Kitaifa na Kimataifa kwa kuwajengea uwezo walimu na waandishi chipukizi kwa kuwapa mafunzo na kuchapisha makala za wasanii wakongwe.
ii. Kuendeleza uandishi wa kamusi la lugha mbili: Kiswahili kwa Kiingereza.
iii. Kuanza na utafiti wa majina ya viumbe vya baharini na mazingira yao kwa lengo la kuandika Kamusi.
iv. Kuanzisha Kijarida cha Kiswahili.
v. Kuimarisha Maktaba ya BAKIZA.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza la Kiswahili limetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Katika kutoa taaluma kwa umma juu ya matumizi ya Kiswahili fasaha na kutayarisha machapisho ya kusaidia kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili, Baraza limerusha vipindi 36 vya kuelimisha Kiswahili kupitia *ZBC*, Redio na *TV*, limezindua makamusi ya lahaja za Kimakunduchi, Kipemba na Kitumbatu pamoja na kutoa mafunzo kupitia vituo vya mafunzo ya walimu (*TC*) kwa walimu wa somo la Kiswahili Unguja na Pemba.

Vile vile Baraza limechapisha Kijarida cha BAKIZA kitakachokuwa na makala zenye mada za fasihi na isimu ya Kiswahili na kulitangaza Kamusi la Kiswahili fasaha katika vyuo vikuu na katika Tamasha la Utamaduni la Afrika Mashariki.

ii. Baraza limeweza kuifanyia matengenezo maktaba yake kwa kuipatia vifaa na zana zinazohitajika kwa kutengeneza rafu ya kuwekea vitabu vya maktaba na kabati la kutilia magazeti na majarida ya Kiswahili kwa ajili ya rejea.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Baraza la Kiswahili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 95,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 52,822,000/= sawa na asilimia 56. Baraza lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 10,000,000/= na kufanikiwa kupata shilingi 2,948,900/= sawa na asilimia 29.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza la Kiswahili limepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kukuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili sahihi na fasaha Kitaifa na Kimataifa na kuweka mazingira mazuri ya kazi**.** Katika kutekeleza malengo hayo Baraza limepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kukitangaza Kiswahili kupitia machapisho ya Baraza, vyombo vya habari, vyuo vya elimu ya juu na Maonesho ya Sanaa ya Afrika ya Mashariki.
ii. Kukusanya taarifa za majina ya viumbe vya baharini na mazingira yao kwa lengo la kuandika kamusi.
iii. Kuanzisha mashindano ya uandishi wa Kiswahili katika ngazi ya Wilaya na Taifa na kuadhimisha siku ya Kiswahili.
iv. Kuandika na kuchapisha majarida, vipeperushi na vitabu na kuvisambaza ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, ili Baraza la Kiswahili Zanzibar liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naomba iidhinishiwe shilingi 95,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kuchangia shilingi 41,580,000/= kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

BODI YA SENSA YA FILAMU NA SANAA ZA MAONESHO

Mhe. Spika, jukumu la msingi la Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho ni kukagua na kuhakiki filamu na sanaa za maonesho ili

kuhakikisha kuwa haziharibu maadili ya jamii zinapooneshwa hadharani na kusikika kwenye vyombo vya habari na rekodi (*CD*, *DVD*). Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Bodi hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukagua na kuhakiki filamu na sanaa mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha haziendi kinyume na maadili yetu.
ii. Kuanzisha na kuzijengea uwezo Kamati za maadili katika Shehia zote za Unguja na Pemba. Sambamba na hatua hiyo kuzipatia mafunzo mafupi kwa njia ya semina ambayo yataziwezesha kumudu kazi yao hiyo.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Bodi imeendelea na mikakati ya ukaguzi wa filamu utakaowezesha kuiokoa jamii na wimbi la mmong'onyoko wa maadili pamoja na kutoa matangazo ya kuelimisha jamii juu ya kuenzi na kulinda maadili na kuelezea athari ya madawa ya kulevya na elimu ya maadili kwa wageni.
ii. Bodi imeendelea na uhakiki na ukaguzi wa filamu na kazi nyengine za Sanaa kutoka Tamasha la Filamu la Zanzibar (*ZIFF*), Tamasha la Busara, filamu za michezo mchanganyiko kutoka katika maduka ya kukodishia kanda na vikundi vya sanaa za maigizo Zanzibar, ili kuhakikisha haziendi kinyume na maadili yetu (Tafadhali angalia kiambatanisho namba 4).
iii. Licha ya kwamba suala la ulinzi na usimamizi wa maadili ni jukumu la kila mwanajamii pale alipo. Hata hivyo, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho imejitahidi kutekeleza wajibu wake kwani ndani ya kipindi cha mwaka wa Fedha 2012/2013 jumla ya matangaazo 6 kwa njia ya maigizo mafupi yalitayarishwa na kurushwa kwenye vyombo vya habari vya Shirika la Utangazaji la *ZBC*.

    Sambamba na hatua hiyo onesho maalumu la igizo linalojuilikana kwa jina la TUNU ZETU lenye lengo la kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuyaenzi na kuyaendeleza yale mazuri yanayotokana na mila na silka zetu limeandaliwa linatarajiwa kuoneshwa katika shehia zote za Unguja na Pemba kwa kushirikiana na Idara ya Habari Maelezo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Bodi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 38,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 25,000,000 /= sawa na asilimia 66.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Bodi ya Sensa na Filamu za Maonyesho imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kuongeza idadi na ubora wa Filamu na Sanaa za maonesho zinazozingatia mila na silka za utamaduni wa Mzanzibari na kuimarisha mazingira ya kazi na wafanyakazi ili kufanyakazi katika mazingira mazuri. Katika kutekeleza malengo hayo Bodi imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kukagua kazi za sanaa kuhakikisha kwamba zinaendana na silka na mila za utamaduni wetu.
ii. Kuandaa vipindi na michezo mifupi ya kutoa elimu kupitia *ZBC TV* na *ZBC* Redio.
iii. Kuonesha filamu maalumu ya kutoa elimu kupitia katika shehia za Unguja na Pemba hasa katika maeneo ya vijijini kwa kushirikiana na Idara ya Habari Maelezo.
iv. Kutengeneza vipeperushi vitakavyosaidia kutoa elimu kwa jamii.

Mhe. Spika, ili Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho iweze kukamilisha shughuli zake, naiombea shilingi 38,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

BARAZA LA SANAA ZANZIBAR

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Sanaa Zanzibar ni kusimamia na kuratibu maendeleo ya shughuli za Sanaa Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza la Sanaa lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia maendeleo ya sanaa na utamaduni wa Mzanzibari kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya ndani na nje ya Zanzibar.
ii. Kufanya utafiti wa sanaa zilizopotea na kutayarisha takwimu za sanaa Unguja na Pemba na kuzihifadhi.
iii. Kusimamia na kuratibu mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa watoto wa Zanzibar.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza la Sanaa limetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Baraza limetoa mafunzo kwa vikundi vya sanaa za maonesho vilivyosajiliwa na kwa watoto kuhusu dhana ya Utalii kwa wote na kufanya mashindano ya sanaa ya uchoraji kwa skuli 6 za msingi kisiwani Pemba.
ii. Baraza limesimamia utoaji wa huduma na upatikanaji wa vifaa vya ofisi kwa kununua vifaa vya kuandikia, mafuta, umeme, vifaa vya usafi na kulipia gharama za masomo kwa wafanyakazi, ili kuleta ufanisi mzuri katika kazi.
iii. Baraza linafanya utafiti wa sanaa zilizopotea ambao unaendelea.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Baraza liliidhinishiwa jumla ya shilingi 42,000,000/= kwa ajili ya kazi za kawaida na mpaka Juni 2013 limefanikiwa kupata shilingi 34,400,000/= Sawa na asilimia 82. Aidha Baraza la Sanaa lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 7,000,000/= na limeweza kukusanya shilingi 4,139,000/= sawa na asilimia 59 hadi kufikia Juni 2013.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza la Sanaa limepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni kuwafanya wananchi wengi kushiriki na kutekeleza shughuli za sanaa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kuimarisha mazingira ya kazi yatakayowezesha Baraza kufanya kazi zake kwa ubora na ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Baraza limejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuibua vipaji vya sanaa kwa watoto na vijana katika wilaya kumi za Zanzibar.
ii. Kuhamasisha wananchi kupitia vyombo vya habari na semina.
iii. Kufanya utafiti wa maendeleo ya kazi za sanaa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, ili Baraza liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliombea jumla ya shilingi 42,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 na kukusanya shilingi 7,000,000/=.

KITUO CHA AFRIKA MASHARIKI NA KATI CHA UTAFITI WA SIMULIZI ASILI NA LUGHA ZA AFRIKA (*EACROTANAL*):

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Kituo cha Afrika ya Mashariki na Kati cha Utafiti wa Simulizi Asili na Lugha za Afrika (*EACROTANAL*) kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 21,000,000/= kwa ajili ya kazi za kawaida na mpaka Juni 2013 kimefanikiwa kupata shilingi 18,000,000/= Sawa na asilimia 86.

Mhe. Spika, chombo hiki kiliundwa na kupewa jukumu la msingi la kupashana habari, kuhifadhi kumbukumbu na kuwa chanzo cha utafiti katika ngazi ya kitaifa na kimataifa kuhusu lugha za Kiafrika na simulizi asili. Wanachama wa Chombo hiki ni Burundi, Comoro, Ethiopia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Somalia, Sudan na wenyeji Tanzania. Hata hivyo, miaka mingi sasa *EACROTANAL* imekosa kuungwa mkono na wanachama wake wote isipokuwa Tanzania pekee.

Mhe. Spika, juhudi mbali mbali zimechukuliwa za kuwasiliana na nchi wanachama wa chombo hicho lakini kwa muda wote huo hakuna hata nchi moja iliyokuwa ikijibu mawasiliano hayo. Kwa kuwa Tanzania imeteuliwa kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali imeamua kubadilisha matumizi ya majengo yaliyokuwa yakitumiwa na *EACROTANAL* kuwa yawe ndio Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya hiyo.

Mhe. Spika, katika kukamilisha taratibu za kukifanya kituo cha *EACROTANAL* kuwa ni Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

i. Mkataba wa Makao Makuu suala hili limetekelezwa kwa kupelekwa barua ya maombi kwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki. Hatua iliyofikiwa ni kuwa tunasubiri vigezo vya kupata "*Headquarter Agreement*" kama vilivyotumika katika nchi za kiafrika kama vile Rwanda, ili nasi tusije tukafanya makosa ya kuacha maeneo muhimu kama vile nafasi za watendaji kazi wa Kamisheni hiyo na wanapotoka.
ii. Kuandika waraka wa kubadilisha umiliki wa majengo ya *EACROTANAL*. Tayari barua imepelekwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, hatua iliyofikiwa ni kwamba wizara inayohusika inalishughulikia suala hilo.

Mhe. Spika, wakati hatua za majengo hayo kukabidhiwa Jumuiya hiyo zinaendelea, kumekuwa na wafanyakazi waliokuwa wakitumikia kituo cha

EACROTANAL, ambao wanatakiwa kupatiwa haki zao, ili Jumuiya ya Afrika Mashariki iweze kutumia majengo hayo kwa kuajiri wafanyakazi wake watakaoshughulikia huduma zote za majengo hayo.

Mhe. Spika, ili kutimiza malengo hayo, naomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 21,000,000/= kwa ajili ya matumizi hayo.

BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO:

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Taifa la michezo Zanzibar ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza hili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha *programs* za vyama vya Michezo vya Taifa.
ii. Kutilia mkazo ushiriki wa jamii kwa kuandaa mabonanza ya michezo na mashindano ya ndani katika ngazi ya Shehia, Wilaya, Mkoa hadi Taifa.
iii. Kuimarisha vyama vya michezo katika ngazi zote kwa kuvipatia vifaa vya michezo.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Baraza limeweza kusimamia chaguzi za vyama vya Michezo, uchaguzi wa Chama cha Mpira wa Pete (CHANEZA) pamoja na uchaguzi wa Chama cha Mpira wa Kikapu (BAZA) ili kuwa na vyama vyenye uongozi imara na kwa muda unaokubalika, aidha taratibu za uchaguzi wa Chama cha Riadha zinaendelea vyema pamoja na vyama vyengine.

ii. Katika kusaidia programu za vyama vya michezo, Baraza limesaidia kukaa kambi mwalimu wa Chama cha michezo cha watu wenye ulemavu wa akili (*SOZ*), mashindano ya Judo Afrika Mashariki na Kati, "Zanzibar Goju-ryu Karatedo" Pemba, mashindano ya kombati – karati Pemba, mashindano ya marathon kwa walemavu, mashindano ya mchezo wa mpira wa mikono pamoja na nauli kwa viongozi na wachezaji kushiriki katika mashindano mbali mbali kama vile (COPA COCA COLA) ili kuimarisha maendeleo ya michezo nchini. (Tafadhali angalia kiambatanisho namba 5).

iii. Katika kuvipatia vyama vya michezo vifaa vya kisasa vya michezo, Baraza la Taifa la Michezo kwa kushirikiana na "Save the Children", kupitia mpango wa "One World Football for All", limeweza kuwapatia vijana wetu mipira 20,000 ambayo imeshasambazwa Unguja na Pemba pamoja na kugharamia vifaa vya mchezo wa mpira wa miguu kwa timu za Pemba na usafirishaji wa vifaa vya Chama cha wanyanyua vitu vizito (ZAWEA) kutoka Nairobi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013. Baraza liliidhinishiwa jumla ya shilingi 147,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2013 imefanikiwa kupata shilingi 60,000,000 sawa na asilimia 41.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza la Taifa la Michezo limepanga kutekeleza malengo makuu mawili ambayo ni kuimarisha shughuli za michezo kwa kuongeza ushiriki na ushindi katika mashindano ya kimataifa na kitaifa pamoja na kuandaa mazingira bora ya kazi yatakayowezesha Baraza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Baraza limepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kuchangia upatikanaji wa vifaa vya michezo kwa vyama 10 vya michezo.
ii. Kutoa mafunzo kwa walimu na waamuzi wa michezo 10 (Mpira wa Miguu, Mikono, Pete, Wavu, Meza, Kikapu, Magongo, Mchezo wa kuogelea, Judo na Riadha).
iii. Kutoa zawadi kwa wanamichezo waliofanya vizuri katika michezo ya kitaifa na kimataifa.
iv. Kusaidia uanzishaji wa viwanja vinne (4) vya michezo katika Wilaya ya Micheweni, Mkoani, Magharibi na Kusini Unguja.
v. Kusaidia uendeshaji wa mashindano ya ndani kwa vyama 10 vya michezo.
vi. Kuandaa Mashindano ya Michezo ya Watoto na Vijana chini ya umri wa miaka 21.
vii. Kusimamia Mashindano ya Michezo ya Watu Wenye Ulemavu.

Mhe. Spika, ili Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliombea kuidhinishiwa shilingi 147,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

SHUKRANI

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza Hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Shukurani maalumu ziwaendee

Mhe. Naibu Waziri Bi Hindi Hamad Khamis , Katibu Mkuu Dk. Ali Saleh Mwinyikai, Naibu Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Nd. Ramadhan Feruzi, Naibu Katibu Mkuu Nd. Issa Mlingoti, Afisa Mdhamini Pemba Nd. Ali Nassor, Wakurugenzi, Wakuu wengine wa Taasisi za Wizara na wasaidizi wao wote kwa kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Kwa kweli wamekuwa wakinisaidia sana kutekeleza majukumu yetu. Pia nawashukuru Wenyeviti wa Mabaraza na Bodi mbali mbali kwa kusimamia vyema taasisi zetu na kunishauri kwa busara. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru wafanyakazi, wanamichezo, wasanii, wadau wa Utalii na wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa mchango wao katika kufanikisha shughuli za wizara. Aidha naomba nishukuru nchi mbali mbali na mashirika ya kimataita kwa misaada yao kwa wizara yangu.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuishukuru Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ushirikiano mkubwa iliyotupa kila tulipoikabili kwa mahitaji ya fedha, hasa katika hali ya dharura.

Mhe. Spika, mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na wasaidizi wako wote Mhe. Naibu Spika na Wenyeweviti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa kunisikiliza kwa utulivu na uvumilivu.

Aidha naomba kuishukuru sana Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji, Habari na Utalii na Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*), kwa michango mikubwa inayoipatia wizara baada ya kupitia taasisi zetu na kuona utekelezaji wa majukumu ya wizara. Hii imetusaidia sana katika kuweka vizuri bajeti ya wizara. Aidha, natanguliza shukurani zangu kwa Wajumbe wote kwa michango yao watakayoitoa katika kujadili hotuba hii.

Mhe. Spika, sasa naliomba Baraza lako tukufu kujadili kwa kina matumizi ya shilingi 9,985,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 510,000,000/= kwa kazi za maendeleo kwa ajili ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2013/2014.

Aidha, naliomba Baraza lako liidhinishe makusanyo ya mapato ya shilingi 1,522,580,000/= kwa fedha zinazoingia katika Mfuko wa Serikali (Hazina). Pia makusanyo ya shilingi 2,111,250,000/= ambazo taasisi za wizara hukusanya na imeruhusiwa kutumia kwa ajili ya uendeshaji wa taasisi zake.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa nawaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili, watushauri, watuelekeze na baadaye watupitishie bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Namba 1 A: Fedha zilizoingizwa Julai 2012 hadi Juni 2013 kwa matumizi ya kawaida

	IDARA	MAELEZO	FEDHA ZILIZOTENGWA	FEDHA ZILIZOPATIKANA	ASILIMIA %
1	Afisi Kuu Pemba	Mishahara	462,700,000	307,970,377	67%
		Matumizi Mengineyo	182,960,000	132,223,703	72%
	JUMLA		**645,660,000**	**440,194,080**	**68%**
2	Mipango, Sera na Utafiti	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineyo	72,135,000	66,200,000	92%
	JUMLA		**72,135,000**	**66,200,000**	**92%**
3	Uendeshaji na Utumishi	Mishahara	605,320,000	541,167,130	89%
		Matumizi Mengineyo	505,750,000	438,667,290	87%
	JUMLA		**1,111,070,000**	**979,834,420**	**88%**
4	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Mishahara	1,234,030,000	1,152,513,696	93%
		Matumizi Mengineyo	621,000,000	319,566,450	51%
	JUMLA		**1,855,030,000**	**1,472,080,146**	**79%**
5	Habari Maelezo	Mishahara	163,630,000	141,866,476	87%
		Matumizi Mengineyo	85,920,000	56,430,000	66%
	JUMLA		**249,550,000**	**198,296,476**	**79%**
6	Shirika la Magazeti ya Serikali	Mishahara	177,561,000	176,643,151	99%
		Matumizi Mengineyo	678,439,000	421,637,270	62%
	JUMLA		**856,000,000**	**598,280,421**	**70%**
7	Chuo cha Uandishi wa Habari	Mishahara	154,800,000	154,800,000	100%
		Matumizi Mengineyo	150,200,000	61,200,000	41%
	JUMLA		**305,000,000**	**216,000,000**	**71%**
8	Tume ya Utangazaji	Mishahara	100,351,000	99,009,664	99%
		Matumizi Mengineyo	67,649,000	44,300,000	65%

	JUMLA		**168,000,000**	**143,309,664**	**85%**
9	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	Mishahara	336,000,000	325,735,777	97%
		Matumizi Mengineyo	84,000,000	56,900,000	68%
	JUMLA		**420,000,000**	**382,635,777**	**91%**
10	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	Mishahara	517,000,000	429,226,888	83%
		Matumizi Mengineyo	206,010,200	164,830,375	80%
	JUMLA		**723,010,200**	**594,057,263**	**82%**
11	Bodi ya Sensa	Mishahara	10,800,000	-	0%
		Matumizi Mengineyo	27,200,000	25,000,000	92%
	JUMLA		**38,000,000**	**25,000,000**	**66%**
12	Makumbusho	Mishahara	334,320,000	314,737,608	94%
		Matumizi Mengineyo	107,878,000	80,000,000	74%
	JUMLA		**442,198,000**	**394,737,608**	**89%**
13	Baraza la Kiswahili	Mishahara	18,822,000	18,822,000	100%
		Matumizi Mengineyo	76,178,000	34,000,000	45%
	JUMLA		**95,000,000**	**52,822,000**	**56%**
14	Baraza la Sanaa	Mishahara	13,200,000	11,400,000	86%
		Matumizi Mengineyo	28,800,000	23,000,000	80%
	JUMLA		**42,000,000**	**34,400,000**	**82%**
15	Eacrotanal	Mishahara	-	-	
		Matumizi Mengineyo	21,000,000	18,000,000	86%
	JUMLA		**21,000,000**	**18,000,000**	**86%**
16	Baraza la Michezo	Mishahara	22,998,000	18,000,000	78%
		Matumizi Mengineyo	124,002,000	42,000,000	34%
	JUMLA		**147,000,000**	**60,000,000**	**41%**
17	Shirika la Utangazaji Pemba	Mishahara	111,194,000	110,282,220	99%
		Matumizi Mengineyo	50,000,000	29,495,000	59%
	JUMLA		**161,194,000**	**139,777,220**	**87%**
18	Habari Maelezo Pemba	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineyo	17,950,000	8,073,000	45%
	JUMLA		**17,950,000**	**8,073,000**	**45%**
19	Makumbusho Pemba	Mishahara	-	-	-

		Matumizi Mengineyo	33,160,000	7,881,000	24%
	JUMLA		**33,160,000**	**7,881,000**	**24%**
20	Kamisheni ya Utamaduni Pemba	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineyo	18,555,000	13,005,000	70%
	JUMLA		**18,555,000**	**13,005,000**	**70%**
21	Kamisheni ya Utalii	Mishahara	415,942,000	412,157,300	99%
		Matumizi Mengineyo	634,782,350	413,330,497	81%
	JUMLA		**1,050,724,350**	**925,487,797**	**88%**
	JUMLA KUU		**8,424,294,550**	**6,770,071,872**	**80%**

Kiambatanisho Namba 1 B: Fedha zilizoingizwa Julai 2012 hadi Juni 2013 kwa kazi za Maendeleo

	Fedha zilizotengwa hadi April kwa Miradi	**Matumizi ya**	**Bajeti**	**Matumizi**	**Asilimia %**
1	Strengthening of Institute of Tourism **SMZ**	Development	400,000,000	400,000,000	100%
2	Multiplex Operator	Development	100,000,000	56,986,215	57%
3	Rehabilitation and Cons of Monuments **SMZ**	Development	100,000,000	51,100,000	51%
	JUMLA KUU		**600,000,000**	**508,086,215**	**85%**

Kiambatanisho Namba 1C: Fedha zilizokusanywa Julai 2012 hadi Juni 2013.

Idara	Fedha zilizopangwa kukusanywa	Fedha zilizokusanywa	Asilimia %
Shirika la Utangazaji (ZBC)	280,700,000	210,326,283	75%
Idara ya Habari	15,500,000	15,037,500	97%

Maelezo			
Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	210,000,000	116,554,201	56%
Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	17,000,000	7,087,900	42%
Kamisheni ya Utalii	1,202,000,000	1,055,601,195	88%
Tume ya Utangazaji	33,000,000	45,142,000	137%
JUMLA	1,758,200,000	1,449,749,079	82%

Kiambatanisho Namba 1D: Fedha zilizokusanywa na Taasisi ambazo zimepewa uwezo wa kutumia makusanyo yake, katika kipindi cha julai 2012 hadi Juni 2013.

SNO.	TAASISI	FEDHA ZILIZOPANGWA KUKUSANYWA	FEDHA ZILIZOKUSANYWA	ASILIMIA %
	Chuo cha Uandishi wa Habari	80,800,000	105,710,000	131%
	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	262,000,000	295,000,700	113%
	Hoteli ya Bwawani	900,000,000	826,953,622	92%
	Shirika la Magazeti ya Serikali	500,000,000	404,454,233	81%
	JUMLA	**1,742,800,000**	**1,632,118,555**	**94%**

Kiambatanisho Namba 2: Makadirio ya Makusanyo kwa Taasisi ambazo zimepewa uwezo wa kutumia makusanyo yake, kwa mwaka 2013/2014.

S/NO.	TAASISI	MAKUSANYO
1.	Shirika la Utangazaji	280,000,000
2.	Shirika la Magazeti ya Serikali	500,000,000
3.	Chuo cha Uandishi wa Habari	101,250,000
4.	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	280,000,000
5.	Hoteli Ya Bwawani	950,000,000
	JUMLA	**2,111,250,000**

Kiambatanisho Namba 3: Wafanyakazi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambao wamekwenda masomoni kwa mwaka 2012/2013

NAM	JINA KAMILI	JIN	TAASISI	FANI	KIWANGO
1	Joseph John Kilangi	Mume	U na Utumishi	Public Administration	Shahada 2
2	Idd Said Haji	Mume	U na Utumishi	Uongozi wa Fedha	Shahada 2
3	Khamisuu Hamid Moh'd	Mkee	U na Utumishi	Utawala	Shahada 2
4	Zaynab Ibrahim Ali	Mke	U na Utumishi	Mawasiliano ya Habari na Uhasibu	Stashahada 2
5	Mafunda Omar Ramadhan	Mke	U na Utumishi	Mawasiliano ya Habari na Uhasibu	Stashahada 1
6	Fatma Abdalla Suleiman	Mke	U na Utumishi	Ukatibu Muhtasi	Cheti
7	Thabit Ali Nassor	Mume	Mipango, Sera na Utafiti	Project Planning	Stashahada
8	Arkam Khamis Mtumweni	Mke	Tume ya Utangazaji Pemba	Uhasibu	Stashahada
9	Makame Foum Makame	Mume	ZBC	Uhasibu	Stashahada
10	Hasina Hamad Rajab	Mke	U na Utumishi Pemba	Utawala	Stashahada
11	Khadija Kombo Khamis	Mume	ZBC	Uandishi wa Habari	Stashahada
12	Mchanga Haroub Shehe	Mke	ZBC	Uandishi wa Habari	Stashahada
13	Marzouk Khamis Sharif	Mume	H/ Maelezo	Uandishi wa Habari	Stashahada
14	Zuweina Shaaban Maalim	Mke	ZBC	Uandishi wa Habari	Stashahada
15	Mwamini Khamis Juma	Mke	U na Utumishi Pemba	Uhudumu	Cheti
16	Raya Abdu Shomar	Mke	K/Utamaduni na Michezo Pemba	Uhudumu	Cheti

17	Ahadi Saleh Khamis	Mume	K/Utamaduni na Michezo Pemba	Utunzaji Kumbukumbu	Cheti
18	Atuu Said Hassan	Mke	ZBC Pemba	Utunzaji Kumbukumbu	Cheti
19	Fatma Moh'd Suleiman	Mke	ZBC Radio	Uandishi	Stashahada
20	Mussa Nyange Suleiman	Mume	ZBC Radio	Electronic & Telecom Engineering	Shahada 1
21	Asya Suleiman Mgeni	Mke	ZBC Radio	Computer Science	Shahada 1
22	Juma Kitwana Omar	Mume	ZBC Radio	Electronic & Telecom Engineering	Stashahada
23	Ali Shaaban Ali	Mume	ZBC RADIO	IT	Cheti
24	Asha Ali Abdalla	Mke	ZBC TV	Public Administation	Cheti
25	Maryam Haji Foum	Mke	ZBC TV	Public Administation	Cheti
26	Maryam Mtumwa Juma	Mume	ZBC TV	Secretay	Stashahada
27	Aisha Mohamed Khamis	Mke	ZBC TV	Uhasibu	Stashahada
28	Mwasiti Zam Bundala	Mke		Uandishi wa Habari	Stashahada
29	Rukia Ali Miraji	Mke	ZBC TV	Record Management	Cheti
30	Hamida Said Kassim	Mke	ZBC TV	Computer Science	Shahada 1
31	Khadija Abdalla Juma	Mke	ZBC TV	Computer Science	Shahada 1
32	Thani Lali Mfamau	Mume	ZBC TV	IT	Diploma
33	Riziki Stanley Dandaroo	Mke	ZBC TV	Uandishi wa Habari	Stashahada
34	Khadija Muhidin Mahmoud	Mke	ZBC TV	Uandishi wa Habari	Stashahada
35	Maryam Ame Chum	Mke	ZBC TV	Development Studies	Shahada 1
36	Mwanajuma Said Alawi	Mke	ZBC TV	Uandishi wa Habari	Stashahada
37	Sbetuu Amour Said	Mke	ZBC TV	Uandishi wa Habari	Stashahada
38	Omar Ahmed Khamis	Mume	ZBC TV	Uandishi wa Habari	Stashahada
39	Juma Moh'd Salum	Mume	H/ Maelezo	International Politics	Phd
40	Idd Haji Issa	Mume	H/ Maelezo	Uandaaji wa Filam	Stashahada
41	Jamila Moh'd Juma	Mke	H/ Maelezo	Public Policy	Shahada 2

42	Ramadhan Makame Suleiman	Mume	Shirika la Magazeti	Mass Communication	Shahada 2
43	Asha Ali Omar	Mke	Shirika la Magazeti	Uhudumu	Cheti
44	Mwanaimani Rashid Ismail	Mke	Shirika la Magazeti	Information Technology	Stashahada
45	Ali Jaku Ali	Mume	K/Utalii	Utalii	Shahada 2
46	Abass Haji Abdalla	Mume	K/Utalii	Ugavi na Manunuzi	Shahada 2
47	Nassra Ali Salimu	Mke	K/Utalii	Uhasibu na Uwekezaji	Shahada 2
48	Khalfan Moh'd Ali	Mume	K/Utalii	Archeology on Tourism	Shahada1
49	Hamad Amini Ali	Mume	K/Utalii Pemba	Hoteli na Biashara	Stashahada
50	Fatma Juma Said	Mke	K/Utalii Pemba	Hoteli na Biashara	Stashahada
51	Hadia Assaa Hamad	Mke	K/Utalii Pemba	Hoteli na Biashara	Stashahada
52	Moh'd Nassor Hamad	Mume	K/Utalii	Uhusiano wa Kimataifa	Stashahada
53	Abdalla Mwarab Khalfan	Mume	ZITOD	Travel & Tourism	Shahada1
54	Nadhir Saleh Ali	Mume	ZITOD	Ict & Accouting	Stashahada
55	Ame Makame Ame	Mume	ZITOD	Utawala wa Hoteli	Stashahada
56	Suleiman Haji Mzee	Mume	ZITOD	Utawala wa Hoteli	Stashahada
57	Khalid Abdul Ameir	Mume	ZITOD	HRM	Shahada 2
58	Farashuu Mussa Skuni	Mke	ZITOD	Financial Accounting	Shahada 2
59	Mbarouk Nassor Said	Mume	ZITOD	Record Management	Cheti
60	Suleiman Juma Mussa	Mume	ZITOD	Nabe Stage I	Cheti
61	Asila Haji Abass	Mke	K/Utamaduni na Michezo	BIT	Stashahada
62	Jamila Moh'd Haji	Mke	K/Utamadun	ICT & Accouting	Stashahada

			i na Michezo		
63	Maryam Juma Baiya	Mke	K/Utamaduni na Michezo	BIT	Stashahada
64	Maryam Kheir Baraka	Mke	K/Utamaduni na Michezo	Human Resource	Stashahada
65	Mustafa Omar Abdalla	Mume	K/Utamaduni na Michezo	International Relation	Shahada 2
66	Rahma Abdalla Awadh	Mke	K/Utamaduni na Michezo	Secretay Study	Cheti
67	Safia Ahmada Ismail	Mke	K/Utamaduni na Michezo	Secretay Study	Cheti
68	Maryam Malik Ali	Mke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Record Management	Stashahada
69	Juma Khamis Jasho	Mume	Makumbusho na Mambo ya Kale	Public Administration	Stashahada
70	Dawa Nyange Makame	Mke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Public Administration	Stashahada
71	Hanifa Abdalla Abdulkadir	Mke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Procurement and Supply	Stashahada
72	Ali Kombo Denge	Mume	Makumbusho na Mambo ya Kale	Social Work	Stashahada
73	Saleh Yussuf Mnemo	Mume	ZJMMC	Mawasiliano ya Kimataifa	Shahada 2
74	Khamis Juma Abdalla	Mume	ZJMMC	Elimu, Sera na Uongozi	Shahada 2

Kiambatanisho Namba 4: Filamu zilizokaguliwa 2012-2013

S/NO	Kazi zilizo kaguliwa	Idadi	Zilizo kubaliwa	Zilizo kataliwa	Zilizo rekebishwa
1.	Filamu mchanganyiko	1,152	1,150	2	-
2.	Rasimu za michezo ya kuigiza	3	3	-	2
3.	Maonesho ya Muziki	1	1	-	-
4.	Michezo ya kuigiza	10	10	-	3
5.	Tenzi zenye maudhui tofauti	7	7	-	1
6.	Ngoma za Asili	4	4	-	-
7.	Mashairi ya nyimbo za Taarab	13	13	-	-
	JUMLA	**1,190**	**1,190**	**2**	**6**

Kiambatanisho Namba 5. : Mashindano mbali mbali kwa timu za Zanzibar zilizoshiriki.

S/NO	MASHINDANO	MCHEZO	NCHI	MWEZI	MAE
1.	Mashindano ya klabu bingwa	Mpira wa mikono	Zanzibar	Februari 2013	Timu z wanau ushind
2.	Mashindano ya klabu bingwa	Mpira wa miguu	Zanzibar	April 2013	KMK
3.	Mapinduzi Cup	Mpira wa miguu	Zanzibar	Januari 2013	Timu y kufika
4.	Muungano Cup	Mpira wa mikono	Tanzania Bara	April 2013	Timu y
5.	Muungano Cup	Mpira wa wavu	Tanzania Bara	April 2013	Timu y mshin
6.	Kilimanjaro Marathon	Riadha	Tanzania Bara	Februari 2013	Zanzib kupata
7.	Mashindano ya CECAFA	Mpira wa miguu	Uganda	Disemba 2012	Timu y nafasi
8.	Mashindano ya Afrika Mashariki na Kati	JUDO	Zanzibar	Machi 2013	Zanzib
9.	Mashindano ya Vijana Afrika Mashariki na Kati	Riadha	Arusha	June 2013	Zanzib

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, ahsante sana kwa kuwasilisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yako na umetumia saa moja na dakika kumi kama ulivyoniambia, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, naomba nikushukuruni na nyinyi, na sasa naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 23/07/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 8:20 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 23/07/2013 saa 3:00 asubuhi)